

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Nne – Tarehe 3 Aprili, 2020

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

(Maswali yafuatayo yaliulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)

Na. 25

Kuwahamisha Wakulima kwenye Maeneo ya Mjini

MHE. RITTA E. KABATI aliuliza:-

Je Serikali inatumia sheria gani kuwahamisha wakulima kwenye maeneo ya mijini?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji, Na.8 ya mwaka 2017 na Sheria ya Ardhi, Na.4 ya mwaka 1999, Serikali haihamishi wakulima kwenye maeneo ya mijini badala yake inazuia wananchi kujihusisha na shughuli za kilimo cha mazao marefu katika maeneo hayo. Aidha, mazao mafupi kama kilimo cha mazao ya mikunde yanaruhusiwa kulimwa maeneo ya mijini kwa kuzingatia Sheria ya Mipango Miji.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, ni kwa nini miji inapopanuliwa maeneo ya mashamba ya mazao marefu yasiachwe mijini kama ilivyo katika nchi nyingine kama Malaysia ambapo kilimo cha michikichi na mazao mengine kinaendeshwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, sheria hiyo haihusishi baadhi ya Mikoa kama Kagera, Kilimanjaro na Arusha ambako wakulima wanaendelea kulima mijini mazao marefu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kama nilivyotoa majibu ya swali la msingi, Serikali huwahamisha wakulima wa mazao ya aina zote kwenye maeneo ya mijini yaliyoiva kwa ajili ya ukuaji au uendelezaji wa miji kwa kuzingatia Sheria ya Mipango Miji, Na. 8 ya 2007 (Kifungu cha 7 na Kifungu cha 28 na Kanuni zake za mwaka 2008. Sheria hii hutumika kwa pamoja na Sheria ya Utwaaji wa Ardhi, Na. 47 ya 1967; Sheria ya Ardhi, Na. 4 ya 1999 na Sheria ya Upimaji na Ramani, Sura ya 324 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, hivyo, sheria za nchi yetu zinazohusika na usimamizi wa uendelezaji wa miji haziruhusu

uwepo wa mashamba ya mazao marefu mijini isipokuwa sheria hizo zinaruhusu kilimo cha mijini (*urban farming*) cha mazao mafupi yaslyozidi urefu wa mita moja hususan kilimo cha mboga mboga.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, sheria tajwa katika majibu niliyoyatoa katika swali la kwanza la nyongeza hapo juu zinatumika katika maeneo yote ya nchi yetu ya Tanzania na hivyo sheria hizi hazitumiki kwa kubagua baadhi ya mikoa fulani ya Tanzania. Sehemu kubwa ya mazao marefu yanayolimwa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Kagera ambayo ni kahawa, migomba na miparachichi yana sifa ya kuhifadhi mazingira na kupendezesha mandhari ya miji na makazi kama ilivyo kwa miti ya vivuli na matunda.

Na. 26

Miongozo ya Fedha kwa Halmashauri

MHE. RICHARD P. MBOGO aliuliza:-

(a) Je, kuna miongozo ya fedha mingapi inayoitaka Halmashauri kutenga fedha za ndani kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo?

(b) Je, ni halali kuwepo miongozo zaidi ya mmoja ukizingatia kuwa sasa Halmashauri hazina ruzuku?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, usimamizi wa fedha kwenye Halmashauri unafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Kifungu cha 37 na Kifungu cha 68 vinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana na Serikali za

Mitaa kutoa miongozo ya usimamizi wa fedha katika Serikali za Mitaa.

(b) Mwongozo wa mgawanyo wa mapato ya ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na Matumizi ya Kawaida umezingatia uwezo wa Halmashauri kukusanya mapato ambapo Halmashauri zenyne mapato makubwa zinachangia asilimia 60 ya mapato yake kwa ajii ya Miradi ya Maendeleo na Halmashauri zenyne mapato kidogo zinachangia asilimia 40 ya mapato yake kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Na. 27

Hatma ya Eneo la Jimbo la Mchinga

MHE. HAMIDU H. BOBALI aliuliza:-

Mheshimiwa Rais amefanya marekebisho ya jina na mipaka ya iliyokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Lindi na sasa kuna Halmashauri mpya ya Mtama inayojumuisha eneo lote la Jimbo la Mtama:-

Je, nini hatma ya eneo lililobaki la Jimbo la Mchinga ambalo hapo awali Lilikuwa ipo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Lindi kama ilivyo kwa Jimbo la Mtama?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatia agizo la Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuhamishia Halmashauri ya Wilaya ya Lindi katika Jimbo la Mtama na Jimbo la Mchinga kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI inaendelea na uhakiki wa mipaka ili kundaa Tangazo la Serikali la kurekebisha mipaka ya Halmashauri hizo. Zoezi hilo

linafanyika sambamba na maeneo mengine yaliyotangazwa na Mheshimiwa Rais ili kuboresha utoaji huduma kwa wananchi.

Na. 28

Tatizo la Maji Bukoba

MHE. JASSON S. RWEIKIZA aliuliza:-

Serikali ilishasema kwamba itatoa fedha ili maji yanayozalishwa na Mradi wa Maji *BUWASA* (*Bukoba Water Supply and Sanitation Authority*) yaweze kufika vijijini katika Kata za Maruku, Kanyangero, Kabaragaine, Katoma na Nyakato:-

Je, ni lini mradi huu utaanza kutekelezwa?

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wananchi wa Manispaa ya Mji wa Bukoba wanapata huduma ya majisafi na salama, mwaka 2016, Serikali ilikamilisha ujenzi wa mradi mkubwa wa maji. Aidha, baada ya kukamilisha mradi huo, Serikali imetoa fedha kwa ajili ya upanuzi wa mtandao wa maji ili wananchi wa maeneo ya Kata za Kibeta, Kagondo, Ijuganyundo na baadhi ya maeneo ya kata za Kahororo, Kashai, Nshambya na Nyaga waweze kunufaika kupitia mradi huo. Kwa sasa upanuzi huo umefikia asilimia 95. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kupeleka maji katika Kata za Maruku, Kanyangereko na Karabagaine.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kata ya Katoma, Wizara kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*RUWASA*) imefanya usanifu ili kutumia Mto Kyeiringisa kama

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

chanzo cha maji katika eneo hilo na Kata ya Nyakato itanufaika kupitia upanuzi wa awamu ya pili ya mtandao wa maji wa mradi mkubwa wa Manispaa ya Bukoba.

Na. 29

Leseni Inayotumiwa na *Garda World*

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO aliuliza:-

Mnamo tarehe 20 Mei, 2019 Kampuni ya *Ultimate Security* ilizwa kwa asilimia mia moja kwa kampuni ya *Garda World* nchini Canada.

Je, Kampuni ya *Garda World* inatumia leseni ya kampuni ya ulinzi ya *Ultimate Security* au imeomba kubadili leseni ili isomeke kampuni mpya?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Alhaji Abdallah Majura Bulembo, Mbunge wa Kuteuliwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Kampuni ya *Garda World* ya Canada imeinunua Kampuni ya Ulinzi ya *Ultimate Security*. Aidha, kwa kuwa *Garda World* imeinunua *Ultimate Security* kwa asilimia mia moja na kwa kuwa kibali cha *Ultimate Security* bado kipo hai, *Garda World* wanaendelea kukitumia kwa mujibu wa taratibu na kanuni zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa jina la *Garda World* linatumika kama chapa (*brand*) ya kibashara tu na limesajiliwa BRELA kama taratibu zinavyoelekeza.

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, ni kanuni namba ngapi zinazoelekeza kampuni ikiuzwa asilimia mia iendelee

kutumia kibali cha kampuni nyingine na jina tofauti la kampuni nyingine?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa nini *brand* ya *Garda World* tumike kama nembo badala ya kutumika kama kampuni nyingine na kwa hali hii hamuoni haki za watumishi wa kampuni ya zamani zinapotea kwa kuhalalishwa na Serikali yenye?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu Maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Alhaj Abdallah Majura Bulembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa usahihi kilichouzwa ni hisa. Hivyo wamiliki wa hisa wamebadilika lakini kampuni inabaki kama ilivyo. Hivyo *Ultimate Security Company* iko palepale, kwa usajili uleule na watumishi walewale na mikataba yake ileile na mali zake zote na vibali vyake vilevile na biashara yake yote. Hivyo uhalali wa kutumia vibali unapatikana na sheria iliyotumika ni *Companies Act, No. 12* kama ilivyorejewa *2002, Cap. 212, section 74 - 83*. Hicho kinachoitwa jina lingine ni "*brand name*" ambalo inaruhusiwa chini ya Sheria ya *Trade Marks, No. 12* ya 1986, *Cap. 326* na *Trade Mark* hiyo imesajiliwa na *BRELA* chini ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, haki za watumishi zinabaki kama zilivyo na kilichonunuliwa ni hisa. Hivyo, kampuni na vyote vilivyomo ikiwa ni pamoa na watumishi na haki zao zinabaki kama zilivyo kwa mujibu wa mikataba yao.

Na. 30

Ukarabati wa Gereza Kuu la Kitai

MHE. MARTIN M. MSUHA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Gereza Kuu Kitai liliopo Wilaya Mbanga?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Martin Msuha, Mbunge Wa Mbinga Vijijiini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Gereza Kuu Kitai ni miongoni mwa Magereza ya wazi liliojengwa kwa lengo la shughuli za kilimo na mifugo. Hata hivyo, Serikali inatambua tatizo la uchakavu hususani uzio wa Gereza uliozungushiwa kwa waya (*Barbed Wire Fence*) na nguzo za miti ambazo zimekuwa zikishambuliwa mara kwa mara na mdudu mchwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutambua tatizo la uchakavu huo, Serikali ina mpango wa kuyafanya ukarabati mkubwa majengo na miundombinu ya magereza nchini likiwemo Gereza Kuu Kitai kwa kuzungushia Uzio kwa tofali na ukarabati wa mabweni ili kuboresha huduma za wafungwa na mahabusu.

Mheshimiwa Spika, aidha, ukarabati na uboreshaji wa miundombinu hiyo imepangwa kutekelezwa kwa awamu kwa kutegemea na upatikanaji wa rasilimali fedha.

Na. 31

Hitaji la Vyuo vya Serikali Geita

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA aliuliza:-

Mkoa wa Geita hauna Chuo cha Serikali hata kimoja:-

Je ni lini Serikali itajenga Vyuo Mkoani Geita ikiwemo vya Afya na Madini?

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa elimu inayotolewa katika ngazi ya vyuo katika kujenga ujuzi unaochochea maendeleo kwa jamii na Taifa kwa ujumla. Hivyo, ni azma ya Serikali kujenga na kuboresha vyuo vilivyopo katika mikoa mbalimbali nchini ili viweze kutoa elimu bora kwa wanafunzi wengi zaidi. Kwa sasa mkoa huu una Chuo Kimoja cha Serikali cha Uuguzi ngazi ya katи (*Geita School of Nursing*). Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa vyuo vingine viwili vya VETA. Wizara pia imepokea maombi kutoka Halmashauri ya Mji wa Geita ya kukabidhi Chuo cha Ujasiliamali kiitwacho Magogo ili kiwe chini ya Mamlaka ya Ufundı Stadi (*VETA*). Serikali imeridhia ombi hilo na taratibu za makabidhiano zinaendelea. Kwa kuwa vyuo hivi vimezungukwa na migodi, pamoja na fani zingine, Serikali itaangalia pia uwezekano wa kuanzisha fani ya madini.

Mheshimiwa Spika, Mkoaa wa Geita pia kuna tawi la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambacho hutoa masomo kwa ngazi ya elimu ya juu. Kwa kuwa masomo ya ngazi ya elimu ya juu ni suala la kitaifa, kwa sasa wananchi wa Geita wanashauriwa kuendelea kutumia vyuo vikuu vingine vilivyopo nchini.

Na. 32

Kufanya Maboresho Mfumo wa Elimu

MHE. ZAINAB A. KATIMBA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufanya maboresho Mfumo wa Elimu Tanzania?

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, suala la uboreshaji wa utoaji wa elimu katika nchi yoyote ni endelevu, ambalo hutegemea

mabadiliko yanayotokea katika nchi kwenye nyanja za kiuchumi na kijamii, pamoja na ulinganisho wa maendeleo ya sayansi na teknolojia. Katika nchi yetu, suala hili la uboreshaji wa mifumo ya elimu limekuwa likifanyika na hutegemea tathmini mbalimbali za kitaalamu zinazofanyika kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Spika, mfano elimu ya sekondari ya chini (*O level*) kutambuliwa kuwa ni sehemu ya Elimumsingi kwa watoto wetu na inatolewa bila malipo ya ada. Aidha, katika elimu ya ualimu tumeongeza miaka ya kumwandaa mwalimu wa elimu ya awali kutoka miaka miwili kuwa miaka mitatu. Pamoja na mabadiliko hayo, Serikali imeendelea na uimarishaji wa elimu yetu kuwa ya umahiri (*competence based*) kutoka katika mfumo wa awali ambao ulimwanda mhitimu kwa nadharia bila mafunzo kwa vitendo ya kutosha. Uboreshaji huu umefanyika sambamba na uimarishaji wa mitaala katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mfumo wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi, Serikali imeunda Mabaraza ya Ujuzi ya Kisekta ambayo yanakuwa kiungo kati ya Vyuo vya Elimu ya Ufundu na wadau, vikiwemo viwanda na waajiri. Mabaraza hayo yatahakikisha kuwa mitaala inayotumika inakidhi mahitaji ya wadau na soko la ajira. Katika ngazi ya elimu ya juu, Serikali imeendelea kuhuisha na kuanzisha programu mbalimbali zinazotolewa ili kuandaa wahitimu wenye ujuzi unaohitajika Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali, immeanzisha vituo atamizi katika taasisi za elimu ili kuhakisha wahitimu wanapata fursa za kulea mawazo na ubunifu wao. Maboresho haya yanalenga kuimarisha umahiri wa wahitimu wetu ili waweweze kuajirika na pia kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuhakikisha kuwa Mfumo wa Elimu unakidhi mahitaji ya soko Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa ustawi na maendeleo ya nchi yetu.

Na. 33

**Sifa za Mzabuni katika Kusimamia Mapato ya Serikali
kwenye Migodi Midogomidogo**

MHE. SALOME W. MAKAMBA aliuliza:-

Je, ni sifa zippi ambazo mzabuni anatakiwa kuwa nazo ili kupewa nafasi ya usimamizi mapato ya Serikali kwenye migodi midogo midogo (*rush*) kama Mwabomba, Namba Mbili, Segese na kadhalika?

WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudii kubwa zinazofanywa na Wizara katika kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kufungua masoko ya madini nchini nzima, kumesababisha ongezeko la wachimbaji wadogo ambaao wamekuwa wakivamia maeneo mbalimbali (*rush*) kama vile kwenye maeneo yaliyotengwa, maeneo yenye leseni kubwa za utafiti, maeneo ya uchimbaji mkubwa, maeneo yasiokuwa na leseni na maeneo ambayo leseni zake hazijaendelezwa kwa shughuli za uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia Tume ya Madini ilitoa Waraka wa Ndani Na. 3 ulioanza kutumika tarehe 15 Oktoba, 2019 wenye dhumuni la kutoa mwongozo kwa Maafisa Madini Wakazi na watumishi wengine katika kusimamia, kudhibiti shughuli za madini na mapato ya Serikali katika maeneo yenye *rush*. Kwa mujibu wa Waraka huo, utaratibu unaotumika kuwapata wasimamizi wa *rush* kama alivyoulima Mheshimiwa Mbunge, ni kuititia Kamati ya Uongozi inayofuatisila na kuimarisha usimamizi katika eneo la *rush*.

Mheshimiwa Spika, Kamati hiyo huteua wasimamizi wa *rush* ambapo Mwenyekiti wa *rush* anapaswa kuwa na

sifa zifuatazo: Awe mchimbaji mzoefu hasa katika usimamizi wa maeneo ya aina hiyo; asiwe na historia ya wizi wa fedha za Serikali; na awe mwaminifu. Aidha, wajumbe wengine kwenye usimamizi wa *rush* ni pamoja na Katibu, Mweka Hazina, Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji, Mjumbe wa *REMA, TAWOMA* na mwakilishi wa eneo/shamba.

Na. 34

Kulisaidia Shirika la Bima

MHE. SAED A. KUBENE aliuliza:-

Kuna taarifa kwamba ubadhirifu bado unaendelea katika Shirika la *NIC*; vilevile taarifa zinaonesha kuwa Shirika hilo halina mipango thabiti ya kukabiliana na washindani wake kibiashara:-

(a) Je, ukweli juu ya taarifa hizo ni upi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuisaidia *NIC* kifedha na kitaalam ili kuliwezesha shirika hilo kukabiliana na ushindani wa kibiashara?

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hakuna ubadhirifu wowote unaoendelea katika Shirika la Bima la Taifa (*NIC*) na Shirika limeendelea kuboresha mifumo yake ya udhibiti wa mapato na matumizi ili kukabiliana na washindani wake kibiashara katika sekta ya bima. Katika kujiiimarisha kibiashara, Shirika limechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mapato yote yanakusanywa kwa kutumia Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali (*GePG*) ambao ulianza kutumiwa na Shirika mwezi Novemba 2019 na kuondoa ukusanyaji wa mapato kwa fedha taslimu (*cash*); kuongeza

udhibiti katika ulipaji wa madai ikiwepo kufanya ukaguzi maalum wa madai yote ya Bima za Maisha ili kujiridhisha juu ya uhalali wa madai haya; Shirika lipo katika hatua za mwisho za kuunganishwa na Mfumo wa Usimamizi wa Shughuli za Kihasibu na Malipo katika Taasisi za Umma (*MUSE*) ambao utaongeza udhibiti katika malipo yote yanayofanyika; kusitisha matumizi ya hundi (*cheque*) ambapo kuanzia mwezi Desemba 2019, Shirika lilisitisha matumizi ya hundi (*cheque*) katika malipo yake yote na kuanza kutumia mfumo wa malipo wa kielektroniki hivyo kuongeza uthibiti wa matumizi na kuzuia uwezekano wa matumizi ya hundi feki (*forged cheques*).

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imechukua hatua mbalimbali kuliimarisha Shirika la Bima la Taifa (*NIC*) kitaalam kwa kufanya yafuatayo: Kuliondoa Shirika kutoka kwenye mashirika yaliyotakiwa kubinafsishwa na kuliwezesha kushiriki katika blashtara ya bima kwa ushindani; imelifanyia mabadiliko ya kiuongozi Shirika ili kuongeza tija na kuleta mabadiliko chanya kwenye utendaji na usimamizi wa shughuli zake; na imelisaidia Shirika kwa kuwapatia wataalamu mbalimbali katika nyanja za mifumo ya TEHAMA, mifumo ya utendaji kazi na mifumo ya utunzaji kumbukumbu (*e-Office*) ili kuweza kuongeza ufanisi wa Shirika na kuweza kukabiliana na ushindani wa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeliimarisha Shirika kifedha kwa kuchukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kupata biashara za Serikali na kushinikiza malipo ya hapo kwa hapo ya *premium* ambayo yamesaidia kupunguza malimbikizo ya *premium* kutoka kwa Taasisi za Serikali kutoka zaidi ya shilingi bilioni 20 hadi milioni 500 kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maendeleo mazuri ya Shirika, Serikali inaendelea kuliimarisha Shirika hili la kimkakati kwa kulisaidia katika kupitia upya Mpango Mkakati wake ili uendane na mahitaji halisi ya biashara ya ushindani; kuongeza uwekezaji katika mifumo ya TEHAMA ili kuwafikia wateja wengi zaidi; kuongeza ubora wa huduma zake na kulipa madai haraka na kwa urahisi; kujitangaza zaidi na

kuongeza uwekezaji wenye tija ili kutoa gawio kubwa kwa Serikali na kushiriki katika shughuli za maendeleo ya Taifa.

SPIKA: Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Ofisi ya Waziri Mkuu

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Majadiliano yanaendelea. Natumaini wote ambao wamepangwa kwa siku ya leo kuweza kuchangia, orodha ya CCM siloni na muda wetu ni mdogo, tunapaswa kuanza *on time*. Basi tuanze na Mheshimiwa Suzan Kiwanga halafu tutaendelea. Mheshimiwa Susan, upande wa Chadema. Orodha ya *CUF* pia sina.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, ukizingatia hili ni Bunge la mwisho la kipindi changu cha kukaa Bungeni nikiwakilisha wananchi wa Jimbo la Mlimba. Nawashukuru Watanzania wote na wananchi wa Jimbo la Mlimba kwa kunipa ushirikiano katika kipindi changu chote cha miaka hii mitano kasoro.

Mheshimiwa Spika, namshukuru vile vile Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa kuniamini mara ya pili; katika kipindi kilichopita nilikuwa Naibu Waziri Kivuli wa Wizara ya Maji, sasa hivi nimekuwa tena Naibu Waziri Kivuli wa Wizara ya Ujenzi. Nakushukuru pia kwa kuwaamini wanawake wengi ndani ya chama chetu na Kambi yetu. Kweli wanawake tunaweza bila kuvezeshwa bali tukipewa fursa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia bajeti yangu hii ya mwisho kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kwenye kipindi hiki cha Bunge. Ningeweza kuchangia mambo mengi sana kama

kawaida yangu, lakini inapotokea dharura ama shida katika nchi, ni vyema nikajielekeza katika shida iliyopo ndani ya nchi yetu hususan kwenye huu ugonjwa huu wa Corona ambao ni muhimu sana tukauchangia kama Wabunge kuangalia hali za maisha yetu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pole kwa wananchi wote ambao wamepatwa na maradhi haya ndani ya nchi yetu na wengine ambao hatujapimwa, hatujui afya zetu, lakini vilevile nitoe pole kwa ndugu wa marehemu ambaye alikufa ndani ya nchi yetu na akazikwa na Serikali. Huu ugonjwa ni hatari.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Waziri Mkuu ni bajeti ambayo inaenda kuangalia Wizara zote. Vilevile tumejionea wenyewe ndani ya nchi hii mabadiliko ya hali ya hewa ya nchi yetu hasa ndani ya mkoa wa Morogoro hususan ndani ya Bonde la Kilombero, Ulanga na Malinyi.

Mheshimiwa Spika, hili bonde lilikuwa linatoa mazao mengi sana, lakini mwaka huu kulingana na mvua zilizoanza mapema, hakuna mkulima aliyepanda mpunga. Walikuwa wanasubiri angalau mvua hizi za mwanzo zilizoanza ziishe ndiyo wapande, lakini mpaka sasa ninavyozungumza, bonde lote limejaa maji, hakuna mkulima ameweza kupanda. Kwa hiyo, hali ya hatari ndani ya bonde letu inaweza ikawa hatari zaidi jatuja suala la njaa.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, napenda kushauri, kwa bajeti hii ya Waziri Mkuu, Serikali iliangalie hili na kitengo chake cha maafa, kitengewe fedha za kutosha kuokoa hali ya Watanzania hususan wananchi wa Mlimba na Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, hali ya ugonjwa bado iko tete, hata hivi karibuni nimetoka kuongea na Mkurugenzi wangu kujua amefanya nini katika kujikinga na hiyo hali kuanzia maofisini mpaka kwa wananchi, kwa sababu yeye ndiye anayekusanya mapato ya wilaya zetu. Alichonijibu, anasema ni kweli ameweka maji na sabuni na nikamsisitiza kwamba ni

muhimu sana kununua na *sanitizer* hasa katika maofisi kwa sababu mtu anaweza asinawe maji lakini akiwa na *sanitizer* itamsaidia zaidi katika kushika vitabu na mambo mbalimbali hapo ofisini na amenikubalia anasema atafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, hali ni tete. Sasa kama sisi hatujapimwa: Je, hali kwa Watanzania ikoje? Nakumbuka Mheshimiwa Kaimu Kiongozi wa Kambi, Mheshimiwa Halima Mdee, aliomba angalau tuanze na sisi Wabunge tuangalie afya zetu sisi ambao tunawakilisha wananchi, tuone hali halisi halafu twende kwa wananchi vile vile.

Mheshimiwa Spika, hili suala linatakiwa liwe nchi nzima kuwe na mafungu ya kutosha, kuwe na vitendanishi vyta kutosha ili tupime afya za wananchi wetu tunapochanganyikana tuonekane kwamba tumeshapima. Hii kupima tu kwa kipima joto, kwa kweli mtu anaweza akanya *Panadol* na akija hapo akakutwa joto limeshuka kwa dakika chache, lakini hali inakuwa siyo nzuri. Kwa sababu dalili zake ni nydingi, siyo kukohoaa tu; mtu unaweza ukaanza kupandwa joto lakini *Corona* ndiyo unayo na bado hujaanza kukohoaa. Sasa tunavyojiaminisha kwa kujipima tu joto, naona siyo sawa kabisa.

Mheshimiwa Spika, hiyo hali ni muhimu tukaiona na kwamba kuwe na bajeti ya kutosha katika Kitengo cha maafa ili tuone namna gani tunaenda na milipuko inavyotokea ndani ya nchi yetu. Siyo hiyo tu, katika Wizara ya Afya kama ilivyosema, kwamba ni asilimia 15 tu ya bajeti iliyotekelizwa. Je, sasa Serikali inakuja na mpango gani mahususi kuhakikisha kwamba hela ya kutosha inatengwa katika hii Wizara ili inapotokea mambo ya mlipuko tusitegemee tu misaada na sisi wenyewe tuwe na uwezo wa kujikinga? Leo unasikia kwamba hapa ni Mloganzila ndiyo wameweka, labda Waziri Mkuu alitembelea Kibaha.

Mheshimiwa Spika, je, unaonaje sasa huku vijijini kwetu? Kwa mfano, Jimbo la Mlimba kuna treni, kuna wakulima, wafanyabiashara wanatoka Dar es Salaam,

wanatoka Tanzania nzima wanaenda kule, lakini wananchi wa kule hawajui hali halisi ya ugonjwa huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kupimwa na wananchi katika vijiji vyetu na katika maeneo yetu na kuweka hizo tahadhari na hospitali kila wilaya au kule tusiokuwa na Hospitali za Wilaya, kwenye zile Hospitali za Kata ambazo ni Vituo vyta Afya, kuna haja kabisa ya kuweka *emergency* ili tunapopata mgonjwa kwa dharura tuwe tunajua tunampeleka wapi? Siyo kama ilivyo sasa hivi, watu tumekaa tu, hatuelewi kitu gani kinaendelea, utafikiri hatuko duniani, tumejifungia hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika hotuba hii ya Waziri Mkuu kuhusu masuala ya *NIDA*. Pamoja na kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani amesema *NIDA* sasa hivi wana mashine, wana hela, lakini hali halisi ikoje ndani ya Wilaya ya Kilombero hususan Jimbo la Mlimba? Wananchi wa Jimbo la Mlimba hawana uwezo wa kupata vitambulisho hivyo vyta *NIDA* kwa sababu hawana cheti cha kuzaliwa wala hawajamaliza la Darasa la Saba.

Mheshimiwa Spika, wako wengi, watu wamezaliwa huko mashambani au machungani, hawajasoma, lakini ni Watanzania wanaotakiwa wapate hizo laini za simu na vyeti. Sasa hivyo hali, naomba kama alivyosema, siyo mipakani tu, watambuliwe na vijiji, hata kwenye vijiji kwetu Wenyeviti wa Vijiji na Mikutano ya Vijiji iwatambue hawa wananchi kama kweli ni Watanzania, wapewe barua ili wapate kujisajili kwenye *NIDA*. La sivyo, watakaa hivyo, wataonekana siyo Watanzania ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni muhimu sana na bajeti vilevile ilikuwa ndogo hawajafika kabisa watu wa *NIDA* ndani ya Kata za Mlimba. Kati ya Kata 16, wamefika Kata mbili tu, Kata 14 hawajafika. Naomba hilo lichukuliwe kwa uzito, waende wakasajili watu ili wapate hivyo vyeti.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa uchaguzi tumeshuhudia, mimi mwenyewe nilikuwa kwenye uchaguzi mdogo Sofi, halini mbaya, tunahitaji Tume Huru ya Uchaguzi.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Kengele ya pili.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ni dakika 10!

SPIKA: Eeh, ukiangalia hata saa yako.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mbona mimi saa yangu iko tofauti!

SPIKA: Haya malizia sentensi ya mwisho.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, yaani dakika saba tu ndiyo mimi nimeongea.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Uchaguzi ndiyo amani ya nchi hii. Bila kuwa na Tume ya Uchaguzi, tunaingiza nchi katika hatari kubwa. Leo tunacheke tuko hapa, lakini hakuna mtu atakayevumilia kuona anaporwa, kuona anafanyiwa vitu vya ajabu, wakati ametimiza masharti halafu tume inakuwa ya mtu mmoja, anateua mtu mmoja.

Mheshimiwa Spika, Katiba iko wazi, tunahitaji Tume Huru ya Uchaguzi ili kuzidisha amani ndani ya nchi yetu. Bila haki, amani haitakuwepo. Haki ni tunda la amani ndani ya nchi yetu. Tusifanye mzaha tukatekeleza kizazi, amani haitakuwepo na miundombinu tunayoifanya ni sawasawa na bure. Naomba sasa Tume Huru ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, mlete sheria, turekebishe vipengele na Bunge ndiyo hili ili twende kwenye uchaguzi salama. Chadema hatuhitaji uchaguzi usogezwe mbele hata sekunde moja. Tunataka hata leo ukitangazwa uchaguzi

tingie kwenye uchaguzi na Tume Huru kwa sababu uwezo tunao, tumejipima tunaweza na kwenye chaguzi ndogo mlishuhudia. Tulishinda, mkatupora. Watanzania hali haijabadilika, hali ni mbaya. Tunaomba Tume Huru ya Uchaguzi, Katiba iseme wazi.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Ninyi Makatibu wa Mezani, acheni mambo yenu hayo!

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Suzan. Nakushukuru sana kwa mchango wako. Unajua kuna Wabunge wanatakiwa kuwa humu ndani, wengine siwaoni, sijui watu wamehama nafasi au inakuwaje! Mchungaji Lwakatare yuko humu ndani! Maana namtafuta simwoni Mchungaji Lwakatare. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, atafatiwa na Mheshimiwa Abdallah Mtolea. Suzan homa hapo! (*Kicheko*)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mimi nitakuwa na masuala mawili. La kwanza ni la Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, imetaja kazi nzuri sana alizofanya Mheshimiwa Rais katika nchi yetu na kila mtu anajua kwa sababu kuna uchaguzi, mimi nilikuwa natoa tu mapendekezo; ili kasi hii iendelee, nawaomba Watanzania wote tumpitishe Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika uchaguzi ujao ndani ya chama na kwenye Uchaguzi Mkuu ili aweze kugombea peke yake, kwa sababu kazi alioifanya ni kubwa, kubwa, kubwa sana na ya kupigwa mfano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu alikuwa anamsaidia vizuri sana Mheshimiwa Rais, nawaomba wapiga kura wa Jimbo la Ruangwa, pamoja na

demokrasia, apite bila kупingwa. Vile vile wa tatu; na hili simung'unyi maneno; katika miaka mitano ndani ya Bunge hili, Mheshimiwa Spika, wetu, Bunge hili umeliongoza vizuri sana, sana, sana na mabadiliko tumeyaona. Nawaomba wapigakura wa Kongwa na wanisikie hao Wagogo watani zangu wakupitishe bila kупingwa ili kusudi kasi hii iliyopo iweze kuendelea. Baada ya huo utangulizi, nilisema nitazungumzia mambo mawili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, wachangiaji wote waliosimama wamezungumzia kuhusu homa kali ya mapafu (*Corona Virus*); nami nitajikita hapo hapo mwanzo mpaka mwisho, kwa sababu ugonjwa huu unatesa dunia.

Mheshimiwa Spika, naomba tuungane na Mheshimiwa Rais kuliombea Taifa letu ili shetani huyu *Corona Virus* aweze kuishia huko allko. Naomba tusiletie siasa katika ugonjwa huu. Ugonjwa huu ni mbaya, ni mbaya sana. Kirusi hiki ni tofauti na virusi vingine. Ni kirusi ambacho hakionekani, hakishikiki na wala hakijulikani, kiko kimya, kinaambukizwa kwa mfumo wa hewa. Naomba sana, hili tumwombe Mwenyezi Mungu atusamehe, atuepushe na ugonjwa huu hatari wa *Corona Virus*.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikisikiliza mara nyingi katika mitandao na ili tusaidiwe, tuombe wataalamu wetu; najaribu kumtazama hapa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ambaye ni mtaalamu wa milipuko, simwoni, wangetusaidia pamoja na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile. Tunaambiwa kwamba ugonjwa huu unaambukizwa kwa hewa; mtu anapopiga chafya, anapokoho. Sasa hizi *masks* ambazo tunatakiwa tuvae usoni kuziba midomo na pua, lakini hizi *masks* bei yake ni kubwa sana. Mtanzania wa kawaida wa kule Sumve, Ruangwa na Kongwa hawezi kumudu kuzinunua.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu na ninafikiri unakubalika; nimemsikiliza mtaalamu jana anasema kwamba tunaweza tukatumia vitambaa kama *mask*. Bahati nzuri kama utaruhusu na kwa sababu shule nyingi zimefungwa sasa na baadaye zitafunguliwa, nina mfano wa *mask* kwa ajili ya

watoto wa shule ambazo ni kitambaa. Bei yake ni chini ya shilingi 500/= kwa *mask* moja ya kitambaa ambayo inazuia.

Mheshimiwa Spika, pili...

SPIKA: Taarifa Mheshimiwa Ndassa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Naam.

SPIKA: Eeh, pokea kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa msemaji ambaye anaongea kwa lengo la kumsaidia tu katika mchango wake kwamba kwanza ugonjwa wa *COVID 19* hausambazwi kwa njia ya hewa. Ni ugonjwa ambao unasambazwa na kutokana na maji maji ambayo yanatokana na chafya kwenye pua au mdogo wake yanapomfikia mtu mwingine na au akishika maeneo ambayo mtu amepigia chafya au maji maji yale ya kutoka kwenye mdogo yatapokuwa yamedondokea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika maambukizi haya, yeote kati yetu akipata maambukizi ni kwamba, moja alikuwa karibu na mtu ambaye alikuwa na ugonjwa huu akampigia chafya au akamkoholea au ameupata kwa kushika sehemu ambazo mtu alipiga chafya au akakoho naye akashika uso wake, akashika macho, pua au mdomo. Ndiyo maana wakati tunaingia hapa nimewaambia Waheshimiwa Wabunge, ukipata ugonjwa huu, hiyo ni kati ya mikono yako. Usafi wa mikono yako ndiyo inaweza ikakukinga.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo nataka nilitolee ufanuzi, *masks* za vitambaa havizuii virusi wala bacteria. Havimkingi mtu kupata virusi vya *Corona*. Kwa hiyo, tuwe waangalifu sana na aina ya *mask* tunazotumia. Kuna *mask* ambazo ni *surgical mask* na N95 ambazo zimethibitishwa

pasipo shaka kwamba zinaweza zikazuia virusi au kumkinga mtu.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya kwa taarifa hiyo muhimu. Tunakushukuru. Hii taarifa ni kwa wote, wala siyo kwa Mheshimiwa Ndassa peke yake. Mheshimiwa Ndassa endelea.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Namshukuru Mheshimiwa Dkt. Ndugulile kwa maelezo ya ziada hayo, lakini nilikuwa najaribu tu kuona namna nzuri zaidi ya kuzuia kwa sababu unapozungumzia hizi *masks za box*, twende kwenye uhalisia, Mheshimiwa Waziri wa Afya na Naibu Waziri wa Afya, kwenye uhalisia hizi *masks za box* kwanza uwezo wake kwa mujibu wa wataalamu wanasema zinatakiwa zivaliwe ndani ya masaa manne. Zaidi ya hapo, yenyewe inabeba ule uchafu tena na hiyo *mask ya box* huwezi kuifua ni lazima uitupe.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa huyu mwananchi wa kawaida, mwananchi wa kawaida uwezo wa kununua mask kila siku ni mdogo, tofauti na hizi *mask 95* Mheshimiwa Dkt. Ndungulile anaifahamu, najaribu kuzungumzia uhalisia kwamba ili tuwasaidie wananchi wetu hasa waliopo chini ni lazima tuangalie namna nyingine mbadala na namna nyingine mbadala wenzetu wa Wizara ya Afya mnawenza kutasaldia ili tutafute na namna nzuri zaidi ya kuzuia haya maambukizi ya *corona virus*.

Mheshimiwa Spika, lingine nishauri tu kama nilivyoshauri mwanzo na mimi kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Ndungulile amesema hazizuii. Lakini bado Mheshimiwa Dkt. Ndungulile, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya nitakupa hizi *sample uende nazo* kwa wataalam wako ili wakadhithibitishé kwa sababu nia hapa ni kuzuia, ni kuzuia huko vijijini maambukizi haya leo tunaona kama ni kitu cha kawaida lakini ugonjwa huu ni hatari sana kwa Taifa letu. Haya mafanikio ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyaeleza ya *SGR*, Reli ya kati hiyo hatuwezi kuyapata kama watanzania

ni wagonjwa niombe sana, niombe sana lazima Serikali yetu ilitazame kwa makini sana suala hili la ugonjwa wa *corona*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Senator Richard Mnganga Ndassa ahsante sana. Nilikwisha mtaja Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea na atafutiea na Mussa Ally Ntimizi. Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru wa kunipa nafasi lakini nianze kwa kumshukuru Mwenyenzi Mungu Allah Subhanahu Wataala kwa kutujalia afya njema na kuweza tena kupata fursa ya kuchangia katika bajeti ya mwisho kabisa katika kupindi hiki cha kwanza cha kukitumikia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja na nina tambua kazi nzuri zinazofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu akishirikiana vizuri na Mawaziri wake Mheshimiwa Jenista, Mheshimiwa Angela, Wasaidizi wake Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Ikupa mmefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na haya mimi leo nina jambo moja tu, na jambo hili ninalielekeza kwa msajiri wa vyama vyaa siasa. Mheshimiwa Spika mwaka jana tuliboresha sheria ya vyama vyaa siasa na kuumpa nguvu sana msajiri wa vyama vyaa siasa ili awe meno katika kuvisimamia vyama vyaa siasa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nijue ni lini msajiri wa vyama vyaa siasa atakuwa amejiridhisha kwamba matukio ya fujo siasa za chuki kuamsha mihemuko ya hasira kwa wananchi zinazofanywa na Chama cha Demokrasia na Mandeleo CHADEMA kuwa ni sababu za tosha ya kukifuta chama hiki.

WABUNGE FULANI: Aaah tulia wewe!

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, chama hiki kimesababisha fujo nyingi na moja kati ya fujo iliyofanyika tarehe 16 Februari, 2018 iliyopelekea kifo mdogo cha Akwilina Akwiline Bafutah. Hapa nina hukumu ya Kesi ya Jinai Namba 112 kesi ya mwaka 2018 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisitu.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, kwa faida ya Bunge lako naomba kunukuu Shauri Na. 4 katika kesi hiyo, kesi hiyo ilikuwa na mashauri 13. Na. 4 inasema hivi:-

"Particularly of the force account are that on 16th February, 2019 along Kawawa Road at Kinondoni Mkwajuni area within Kinondoni district in Dar es Salaam Region jointly and together with more than twelve other persons not in quote having riotously assembled in disobedior of proclamation to dispense made SP Gerald Thomas Nginja failed to dispence..."

SPIKA: Labda jambo moja Mheshimiwa shauri hilo limekatiwa rufaa au halijakatiwa rufaa?

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, halijakatiwa rufaa.

SPIKA: Nawauliza upande huu.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, *notes* ya rufaa imeshatolewa na rufaa imeshakatwa kwa hiyo namshangaa anavyohaika tena...

SPIKA: Basi liruke tu...

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, endelea tu halafu utafisiri kwa Kiswahili baada ya hicho kingereza.

SPIKA: Kwa ajili ya taarifa hii ambayo tumeipata. Endelea ana hoja yako.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, naendelea na hoja yangu kwa maana niache kunukuu kwa sababu wametoa *notes* ya rufaa na rufaa hajashikiliwa na kwa sasa hukumu halali ya *public* ni *public document* inaweza kutumika mpaka mahakama nyine itakavyosema vinginevyo ndio maana nimeichukua hapa kuinukuu.

WABUNGE FULANI: Endelea endelea!

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, katika shauri hili Na. 4 fujo zao za kukataa amri halali ya polisi zikasabisha kifocha huyu binti Akwilina Akwilini Bafutaa. Lakini kibaya zaidi chama hiki hakionyeshi kujutia tukio hili, hukumu hii ilivyotoka chama hiki tulitegemea kama viongozi wa wananchi wanetoka kwenda kuiomba samahani na kuipa pole familia ya huyu binti marehemu. Lakini wao wakaanza kufanya vikao na waandishi wa habari vyta kisiasa vyta kujijenga kisiasa wakafanya vikao asubuhi mchana na jioni wakawa wanawaita waandishi wa habari wakilia kwa furaha ya shauri hili kuisha. wakati hawa wanalia kwa furaha mama wa marehemu Akwilina analia kwa uchungu. Wakati hawa wanafuata machozi ya furaha mama yake marehemu Akwilina hana mtu wa kumfuta chozi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama sio sisi wakumesemea mama Akwilina ambaye amempoteza mtoto kwa fujo za CHADEMA ni nani mwagine anaweza kumsemea? Kwa hiyo, majigambo waliyokuwa wakifanya mbwembwe za kuchangishana fedha walizokuwa wazikifanya hazikuwa zinafanya dhidi ya CCM, hazikuwa zinafanya dhidi ya Serikali zilikuwa zinafanya dhidi ya mama yake Akwilina aliye poteza mtoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mambo haya kama msajiri wa vyama vyta siasa anaendelea tu kuyaangalia tunakwenda wapi? Na mimi nikukumbushe hizi hatua za kuachana na ubinadamu wanapiga kila siku, walianza kila ikitokea msiba labda wa CHADEMA aaah! Labda au wa Mbunge wa chadema au mwana CHADEMA mwenzao wakawa

wanageuza misiba hiyo sio kuwa sehemu ya mbaombolezo bali kuwa jukwaa la kisiasa.

Mheshimiwa Spika, nikukumbushe wakati wa msiba wa marehemu Kasuku Bilago, wewe na ofisi yako mlikuwa mkishirikiana vizuri na familia ya marehemu Bilago. Ukafunga safari hapa mpaka Kankongo kwenda kuzika kwa tarehe ambayo umepanga. Kufika kule CHADEMA wakaairisha ule msiba usizikwe siku ile ili wewe usizike wao waweze kufanya siasa siku inayofuata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiendelea kuyavumilia haya tunatengeneza siasaya aina gani? Ifike mahala msajiri awe mkali asilichoshe jeshi la polisi kufanya vitu ambavyo na yeye pia ana nafasi ya kuweza kuvifanya. Maadili ya vyama vyaa siasa yanasmamiwa na msajili iwa vyama vyaa siasa yanasmiliwa na msajili wa vyama vyaa siasa. Hapa katika haya mauaji ya marehemu Akwilina wenyewe walipanga wafe watu 200, ukisoma shauri Na. 10 ambalo ameshtakiwa Mheshimiwa Mboge peke yake katika kesi hiyo hiyo, muendesha mashtaka ana mnukuu wakati anawaanda sasa ili watoke wakati wanaingia mtaani kwamba wafe angalau watu 200.

Mheshimiwa Spika, ule ulikuwa ni uchangazi mdogo wa jimbo moja Kinondoni akafa mtu mmoja katika *target* ya watu 200. Tunaelekea uchagazi mkuu kila kata kutakuwa na uchagazi kila jimbo litkauwa na uchangazi nchi nzima itakuwa na uchangazi hivi unajua wamepanga kuua watu wangapi? Lakini wewe mwenyewe ni shaihidi baadhi ya Wabunge hapa mara kadhaa wanasmama wanasema mimi nisingetangwa kama watu wawili wasingekufa mimi singetangazwa kama watu watatu wasingekatwa miguu. Haya yote ni mwendelezo wanayoyapanga wenzetu, sisi tunapanga kwenda kushinda majimbo wao wanapanga kwenda kuua watu msajili wa vyama vyaa siasa yupo wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya mambo ni lazima kama Bunge tuamue, tuamue kwamba tunalaani siasa hizi

zinazofanywa na CHADEMA. Hata kama msajili atachelewa, lakini sisi kama Bunge *part* yetu tuifanye. Nilikuwa hata ninapata hisia kwamba mwishoni wa mchango huu nitoe hoja angalau tukatoe pole kwa familia ya Akwilina kwa kilichotokea tukamfute chozi huyu mama haiwezekani anaonewa mtu mmoja anashambuliwa na taasisi fulani tena ya viongozi wengine ni Wabunge halafu tukaa kimya tu ni lazima huyu mtu afutwe chozi. Na wakumfuta chozi sio hawa waliosababisha mauaji ya mwanae ni sisi tunayeyaona haya kwa mbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiyaacha haya mambo na msajili akaendelea hivi hivitutaipeleka hii nchi kubaya. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Mtolea nillishakutaja Mheshimiwa Mussa Rashid Ntimizi.

MHE. MUSA R. NTIMIZI: Mheshimiwa Spika, naashukuru mimi Musa Rashid Ntimizi huyu Ahangazi wa Tanga huko. Nashukuru kwa kupata nafasi niweze kutao mchango wangu kidogo, katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa pongezi za dhati kwa hotuba nzuri na kazi nzuri ambazo zinafanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Nimpongee dada Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kuwa kiungo kizuri sana kati serikali na Bunge letu tukufu kwa kazi zuri ambazo zinafanyika pale. Waziri wa Uwekezaji, dada yangu Mheshimiwa Ikupa na mdogo wangu Mheshimiwa Mavunde kwa kazi nzuri ambazo anafanya kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kutekeleza majukumu yake mazuri kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nichukue nafasi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Igalula kupongeza kazi nzuri ya Serikali hii ya Awamu ya Tano waliyoifanya katika kipindi chote na sasa wanaelekea kumaliza na sasa tunaelekea kumaliaz miaka mitano. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri aliyoifanya Mheshimiwa Rais

amesimamia kauli zake, Mheshimiwa Rais amesimamia ahadi zake ambazo alituahidi wana Igala ambacho kipindi chote ambacho amekuwa katika uongozi wake.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii fupi nikupongeze wewe na Bunge lako tukufu kwa kazi kubwa ambazo umezifanya mafanikio mazuri ya serikali yetu ya Awamu ya Tano yanatokana na kuungwa mkono na Bunge lako na kutekeleza na yanastahili kulifanya. Nakuongeza sana na pia nawapongeza Wabunge wote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia miradi iliyotekelawa kimkakati katika nchi yetu katika kipindi cha miaka mitano, ikiwemo bwawa na ufuaji la umeme la Mwalimu Nyerere Mradi mkubwa wa *Standard Gauge*, mradi wa REA, ununuzi wa ndege sisi kwa tabora maji ya kutoka Ziwa Victoria, ujenzi wa wilaya na vituo vyaa afya, elimu bure na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba hii miradi yote ambayo imezungumzwa hapa imeleta *impart* katika uchumi wetu na kuongeza ajira kubwa sana rasmi na zisizo rasmi kwa nchi yetu, watu wengi wanasesma Serikali haitakangazi ajira lakini miradi hii katika utekelezaji wake kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu imeleta ajira nyingi sana zilizo rasmi na zisizo rasmi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba nigosie miradi ambayo ni ya kimkakati aliyozungumzia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kutoa ushauri ili iweze kuboresha huko tunakokwenda mbele. Nikianzia katika eneo la kilimo kwa haraka haraka pamoja na kwamba tunaporesha miundombinu yote hii yote ambayo tumeitaja ya reli, kutengeneza mradi wa umeme, REA na kadhalika inaenda ku-*effect* kwenye kilimo chetu. Lakini yapo mambo ambayo tunatakiwa tuyafanya ili kusaidia kilimo ambacho kinachangia wa asilimia 29 ya *GDP* ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia suala la miundombinu la umwagiliaji ni eneo ambalo hatujaliwekea msisitizo sana.

Niombe Wizara ya Kilimo iliangalie hili eneo ili tutakapoboresha miradi hii ya umwagiliaji itaenda kusaidia uchumi kama onavyoona eneo hili la kilimo linasaidia katika asimilia 29 katika *GDP*. Tukirekebisha miundombinu ya uwagiliaji na hakika tutaongeza upatikanaji wa chakula na mwisho wa siku wananchi wetu wakulima tutawasaidia.

Mheshimiwa Spika, lakini hapo hapo tuangalie masoko ya mazao yetu ya kimkakati ikiwepo Tumbaku, Kahawa, Korosho, na Pamba. Tuangalie bei ya mazao haya, tuangalie soko la mazao haya tuangalie upatikanaji wa pembejeo ya mazao haya hapa nazungumizia tupate mbolea kwa wakati mbolea ya kupandia ije wakati wa kupanda, mbolea ya kukuzia ije wakati wa kukuzia. Lakini pia tuongeze ruzuku kwenye mbolea ili kushusha bei ya mbolea iweze kumsaidia mkulima. Lakini vile vile usimamizi wa vyama vya msingi ushirika ili mwisho wa siku mkulima aweze kupata tija.

Mheshimiwa Spika, naomba nzungumzie suala la miundombinu ya barabara, unapozungumzia ukuaji wa kilimo unazungumizia masoko yake unazungumzia na bei yake. Kama barabara zetu za kijiji hazipitiki mwisho wa siku bei ya mazao haya bei inakuwa ndogo au itakuwa kubwa mwisho wa siku mkulima hatopata faidi. Gharama za usafirishaji zitaongeza na mwisho wa siku hata mazao yanaweza fika sokoni yakiwa yameharibika. Niombe tuiongezee *TARURA* uwezo wa kifedha ili mwisho wa siku tuweze kutengeneza barabara hizi zisaidie mkulima huko kijijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba naomba kidogo nzungumzie kidogo *REA*, *REA* inafanya vizuri nipongeze kwa kazi nzuri inayofanyika. Maeneo yetu ni makubwa changamoto zake ni nyingi lakini wanajitahidi wanafika maeneo mengi kwa hili kabisa naomba nitoe shukrani za dhati kwa miradi ya rea inayofanyika. Lakini ninachotaka ni shauri hapa zipo changamoto ndogo ndogo. Vipo baadhi ya vijiji ambavyo vinarukwa, vipo baadhi ya vitongoji ambavyo vinarukwa basi haya mapungufu yaweze

kufanyiwa kazi, na serikali iweze kutoa fedha kwa REA kutekeleza miradi yake.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la afya nipongeze kazi kubwa ya ujenzi wa hospitali za wilaya nipongeze kazi kubwa ya ujenzi wa vituo vya afya, nipongeze kazi kubwa inayofanya ya kuleta madawa n.k. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hili eneo nataka nishauri kitu kimoja tusisahau ujenzi wa zahanati, wananchi wamechangia kujenga zahanati lakini mwisho wa siku hatujawasidia vya kutosha. Rufaa yakutoka zahanati inaenda kituo cha afya, kituo cha afya inayo hospitali ya wilaya *then* hospitali ya mkoa. Tusiporekebisha huku kwenye zahanati tunakapatikana zahanati za kutosha na huduma zikawa nzuri tutakuwa tuna mapungufu kidogo katika utoaji wa huduma za afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengine nitazungumza kwenye sekta husika lakini nataka nimalizie moja, la watendaji wetu wa vijiji na kata. Hawa ndio wasimamizi wakubwa wa maeneo yetu ya maendeleo katika maeneo ya vijiji. Nilikuwa nashauri la kwanza tuwatafutie usafiri wa ukakika wa kufanya shughuli zao ikiwe hata pipipiki. Lakini na pili watendaji wa vijiji wanajenga nyumba za waganga lakini wao hawana nyumba za kuishi. Watendaji wa kata wanajenga nyumba za waganga lakini wao hawana nyumba za kuishi. Tujenge nyumba za watendaji hawa tuwapatie usafiri mwisho siku wasimamie vizuri miradi katika maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka nichangie hayo naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi tunakushukuru sana kwa mchango wako. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Lijualikali naona Wabunge wa Kilombero wanaongea anatafuatiwa na mheshimiwa Mganga Ngereja. Mheshimiwa Lijualikali tafadhalii.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Spika, tangu mwanzo wa Bunge hili linaanza 2015 nimekuwa nikizungumzia sana ujenzi wa barabara yetu ya Ifakara - Kidatu ambayo inatakiwa itoboe iende mpaka Songea. Hii barabara inafadhiliwa na wafadhili katika mradi wa Sagoti wafadhili kama wanne hivi USA Aid na wengine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Magufuli Rais wetu mwaka 2017 aliweka na akasema anaamini hizi km 75 ndani ya miaka mitatu itakuwa zimeisha yaani illitakiwa mwezi huu 4 barabara iwe imeisha. Lakini mpaka dakika hii barabara imefanyiwa kazi kwa *almost asilimia* tano au sita. Leo ni miaka mitatu wafadhili wanalipia kila kitu asilimia 98 ni ufadhili serikali ya Tanzania inatakiwa itoe asilimia mbili tu kwa ajili ya fidia kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mpaka leo barabara inasuasua na juzi nikamwona *RAS* baada ya daraja kuwa limekatika pale kutokana na hizi mvua, anakwenda anamshutumu mkandarasi, anasema mkandarasi ni mzembe, anazembea, Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga barabara hii iishe lakini wewe mkandarasi unazembea kitu ambacho siyo kweli, anajua ukweli. Ukweli ni kwamba Serikali yetu inataki mkandarasi yule atoe kodi (*VAT*) wakati mikataba haitaki kodi kutoka. Kumekuwa na ubishani wa kodi itoke au isitoke, tangu mwaka 2017 mpaka leo miaka mitatu, kitu ambacho tunapewa bure. Yaani wazungu wanatuambia wanataka watujengee barabara na fedha wanatupa, wazungu, mabeberu, ninyi hamtaki barabara ijengwe mnataka kodi. Hii ni aibu kabisa, ni aibu na ni kitu kibaya na sielewe *commitment* ya Serikali katika hili maana yake ni nini. Yaani tafsiri ni nini! Hapa napata mashaka hivi ni kweli wizara zinaweza zikagombana na mkandarasi kama Mheshimiwa Rais Magufuli hajui, kweli!

Mheshimiwa Spika, wnataka watu wa Kilombero tuamini kwamba nyuma ya kwenye huu mpango, kwenye huu ukwamishwaji Mheshimiwa Rais yupo? Kwa sababu kama Mheshimiwa Rais amekuja kuzindua barabara na akasema ndani ya miaka mitatu barabara iishe, leo ni asilimia tano na

Mheshimiwa Rais ana vyombo vyake, ana watu wake wote. Ana Mawaziri, ana Waziri Mkuu, ana Wakuu wa Majeshi, ana TAKUKURU, ana vyombo vyote, kweli hajui. Hivi kweli nyle hamjui!

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hili ni jambo la aibu na hiyo *commitment* ya Awamu ya Tano wanayosema wao wapo hapa kutetea maslahi ya watu yako wapi kwenye hili jambo. Barabara yetu hiyo sisi huo ni uchumi, sisi kwetu ni uchumi ule.

TAARIFA

SPIKA: Mheshimiwa Lijualikali kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Kamwele tafadhalii.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Lijualikali ambaye ana dakika za kuendelea kuchangia katika bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, barabara ya Kidatu-Ifakara ujenzi unaendelea, Iakini tulikabiliwa na changamoto za hali ya hewa. Mkoa wa Morogoro tangu tarehe Mosi Oktoba, mwaka jana, mvua ilianza kunyesha hajjasimama mpaka leo na kwa asili ya ukandarasi anatumia udongo. Mvua zikishanyesha kuna *moisture content* inayotakiwa ili aweze kujenga barabara, sasa kutoptaka na hayo mazingira ameshindwa kuendelea.

Mheshimiwa Spika, tutakuwa na vitu vingi tunavyoviongea Iakini sisi wasimamiaji, mimi ndiye ninayesimamia ule mradi, sehemu kubwa ambayo imefanya hii barabara isikamilike ni kwa sababu ya hali ya hewa na yale maeneo yana mvua nyingi kila wakati na yeye anaishi kule. VAT siyo sababu, VAT ni suala la kiutawala wala halina mgogoro wowote, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Ifakara kule niwaaminishe kwamba Serikali ina nia nzuri ya kujenga barabara ile yote mpaka Malinyi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ndio maana imeshaanza lakini kutokana na hali ya hewa haiwezi ikajengwa katika kipindi cha hali ya hewa mbaya, hivyo ubora wa barabara unaotarajiwa hautapatikana na tutakuja tena kuleta lawama nyingine. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge suala hili tusubiri mvua ikishakatika ataona *speed* tutakayokwenda nayo, hatuna mgogoro mwiningi, e mambo mengine ni ya kiutawala tu. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Lijualikali, taarifa hiyo.

MHE. PETER A. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Spika, utakumbuka Bunge la mwezi wa Tisa mwaka jana nilikuwa humu peke yangu, nilikaa kiti hicho baada ya wengine kuwa wametoka nje kutokana na ambacho kimetokea, niliongea hii hoja. Nakumbuka uliniambia sasa umeona umetoa ya moyoni sasa utulie umeongea umesikika na unakumbuka, hoja ilikuwa ni hii hii. Bunge liliopita mwezi wa Kwanza nimeuliza swali na *hansard* zipo, Mheshimiwa Waziri kwa mdomo wake anasema tatizo ni VAT, Serikali kutaka kodi na akasema mgogoro wa kodi umeisha. Amekiri mwenyewe na *hansard* zipo kama ni uongo mimi leo naacha ubunge, *hansard* ije hapa, kama ni uongo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuendesha nchi kwa ujanja ujanja, huwezi kuwa Waziri unakuwa mjanjamjanja, uongouongo hauwezekani. Majibu ya Serikali lazima yawe ya ukweli, watu wanaiamini Serikali, wanaamini jibu la Serikali; leo unapokuwa unajibu hili, kesho jibu hili maana yake *commitment* yako wewe haipo. Kwa hiyo niseme kwenye hili nasema wazi Mheshimiwa Waziri ametudanganya, amedanganya Bunge kwa sababu tayari kuna *hansard* za majibu yake akisema shida ni VAT. Haiwezekani Serikali ambayo wanasema wana fedha wanaanza kugombania fedha za msaada, haiwezekani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kila siku wanasema hapa, nchi hii ina fedha, nchi iko vizuri, wazungu wanatujengea barabara wao hawataki, haiwezekani, haiwezekani. Nimwambie Mheshimiwa Waziri asisingizie habari za mvua, mvua tangu

mwaka 2017 mpaka leo, mwaka 2017 mpaka leo mvua gani hiyo, Mvua ya Nuhu! Ni gharika! Ni gharika nasema! (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sisi tunaumia sana, nyie kama mnakaa huku kwenye viyoyozi barabara safi, sisi kule tuna shida hatujihisi kama tuko Tanzania. Haiwezekana halafu Mheshimiwa Waziri anakuja hapa anaongea vitu vya uongo kabisa, haiwezekani, haya mambo yanaudhi, Mheshimiwa Waziri namwomba sana aheshimu kiti alichokaa hapo na mwaka huu tunawang'oa. (*Makofi*)

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, mwongozo.

SPIKA: Mheshimiwa Lijualikali ni kengele ya kwanza, lakini naona yuko juu sana nataka nimpe likizo kidogo, nimrudishe baadaye ili atulie kidogo. (*Kicheko*)

Unaonaje dakika tano zako nikikupa baadaye.

MHE. PETER A. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Spika, ni sawa haina shida.

SPIKA: Ili upoe kidogo.

MHE. PETER A. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Spika, ni sawa haina shida.

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. PETER A. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Spika, ameniudhi.

SPIKA: Anafuata Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Zainab Katimba atafuatia.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii na naungana na wenzangu kumuunga mkono mtoa hoja Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Hotuba hii ni elekezi kwa maana ya utendaji Serikalini lakini pia mengi yaliyozungumzwa sisi ni mashahidi yanavyoendelea katika maeneo yetu tunakotoka. Ni ukweli ambao haufichiki kwa kweli, nikitisha *almost* kila Jimbo limeguswa labda nitakuwa nazungumza kwa niaba ya wenzangu ambao mahali pengine sina taarifa sahihi, lakini ukweli ni kwamba, mambo makubwa sana ndani ya miaka mitano hii yamefanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano tu, sisi huko Sengerema kwa mfano kwenye bajeti hii ambayo tunaihitimisha tarehe 30 mwezi Juni, tumetengewa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya jambo jema kabisa kama ambavyo zimo halmashauri nyiningine 26 ukijumlisha na kwetu tunakuwa na 27. Taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inaonesha kwamba kwenye bajeti hii ambayo 2018/2019 kulikuwa na hospitali za halmashauri 69 zimejengwa, kwa hivi ni jambo kubwa ambalo hatukuwahi kulifanya miaka mingi toka nchi yetu ipate uhuru.

Mheshimiwa Spika, pia huko Sengerema wamenituma niipongeze Serikali kwa kutenga fedha shilingi milioni 750 kwenye bajeti ambayo itaanza tarehe 01Julai, mwaka huu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala, jengo la Mkurugenzi pamoja na ofisi nyiningine. Sisi tunasema ahsanteni sana Serikali kwa kutujali, kwa kutukumbuka, kama ambao mnawakumbuka maeneo mengine, hatuwezi kuyazungumza yote kwa sababu mijadala ya kisekta inakuja.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu waliochangia kukupongeza wewe kama Kiongozi wetu Mkuu wa Mhimili huu, wewe pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyevitii wa Bunge hili Tukufu wakisaidiwa na Watendaji wakiongozwa na Katibu wa Bunge, Ndugu Kagaigai mmeefanya kazi kubwa sana. Ni vyema tuweke kumbukumbu sahihi, pamoja na kwamba Bunge hili majukumu yake ya msingi ni ya kutunga sheria na kuvisimamia Serikali, lakini yako mambo ya msingi wewe uliyoyafanya ni vyema taifa likaendelea kuyakumbuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, moja, umelifanya Bunge hili litoke kwenye utengaji kazi wa *analogy* tukahamia kwenye *digital*, tunafanya kazi kwa kutumia mitandao, umelifanya Bunge liwe *e-parliament* ni jambo la msingi sana tunakupongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye ukurasa wa 18 aya 32 utaona pale Serikali inakiri yenye we kwamba michango ya Bunge lako Tukufu imesaidia sana kuanzisha Mfuko wa Maji, lakini pia tukatengeneza utaratibu wa kuanzisha chombo maalum kwa ajili ya maji vijijini (*RUWASA*) jambo la msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kikubwa tunakupongeza wewe na wasaidizi wako kwa namna ambayo ulisaidia kusimamia hii hoja hatimaye Serikali kwa kushirikiana na wewe, kwa kushirikiana na Bunge Tukufu hili tukafanikiwa kuanzisha hiki chombo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo tunakukumbuka wewe, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenye viti wetu ni kwa kuanzisha na mimi nazungumza hapa nikiwa na *interest*, kuianzisha ile Kamati ya Sheria Ndogo, naomba Waheshimiwa Wabunge wanisikilize vizuri hapa, simaanishi kwamba Kamati ya Sheria Ndogo ni ya muhimu sana, lakini wenye historia ya Bunge hili wanafahamu hii ni kamati ambayo imekuwa ikiingia na kutoka. Tunafahamu ilishaingia huko nyuma ikatoka, ikarudi ikatoka na sasa imeingia tena.

Mheshimiwa Spika, umefanya jambo kubwa sana tunakupongeza kwa sababu yale ambayo tunayafanya sisi chini ya uongozi wetu wa Mheshimiwa Chenge kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla kama kusingekuwa na kamati mahsusimaa maalum kuzungumzia mambo haya na hii ni Kamati inayoshughulika na Sheria Ndogo. Masuala ambayo kila siku ndiyo yanasisimamia uendeshaji wa maisha ya Watanzania, ina maana kwamba wananchi kwa kiwango kikubwa wangkuwa wanaumia

kwa yale ambayo Serikali ilipitiwa ama kwa kutoyaona au kwa kutoyapa tu nafasi yake na sisi tunakuja kuyabaini na kuyafanya kazi. Kwa hiyo tunakupongeza sana, lakini tujipongeze wote kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la nne ambalo napenda kuliweka kwenye kumbukumbu zaidi ni kwa namna ambavyo una-support suala la michezo. Suala la michezo si la michezo, suala la michezo ni fursa lakini suala la michezo ni afya na suala la michezo ni kiwanda kinachotembea. Tukizungumza kwa muktadha wa hapa Bungeni mimi ni Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, nakupongeza na kukushukuru sana kwa namna ambavyo umetupa support kwa miaka mitano yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze jambo moja ambalo nimelibaini kwenye hotuba hii. Ukitosoma mafungu haya na hasa uchambuzi wa Kamati ya Bajeti. Wanasesma kwenye bajeti makadirio ya fedha iliyotengwa mwaka mpya wa fedha unaokuja hatujatenga fedha kwa ajili ya ushiriki wa michezo kwa Bunge hili, kwenye mashindano ya Mabunge ya Afrika Mashariki. Nina ushauri, ni jambo la kawaida kwamba na tunafahamu wenyewe historia nzuri katika mashindano haya kwamba kwa kila nchi ambayo inakuwa ndani ya mwaka huu wa mashindano ina Uchaguzi Mkuu taratibu zinaruhusu nchi hiyo isishiriki.

Mheshimiwa Spika, nataka nitofautishe ushiriki na mashindano haya yanakofanyikia mwaka huu, mwenyeji wa mashindano haya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka huu ambayo yatafanyika mwezi wa 12 yanafanyikia Jijini Arusha na wenyeyeji wa mashindano haya ni Bunge la Afrika Mashariki. Kiutaratibu wenyeyeji ni *EALA*, lakini kiuhalisia yanafanyikia Tanzania. Naomba Bunge lako Tukufu litafakari vizuri na hasa Kamati ya Bajeti, ile nadharia ya kwamba nchi ambayo ina Uchaguzi Mkuu isishiriki mazingira ya mwaka huu ni tofauti. Jambo la pili juu ya hilo ni kwamba gharama zake kwa mwaka huu kwa sababu mashindano yanafanyika ndani ya nchi ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, nafanya hesabu tu *rough* hapa, sisi kwa mahesabu tuliyofanya kwa ushiriki wa mwaka huu tukichukulia wachezaji 100 ambao wanaweza kwenda kushiriki pale Arusha gharama yake haifikii hata silimia 50 kama mashindano yangefanyika nje ya nchi. Kwa hivyo, najaribu kuzungumzia hili jambo tulitafakari vizuri wakati tunaendela kufanya majadiliano kadri ambavyo majadiliano yanaendelea, kwa sababu kadri tunavyozungumza kwa mfumo tulionao wa bajeti, ndipo pia tunaweza kupata fursa nyingine za kurekebisha mahali hapa ama kule. Kwa hiyo tulikuwa tunaomba sana turuhusiwe.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kulizungumzia ni lile ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu amelizungumzia kuhusu mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara Tanzania. Ni kweli takwimu zinaonesha kwamba tunesogea kidogo kutoka namba ya 144 tukasogea nafasi ya 141, lakini hii inaonesha mazingira yetu ya ufanyaji biashara na uwekezaji bado tuna changamoto kubwa. Ile *blueprint* ambayo imetayarishwa na wataalam wetu nashauri kwamba ifanyiwe kazi, tuitekeleze rasmi kwa sababu inafungua fursa lakini pia inarekebisha kasoro nyingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kasoro moja, mimi ni mpenzi wa kuwa na vyuo vikuu vinavyomilikiwa na umma kikanda. Tunafahamu Dodoma kuna Chuo Kikuu cha Serikali, Dar es Salaam visto, Nyanda za Juu Kusini Mbeya kipo, Arusha kipo, lakini mikoa saba ile ya Kanda ya Ziwa hatuna. Pale Sengerema Sekondari Mheshimiwa Profesa Ndalichako Waziri wa Elimu yuko hapa ni shahidi, kwa maboresho yaliyofanyika kwenye shule kongwe Tanzania na Sengerema Sekondari ni eneo lisilopungua ekari 143, linafaa kabisa kama Serikali itaamua kutafakari vizuri. Tuigeuze ile Shule ya Sekondari kuwa Chuo Kikuu, lakini hilo naiachia Serikali itaendelea kutafakari.

Mheshimiwa Spika, la mwisho Corona; naomba uniongezee dakika moja katika hili, nataka nizungumze kama mwananchi wa kawaida ambaye sina taaluma yoyote katika masuala ya afya, lakini nataka nizungumzie jambo moja la kimapokeo. Tumekuwa tukielezwa kwamba iko tiba ya mafua

ambayo ni ya kienyeji ile ya kujifukizia, sijaelewa ni kitu gani ambacho kimetukumba kama Taifa, sina taarifa sahihi lakini mimi nafahamu pale Muhimbili hasa MUHAS pale kuna Kitengo cha Tiba Mbadala. Yaliyotokea China leo wamedhibiti ugonjwa wa *corona* huu hatufahamu siri zake kwa sababu siri zote hazijitokezi. Ninachotoka kusisitiza na kuliomba Bunge lako Tukufu, wewe unaweza kutumia Kanuni ya 5 kutoa mwongozo kwa Serikali ama Serikali itafakari. Kwa nini hii tiba mbadala ya kimapokeo ambayo wengi tumetibiwa na tukapona kwa miaka mingi hatuipi nafasi katika vita hii.

Mheshimiwa Spika, tuna *corona* hapa ambayo ni janga la kidunia.

SPIKA: Mheshimiwa Ngeleja, malizia.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, hili janga naomba kila nchi ipambane na hali yake kwa mazingira iliyonayo. Kama tulivyosema China hatujajua kitu gani kimewafanya wakadhibiti, lakini kama hili jambo halina madhara kuli-*promote* kwa maana ya Serikali kulizungumza Watanzania wakafanya.

Mheshimiwa Spika, chukulia mfano kila mtu ajifukizie asubuhi yeye na familia yake, kuna hasara gani kama tumejfukizia na tukapata nafuu lakini itatokea nini kama inawezekana kujifukizia kunatibu halafu sisi hatuipi nafasi hii fursa, maana yake ni nini.

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, narudia tena kuunga mkono hoja, lakini naomba jambo hili mlitafakari vizuri. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa William Mganga Ngeleja. Hii kujifukizia hata Ugogoni ipo kwa hiyo siyo ya Kanda ya Ziwa peke yake na haihitaji kuwa kila siku, hapana, hata ukipiga mara moja, kwa wiki, wiki mbili wala haina shida. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mmepata *tipya* bure hiyo, ila sasa usije ukajifukizia yasiyofukiziwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Zainab Katimba, Waheshimiwa Wabunge, kengele ya kwanza ni baada ya dakika saba halafu zinapobaki dakika tatu ndio ya pili inayomalizia. Mheshimiwa Katimba.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani. Kwanza na mimi nianze kutoa pongezi kwa kazi kubwa ambayo ni dhahiri ambayo imefanywa na Serikali ya Awamu ya Tano. Sisi sote ni mashahidi kwa kiasi gani miaka hii mitano imekuwa ni ya utekelezaji wa yale yote yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi, Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2015/2020. Kwa sababu ni dhahiri hata sisi huwa tukizungumza na marafiki zetu wengine hususan hawa ambao wamekaa upande wetu wa kulia, tukiongea kiurafiki huwa wanakiri jithada kubwa ambazo zimefanyika katika utekelezaji wa Ilani.

Mheshimiwa Spika, aidha, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuhakikisha utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini kwa hotuba yake hii ambayo tunachangia leo. Nafahamu kwamba ana wasaidizi wake Waziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na watumishi wote wa Serikali ambao wanafanya kazi hii kubwa, kwa hiyo nipongeze jithada hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika masuala ya vijana na kabla ya kuchangia katika masuala ya vijana ningependa na mimi nigosie changomoto hii au janga hili la kidunia na hasa katika sekta ya afya, la ugonjwa wa *SARS-Cov2* au tuseme *COVID 19*. Ugonjwa huu kama wote tunavyofahamu ni janga la dunia, janga la kiafya ya kidunia

na sisi Tanzania ni nchi mojawapo ambayo imekutwa na ugonjwa huu. Nafahamu kuna jitihada kubwa sana na sisi wote ni mashahidi, ambazo zimefanywa na Serikali katika kuhakikisha kwamba tunautokomeza ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, kuna wazo ambalo lipo katika jamii ambalo naona halijatolewa ufanuzi. Kuna mawazo (*misconception*) kwamba ugonjwa huu hauathiri watu wenyewe ngozi nyeusi kama unavyoathiri watu wa mabara mengine, yaani kwamba Bara la Afrika sisi tuna upekee ambao unatupa nafuu katika kudhurika na ugonjwa huu. Mawazo hayo sidhani kama ni mazuri sana kwa sababu pia yanafanya wananchi wanaweza wakazembea katika kujikinga kwa kuamini kwamba wao wakiwa wana ngozi nyeusi watakuwa wana nafasi kubwa zaidi ya kupambana na ugonjwa huu, hiyo ni moja.

Mheshimiwa Spika, lakini kitu kingine, tunafahamu kwamba ugonjwa huu unaleta athari za kiuchumi. Bila shaka Serikali itakuwa ina mkakati wa kuona ni namna gani inachukua hatua za kifedha ili kupunguza madhara ya kiuchumi yanayotokana na janga hili. Kwa hiyo, naomba Serikali na yenye we iangalie kuona kwamba watachukua hatua gani ambayo itasaidia kuokoa sekta zile ambazo zimeathirika kiuchumi na janga hili la ugonjwa huu

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu wamezungumzia na wametoa maelezo yanayojitosheleza kwa namna gani masuala ya ajira na uwezeshaji yamefanyiwa kazi na mikakati ya kusonga mbele. Mimi nina ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kuhusiana na mfuko kutengwa kwa asilimia kumi ya mapato ya ndani ya kila Halmashauri kwa ajili ya kuwezesha makundi maalum ikiwa ni pamoja na vijana, wanawake na kundi la ulemavu. Tumeona katika kipindi hiki cha miaka mitano kwenye Bunge hili tulifanya marekebisho ya sheria na sasa tumehakikisha kwamba fedha hizi zinatengwa. Ushauri wangu ni kwamba Serikali ione ni namna gani itatengeneza mfumo wa

kielektroniki ambao utaweza kusaidia kufanya michakato yote ya uombaji na utoaji mikopo hii.

Mheshimiwa Spika, pia mikopo hii kuwe na *formula* kwa sababu jinsi ilivyo sasa hivi kila Halmashauri inakaa vikao vyao kuangalia ni kiwango gani cha chini au cha juu kitatolewa kwa ajili ya mikopo. Kwa hiyo, kuna mbinu tofautitofauti zinazotumika katika maeneo tofauti. Kwa hiyo, katika siku za mbele tuone ni namna gani tunakuwa na mfumo wa kielektoniki ambao utasaidia kusimamia na kuratibu mfuko huu kwa ajili ya kuwezesha vijana, wanawake pamoja na kundi la watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, pia tukiangalia kuna Sheria hii ya Manunuzi ya Umma, Sura 410, kwenye kifungu cha 64(2) kimetoa masharti ya kwamba taasisi au tuseme mashirika ya umma yatenge asilimia 30 ya manunuzi yake kwa ajili ya kuwezesha vikundi nya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Naiomba Serikali iweke mkazo na msisitizo kuona kwamba kifungu hiki cha sheria ikiwa ni pamoja na Kanuni zake kinazingatiwa kwa sababu ni eneo pia la vijana wetu, wanawake pamoja makundi ya watu wenye ulemavu kujipatia nafasi ya kutengeneza kipato na kutatua changamoto ya ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa maoni yangu kwenye suala zima la elimu. Sisi sote ni mashahidi ni kwa kiasi gani jitihada zinafanyika kuhakikisha sekta ya elimu inaboreshw Tanzania. Tumeona kuna mkakati wa elimu bure, lakini tunaona Bodi ya Mikopo imeongezewa bajeti kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vijana wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nachoomba, kwa sababu sote tunafahamu tuko katika harakati za kuhahakisha tunatengeneza vizuri uchumi wa viwandana tunajua uchumi wa viwanda unahitaji zaidi kada ya kati, kwa hiyo, kuna kila haja pia tuwekeze kwa hali inayotosheleza katika kada ya kati. Tunaona kuna jitihada tofauti tofauti lakini tuijulize ni kwa kiasi gani hawa wanafunzi tuseme wanaosoma masuala ya ufundi, hawa *technicians*, wale wenye uhitaji kwa mfano wa

kupatiwa mikopo kwa ajili ya kuwezeshwa wao kupata taaluma hizo umewekwa kwenye utaratibu kama vile tunavyoona kwenye Bodi ya Mkopo.

Mheshimiwa Spika, hawa *graduates*, unaweza ukawa na Mhandisi mmoja akasimamia Mafundi Mchundo 20 au Mafundi Sanifu hata 60 lakini hawa Mafundi Mchundo pamoja na mafundi Sanifu wanahitajika wengi zaidi. Sasa itakuwa vizuri zaidi kama pia tukijielekeza katika kuhakikisha tunatengeneza mazingira wezeshi zaidi kwa ajili ya kada ya kati kwa sababu yenyewe ndiyo itakayohitajika zaidi katika uchumi wa viwanda tofauti na hizi ngazi zingine za elimu ya juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia katika suala zima la elimu tufanye maboresho ya mitaala ya elimu ili iweze kumuandaa mhitimu kuweza kuwa na uwezo wa kutengeneza pesa. Nina maana kwamba mitaala yetu ya elimu iwe inampa mhitimu *financial literacy*, kwamba akishamaliza kusoma, je, ana uwezo wa kutengeneza pesa? Kwa sababu hiyo ndiyo hoja ya msingi. Unaweza ukawa na *degree* hata nne lakini kama zile *degree* zako hujaweza kuzibadilisha katika uzalishaji na kujitengenezea kipato ina maana zinakuwa hazijasaidia. Kwa hiyo, tuone ni namna gani tunaboresha mitaala ya elimu ili iweze kuwaandaa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Spika, kuwaandaa wahitimu kuwa na uwezo wa kuzalisha pesa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja hii muhimu sana ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza, napenda kushukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano na hasa Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya hususani kwenye mambo ya miradi mikubwa ambayo inaendelea. Napenda pia kumsifu Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri na Naibu Mawaziri wote ambao wapo katika Ofisi yake, wanafanya kazi kubwa na tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kufanya ziara yake Muheza, katika Mkoa wa Tanga. Naamini alipokuja ziara imeweza kufufua mambo mengi na wananchi wa Muheza hawawezi kumsahau hususan kwenye suala la maji ambapo aliongozana na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Waziri. Kwa kweli kuja kwake kulfanya tenki kubwa ambalo linajengwa pale Muheza la lita laki saba liweze kuja maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, najua Mheshimiwa Waziri Mkuu aliacha kiporo lakini yale maji kwenye lile tanki la lita laki saba bado yamejaa. Tunaamini kabisa kwamba atakaporudi basi atawea kuyafungulia na wananchi wa Muheza waweze kupata maji. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kukupongeza hasa katika kuingia kwenye *digital*, sasa hivi tunatembea na *tablet*. Hata hivyo, tulikuwa na mawazo kwamba basi Bunge lijalo watakaorudi waweze kuwa na *screen* katika *table* zao ingekuwa ni vizuri sana. Tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, napenda kuchangia mambo yafuatayo. Pale kwa Waziri Mkuu kuna Kitengo cha Maafa lakini kwa kweli hakipewi umuhimu unaostahili. Kitengo kile naamini kabisa kina upungufu mkubwa wa fedha na ni vizuri kikaimarishwa kwa sababu mafuriko ambayo yametokea wakati huu wataalam wanasema hatujawahi kuyapata katika kipindi miaka 15 au 20 iliopita. Kitengo kile kikiimarishwa naamini kitaweza kusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, sisi tuliambari kwa kiwango kikubwa sana kule Amani ambapo kwenye ziara ya Waziri Mkuu pia tulikuwa tumpeleke Amani lakini tulishindwa kumpeleka kutokana na barabara. Mafuriko yaliharibu sana barabara za kule na mpaka sasa hivi barabara za kule vijiji kuna sehemu kata huwezi kupita. Kwa hiyo, tunaomba kabisa kwamba Kitengo kile kiimashwe na *TARURA* ambao wanashughulika na barabara za vijiji waweze kuongezewa fedha kwa sababu kazi wanayofanya *TARURA* ni nzuri, lakini uzuri wake hauonekani kwa sababu ya ufinyu wa bajeti ambayo inapatika.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kushauri kwenye Kitengo cha Uwekezaji cha *TIC*. Utaona kwamba Kitengo kile kina Mkurugenzi Mkuu mzuri sana na kuna kitu kile wanakiita *One Stop Center* lakini Maafisa ambao wamebekwa pale hawana uwezo. Maafisa ambao wamebekwa pale kutokana na Wizara zao ili waweze kukifanya kile Kitengo kiwe *the real One Stop Center* hawa uwezo wa kutoa vibali, leseni, kuangalia ni vitu gani ambavyo mwekezaji anatakiwa kupewa bila kupata *consultation* tena kutoka Wizarani, sasa hiyo inakuwa siyo *One Stop Center*. Inatakiwa Maafisa ambao wanapelekwa pale wawe na uwezo wa kuamua, wawe na uwezo wa kutoa vibali na kufanya mambo yote yanayohusiana na mwekezaji. Anachotaka mwekezaji akifika *TIC* apate vibali vyote pale siyo aambiwe tena aende *Labour* au *TRA*, hapana, ule ni usumbu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri tuangalie uwezekano wa kukiongezea nguvu. Waheshimiwa Mawaziri ambao wako kwenye Wizara zinazohusika wapeleke *Senior Officers* pale ambao wanaweza kutoa maamuzi, hapo ndio tunaweza kukifanya kiwe *One Stop Center*.

Mheshimiwa Spika, nilitoa mfano kwamba twende Mauritius, ni nchi ambayo *One Stop Center* yake wanaikiita *Mauritius Enterprise*, ina *lead*. Pale mwekezaji akienda, *at the time* naondoka pale ilikuwa *three days* anakuwa amepata kila kitu sasa hivi naambiwa ni *some hours*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Waziri mhusika kwanza namshauri sana aende Mauritius, aangalie *One Stop Center* yao iko vipi, Mauritius *Enterprise*, naamini atajifunza. Hapa tunasema kwamba mtu anapata vibali siku saba lakini mwekezaji anakuja hapa na siku saba hizo anakuwa hajakamilisha kupata vibali vyake. Sasa tutakapokamilisha mambo haya nafikiri yatasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaitwa *roadmap* ambacho amekiongelea Waziri kwenye Kamati na pia *blueprint*. Ni vizuri hiyo *blueprint* basi itoke maana imekuwa ni kama kizungumkuti, kila siku inasemwa iko tayari lakini haitoki. Kwa hiyo, ni vizuri mambo haya yaweze kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, kuna miradi mikubwa ambayo imekwama hasa ukiangalia Mradi wa Bomba la Mafuta, umeanza kwa nguvu sana sasa hivi naona mambo yamepoapoa sjui kwa nini. Vilevile *LNG Project* nayo ilianza kwa nguvu sana imepoapoa. Twende Mchuchuma na Liganga nayo ilianza kwa nguvu sana nayo imepoapoa. Hivi vitu unaambiwa kwamba bado majadiliano yanaendelea, ni vizuri hayo majadiliano yaendelee na yamalizike na kama pia kuna *compensation* ambazo watu wanatakiwa walipwe basi walipwe.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni *Corona* ambalo kwa kweli ni janga kuu Waheshimiwa Wabunge wameliongelea kwa hisia tofauti na kubwa sana. Ni vizuri basi Serikali ikatenga fungu maalum, kwa sababu tumeangalia kwenye Mpango halikuwepo, lakini ni vizuri ikaja hapa na mpango, tusingoje hali ikawa *worse* tutashindwa kuizua. Ni afadhalii sasa hivi Serikali ije na mpango ambao utaeleza, najua kuna Kamati ambayo imeundwa, lakini Kamati haijaja na taarifa yoyote ambayo inaelezea ni kitu gani hasa ambacho kinatakiwa, kama ni suala la *financial* basi zitengwe.

Mheshimiwa Spika, hata wewe kwenye Kamati ya Uongozi uliongelea hata Bunge lenyewe lichangia na Wabunge tuchangie lakini tukasema aah, aah. Hata hivyo, ni vizuri pia ukafikiria tena ili tuone kwamba na sisi mchango

wetu kama Wabunge, siyo kama ulivyosema siku ngapi zile hata siku moja, siku mbili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajabu. Umechangia mambo mengi mazuri sana lakini mojawapo ni hilo la tukifika mahali na sisi mkono wetu kama Wabunge uonekane katika kuchangia mapambano dhidi ya janga hili, tusiwe tunaongea tu mdomoni. Mara nydingi sisi tumekuwa ni mfano, nadhani tukifika mahali tukishauriwa itatusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Moses Mlata.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, nami naomba niungane na waliotangulia kukupongeza wewe na timu yako, Makamu wako na Katibu wa Bunge kwa jinsi mnavyotuendesha. Mimi mwenyewe hapa nasimama kwa nguvu za Mwenyezi Mungu nikiamini kabisa kwamba Bunge litakapokutana Novemba, 2020, nitakuwa nimeng'atuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa muda ambao tumekaa pamoja na hasa nikijielekeza kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye tunajadili hotuba yake. Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa karibu sana na sisi watu wa mbali, wa Kagera, ametembelea Jimbo langu. Juzijuzi kama mlezi wa Chama cha Mapinduzi, Mkoa wa Kagera alikuja kututembelea na kuangalia hali yetu. Naomba tumpigie makofi Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni nzuri, mipango ni mizuri lakini nyakati zenyewe ndiyo siyo rafiki. Kwa hiyo, nami sina budi kuungana na Wabunge wengi, wanasema *the time demand action*, Corona ni tukio

ambalo limetokea na huwa linatokea miaka mia moja mia moja ukiangalia historia ya *pandemic*. Mara ya mwisho limetokea 1918/1920, *Spanish Influenza* ambayo iliua watu takribani milioni 15, 20 au hata zaidi maana takwimu zinatofautiana na sasa hapa tuna hii *pandemic*.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite kwenye suala hili kwa sababu ni muhimu sana na lina *demand* kwamba tuliangalie kama Bunge. Uwezo wetu Afrika ku-*respond* kwa mambo ambayo nyaona kwenye mtandao yaliyotokea China, London St. Thomas ambapo Mwalimu wetu Nyerere alitibisha na umauti umemkuta pale, wagonjwa wamelala chini na hata St. Mary's. Juzi nimemuona Meya wa New York akilia hana *ventilators* sisi *ventilators* hatutaweza kuzipata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nirudie alichokisema kwa ufupi sana Mheshimiwa Ngeleja kwamba sisi ni lazima tuwe na mpango mbadala ambao unajikita katika jamii yetu. Lazima tuhimize kunawa lakini tunapozungumza hapa kuna hospitali zingine hazina maji. Kunawa ni lazima lakini wananchi wetu wengine hawana maji. Kwa hiyo, huwezi kusema kwamba mkakati ni kunawa wakati unajua nusu ya watu hawana maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sisemi kwamba tuisinawe nasema kwamba ikiwa zahma ikitufikia kama tunavyoiona kule itakuwa kizungumkuti. Hapa ndipo naungana kabisa na kumpongeza Rais wetu tunaanza na sala kwa sababu lazima tukiri kwamba mpaka sasa hivi Mungu ametuhurumia, tumshukuru Mungu jamani. Ametuhurumia kwa sababu yale yanayotokea yangefika hapa hatuna uwezo wa ku-*respond*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasa nachotaka kupendekeza, hapa ndipo nasema jamii inahitaji *survival strategies* ambapo kujiuliza tiba zetu mbadala (za asilia) ziko wapi? Hakuna jamii yoyote itakayokaa na kusubiri kifo lazima itajihami. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu asipopitisha dude hili mbali tukafikia pale walipofika ni lazima tuangalie makabila

yetu mbalimbali maana yana mbinu mbalimbali za kukabiliana na homa za mapafu.

Mheshimiwa Spika, wanasema *Covid19*ni mpya lakini siyo mara ya kwanza kwa *virus* kama hivi kutokea. Kufukiza ni muhimu lakini unahitaji mkaa na kuni. Kwa hiyo, ni lazima sisi kama Serikali tuhakikishe watu wanapata mkaa yaani wawe nao karibu, watu wawe na sigiri, wawe na kuni karibu maana katika tiba zetu nyingi asilia inabidi uwe karibu na joto.

Mheshimiwa Spika, nataka kuomba Wizara ya Afya na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile nimeshamwandikia barua rasmi nikimweleza kwamba ni lazima tuangalie pia *option B*. Sisemi kwamba tusitekeleze *option A*, tuvae *mask*, tutafute *ventilators* lakini kama watu wengi watakuwa wameambukizwa ni lazima tuangalie namna ya kuwaokoa na mimi naamini kwamba wataokoka. Nimeangalia *figures* leo, Ghana sasa hivi wameshapona watu 33 wakati Holland hakuna hata mtu mmoja amepona kwa sababu wao wamerudi kwenye muarobaini, wanafukiza wagonjwa na wanapona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mambo haya naomba kusema kwamba Wazungu hapo wametupoteza. Tuna kasumba nyingi na huwezi kuwalamu Madaktari wetu, wengi wamekuwa *trained* kwenye *western tradition; oxford tradition*, wanabeza mambo yetu kana kwamba sisi kabla ya Wazungu kuja tulikuwa hatuishi au tulikuwa hatuugui. Kwa hiyo, tiba mbadala ni kitu muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimeona niliseme hili kwa sababu ni *survival strategy*, ni lazima Serikali sasa isaidie. Kule kwangu kuna *barrier* fulani wanazuia watu wa mkaa, sijui wanataka watu wapikie nini! Unamwuliza mtu wa mkaa; mtu haruhusiwi kuwa na mkaa wake wa kupikia kwa mfano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kusema kwamba nionavyo mimi katika kukabiliana na hili *Covid- 19*ni kwamba tuangalie *Plan A* na *Plan B*. *Plan A* ni hii ambayo tunayo *standard procedure*, hospitali; *Plan B* ni kwamba kama

tukizidiwa, lazima tupeane maarifa; Wagogo wanafanyaje? Wapogoro wanafanyaje? Wanyakyusa wananyaje? Wahaya tunafanyaje? Kwa sababu hii *knowledge* ipo, ni *indigenous knowledge*, lakini inakuwa *ignored* watu tumekuwa *brainwashed*. Sasa sisi na wengine wengi humu ni vijana siwalaumu, ninyi hamkukulia vijijini. Sisi tumelelewa na wazee, tumeshuhudia haya mambo. Sasa watoto wa mjini hawayajui haya mambo kwamba *Plan B* iweipo kusudi Afrika iweze ku-survive. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaposema hivyo, niseme pia, magonjwa mengine tusiyasahau, kwa sababu na yenye we yatakuja kukuza hili tatizo. Kule kwangu Muleba, kule kwenye Hospitali ya Wilaya hatuna damu salama. Kwa hiyo, kuna wanawake watatu walipoteza maisha wakiwa wanajifungua kwa kukosa damu salama. Kwa hiyo, naomba hili nalo liangaliwe. Kwa sababu tusipoweka mambo ya kulinda sehemu nyininge ambazo zitatuletea matatizo, hata na hii *Corona Virus*, kama Mungu akitusaidia; na vile vile tusali; na tunaposali hata nyumbani unaweza ukasali, sio lazima uwe na mkusanyiko mkubwa kusali, lakini Mungu yupo kila mahali, au sio! Hata na hapa Bungeni tunaweza tukasali, mahali popote ni mahali pa ibada.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani hilo nimelisema, lakini nawasiliana na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, nimeshamwona, nami najaribu kutoa mawazo kwa sababu *the time reminds it*. Ni dhana kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda ni mfupi, hilo nadhani tutaendelea na naomba nimpongeze Mheshimiwa Ummy Mwalimu, kwa kweli naona kama ni Jemedari. Namsikia kila siku anatangaza, yaani *she is doing a great job*. Sasa tumsaidie na sisi katika kutafuta hii *Plan B*.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Profesa.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Spika, ni dakika saba, nimeweka *stop watch* hapa. Ni dakika saba. Nimeweka *stop watch*, ninayo hapa dakika ya nane sasa. (*Makofii*)

SPIKA: Basi malizia, inaelekea *stop watch* ya Katibu wangu ina matatizo.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Spika, katika dakika zangu hizo mbili kwa ruhusa yako, niendeleee. Kitu kingine ambacho nataka kuongea na ni cha kimkakati, tunampongeza Mheshimiwa Rais wetu, anafanya kazi nzuri sana, lakini naomba kwa kupitia Bunge lako hili Tukufu nipeleke maombi maalum kwa Mheshimiwa Rais Magufuli. Program ya *NIDA* kwa sasa hivi ni kama imefeli.

Mheshimiwa Spika, *NIDA* kama ilivyo sasa hivi, imekuwa kero kubwa kwa wananchi kwa sababu simu zao zimefungwa. Sasa sijui ninyi wenzangu huko kwenu mkoje, lakini kule kwangu Muleba, watu simu zao zimefungwa na mtu ambaye umemfungia simu, hata kama umefanya mambo mazuri mangapi atakuona kwamba umemharibia. Kwa hiyo, naomba kitu hiki kilipofika; na zoezi lenyewe la *NIDA* ni zuri lakini mkakati ndiyo kwa kweli haujitoshelezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba Afisa Uhamiaji wanaodhibiti uhakiki wa hizi namba, warudishe na wakasimu madaraka yao kwa Watendaji wa Vijiji. Kwa sababu mtu atakayejua kama mimi ni Mnyarwanda au ni Mtanzania ni kijiji changu au siyo! Haiwezi kuwa ni mtoto mdogo, *migration officer* namkuta kwenye Wilaya eti ndio anasema mimi sio Mtanzania. Kwa hiyo, unakuta hizi ni kero kwa wananchi na kwa upande wa Muleba na mikoa ya pembezoni. Huko pembezoni kwa kweli imekuwa kero kubwa. Sisi kwa upenzi wa Rais wetu lazima tutoe *feedback* ya hali halisi ilivyo. Kwa hiyo, hilo naona niliseme kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa kupitia ofisi yako, nashukuru kwamba umemwandikia Mheshimiwa Jenista Mhagama, nakukabidhi hoja yangu binafsi ambayo

nimehangangaika nayo tangu Bunge la Kumi. Naomba kabisa Bunge lako tukufu, kwa kuwa naamini kabisa wewe unaendelea kabisa, tutakuwa nawe katika Bunge linalofuata, Mheshimiwa Jenista Mhagama naomba *record* ya *Hansard* irekodi kwamba nimekukabidhi hoja yangu binafsi, kwa sababu najua kwamba Mheshimiwa Spika, alikukabidhi hoja ile.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Waunge, hoja hiyo ilikuwa inasema hivi, baada ya kukumbwa na tatizo la *ESCRO* nikajikuta katika *situation* ambapo nahukumiwa na Bunge, niko ndani ya Bunge, ni Mbunge na siruhusuwi kusimama kujitetea. Nikaona tuna upungufu mkubwa sana katika mfumo wetu. Kwa hiyo, nimehangangaika na hoja binafsi na Muswada binafsi.

Mheshimiwa Spika, Bunge la Mheshimiwa Makinda wakasema hatuna wakati; Bunge lako hili wakati haukupatikana, lakini angalau umepiga hatua umeikabidhi Serikalini. Kwa hiyo, naomba niukabidhi *rasmi for the sake of the record* nina historia kwamba ioneckane kwamba Muswada binafsi, lazima Wabunge wawe na uwezo wa kuandika Miswada binafsi. Kazi ya Mbunge ni kutunga sheria, siyo lazima kujadili tu sheria zinazoletwa na Serikali, mwisho wa siku lazima Serikali itakuunga mkono. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni jambo kubwa na la msingi ili kuboresha demokrasia yetu. Nadhani muda wangu umekwisha. Nakushukuru kwa kunivumilia. Nawashukuru sana wananchi wa Muleba Kusini kwa kunipa nafasi kuwa na ninyi katika Bunge hili. Miaka 10 nimejifunza mengi, naenda kuandika vitabu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, unafanya kazi nzuri. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Profesa Tibaijuka. Hii ni *speech* maalum kabisa kwetu. Tunajua bado tuko nawe na utachangia tena bajeti hii inavyoendelea, lakini ni katika

kuendelea kutuaga. *We are proud of you, tunathamini sana mchango wako. (Makofi)*

Kwa kweli anastahili makofi ya Bunge zima, mimi naomba tumpigieni makofi. *(Makofi)*

Ahsante sana Mheshimiwa Profedsa Anna Tibaijuka.

Nilishakutaja Mheshimiwa Martha Moses Mlata, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga. *(Makofi)*

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nakushukuru kwa nafasi hii. Kwa sababu bajeti hii inagusa na Mfuko wako wa Jimbo wa Bunge nilikuwa naanza nataka nianze kwa kutoa shukurani kwanza kwako, nikianza na Mwenyezi Mungu kwa hali hii niliyosimama hapa.

Mheshimiwa Spika, nina mwaka sasa zaidi na miezi kama mitatu/minne sijasimama hapa Bungeni kuchangia, lakini leo Mungu ni mwema sana kwangu, nimeweza kupata nafasi hii ya kuweza na mimi kusimama na kuongea mbele ya Bunge lako Tukufu kuweza kutoa mchango wangu. Mungu wetu ni mwema na atukuzwe sana, tuzidi kumwamini na kumtegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Rais, nikushukuru wewe kwa sababu Mfuko huu wa Bunge umetajwa na umetaja huduma za afya kwa Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya matibabu. Siwezi kusimama nianze kuzungumza tu bila kuupongeza mfuko huu ukiongozwa na wewe pamoja na Katibu wa Bunge na Viongozi wengine ukisaidiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama anayeshughulikia masuala ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, mmenitunza, mmenitibu na leo nimesimama hapa. Mungu akubariki sana na wote waliohusika. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye alifuatilia sana afya yangu. Mungu akubariki sana. Sina maneno mengine ya kusema, bali Mungu aendelee kukubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, ninashukuru madaktari wote na Mheshimiwa Waziri Ummu pamoja na Naibu wake. Nasema waendelee hivyo kwa sababu wataokoa maisha ya watu walio wengi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya shukurani hizo, kwa kweli bado nitaendelea kutoa pongezi. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakupongeza sana pamoa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, tunaye Mheshimiwa Angella Kairuki, tunaye Mheshimiwa Stella Ikupa mama yangu. Nikimtaja Mheshimiwa Stella Ikupa mama yangu, ninataka nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa sababu nami nikimtaja Mheshimiwa Stella Ikupa, mama yangu ni kama Mheshimiwa Stella Ikupa. Nafikiri mnanielewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hilo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutambua mchango mkubwa wa watu wenye ulemavu, kuwapa nafasi kubwa kwenye Serikali yake. Ameonesha kwamba anawenza. Ni kweli wanawenza. Mheshimiwa Rais Mungu ambariki sana, kwa sababu sisi ni watoto wa akina Mheshimiwa Mama Stella Ikupa kama Stella. Mama yangu amenilea mpaka nimefikia hapa nipo ndani ya Bunge, siyo kwa sababu ya ulemavu, bali ni kwa sababu wanawenza. Nakupongeza sana Mheshimiwa Stella Ikupa.

Mheshimiwa Spika, pia kijana wetu Mheshimiwa Mavunde, ni kweli vijana wanawenza na ameonesha mfano mzuri na vijana wataendelea kuaminiwa kwenye Uongozi Serikalini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyoifanya, nataka niseme ameongoza vizuri. Mawaziri wote tumewaona jinsi ambavyo wamechapa kazi kwa sababu ye ye amekuwa mchapakazi. Nilikuwa namwita Mheshimiwa Mzee Kamwele pale, nimesema leo nitaanza kukuita mzee. Nilimwona ameingia kijana, lakini sasa hivi naona amezeeka; ni kwa sababu ya kuchapa kazi; asubuhi huku, jioni huku, usiku yumo, kwa hilo,

ni lazima anaonekana mzee kwa sababu amechapa kazi. Mheshimiwa Waziri Mkuu umeongoza kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, nikimwangalia Mheshimiwa Mzee Mpango pale, namwita Mzee Mpango kwa sababu alilingia kijana, sasa namwona ni mzee kwa sababu ya gwaride ambalo wamelichapa. Kwa kweli wanaweza, wamefanya kazi nzuri sana, ninaamini huko Majimboni watakapokwenda hawatakuwa na Wapinzani kabisa kwa sababu Taifa hili bado linawahitaji sana. Ni pongezi hizo za kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna jambo moja ambalo pia nataka tu nipongeze wakati namwangalia Mheshimiwa Mpango pale, kweli Watanzania wamelipa kodi sana. Mara ya kwanza tulikuwa tuna wasiwasi, watu wakasema kuna watu wanaondolewa leseni zao, miradi inafungwa, nani atakayelipa kodi? Kwa kweli tuna kila sababu ya kuwapigia makofi Watanzania, wamelipa kodi ndiyo maana maendeleo yamerudi kwao. Huu ni usimamizi mzuri wa Serikali, wamekuwa waadilifu walipa kodi na sisi tumerudisha.

Mheshimiwa Spika, ukirudi nyuma pesa ambazo tulikuwa tukipitisha hapa zilikuwa haziendi au zinaenda kidogo, lakini safari hii zimekwenda, watu wamefanya kazi. Michango imelipwa, kodi zimelipwa, maendeleo yamekwenda, ukienda kwenye upande wa afya, tumefanya vizuri; ukienda kwenye upande wa barabara, tumefanya vizuri; ukienda kwenye upande wa elimu, mpaka hii elimu bure, nilikuwa namwangalia yule mtoto wa pale Simiyu, machozi yalinitoka. Nikasema hivi isingekuwa elimu bure, mtoto *genius* kama huyu tungemwona wapi? Sasa kwa sababu ya elimu bure, kuna watoto wengi kama ye ye ambao hatukuwaona wameweza kufanya vizuri na wamebadilisha maisha yao. Kwa kweli nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na tunampongeza Mheshimiwa Rais, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa afya ukienda hata kule kwetu Mkalama kwa Wahadzabe tulikuwa hatuna hospitali, lakini sasa hivi aka! Mambo ni safi. Akina mama

wakiingia, mtoto wake wa kike, wa kiume anatoka salama bila matatizo, kwa sababu vituo na zahanati zimefika kwenye maeneo yote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine tu nilikuwa nataka kusema, nilikuwa nasikiliza sana, jana nimesikiliza ile *speech* ya Mwalimu huwa inarudiwa ya yule mposaji. Kwanza ilikuwa ni baada ya Aridhio *TBC*. Pamoja na kutamka *TBC*, niseme tu, Mwenyezi Mungu aiweke mahali pema Peponi roho ya Marehemu Marin Hassan Marin kwa sababu alikuwa ni mtangazaji mahiri sana.

Mheshimiwa Spika, kile kipindi kilionyesha Mwalimu Nyerere akisema, yule kijana mposaji; ile kuzomewa huyo, huyo, huyo, eeh, huyo! Mimi nilikuwa natafakari sana, nikasema Mheshimiwa Waziri Mkuu zile kelele za huyo, huyo, huyo, tumeshinda. Kwa sababu kuna mambo mengi ambayo tusingeweza kuyafanya kama Mheshimiwa Rais asingeziwa masikio. Tumenunua ndege, bwawa la kufua umeme, reli inakuja na mambo engine mengi kweli. Kama angeweza kusikiliza zile kelele za huyo mkamate, huyo hawezi, huyo anadondoka, tusingeweza kufika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba tuendele, tusonge mbele kwa sababu bado hatujafika. Kwa hili nataka tu niseme kwamba namwombea Mheshimiwa Rais wangu, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, kazi aliyoifanya ni kubwa sana, hatuna sababu kwa sababu mimi najua kabisa ndugu zetu hawa wako kwa ajili ya kukosoa yale mambo ambayo hatuwezi kufanya, lakini yale mambo yaliyofanyika hakuna sababu hata ya kumpeleka Mheshimiwa Rais akaanza kuomba kura. Anaomba kura wapi?

Mheshimiwa Spika, wananchi wameziona kazi; anaomba kura za nini tumsumbue barabarani huko, azunguke akaombe kura! Tunamwacha, sisi tupambane kwenye Majimbo huku, nafasi ya Rais ibaki yule yule. Ninjiooni kwenye Majimbo tupambane, lakini Rais abakie yule yule kwa sababu anatosha kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kabisa, wewe ni mtani wangu, najua utarudi tu, mimi nitakutambikia, wewe usiwe na wasiwasi, hakuna mtu atakuja pale, wewe tulia tu. Wewe chukua fomu, rudisha, njoo endelea kuandaa Bunge linalokuja kwa sababu wengi wetu tutarudi kutokana na kazi kubwa ambayo Serikali hii imeifanya na wananchi wameiona. Kwa hiyo, hakuna mpinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo nilitaka nizungumze ni suala la *Corona*. Mheshimiwa Rais alionesa mfano mzuri sana wa imani na watu wameendelea kusali. Nataka niwaambie, tuendelee kusali lakini pia huku tukichukua tahadhari, tukiwafuata viongozi wetu wataalam wanatuambia nini? Ukipali na huku ukamwomba Mwenyezi Mungu na ukachukua tahadhari, huwezi ukawa juu ya mtu ukasema wewe jirushe tu Mungu atatumwa Malaika, hapana. Ni kwamba unashuka taratibu na Mungu atakusaidia, utashuka kwenye huo mti. Kwa hiyo, tuendelee kusali, tumwombe Mwenyezi Mungu huku tukichukua tahadhari zile ambazo tunaelekezwa na viongozi wetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Mama Tibaijuka ye ye amezungumza kuhusu tiba asilia nikamkumbuka, mimi ni wifi yangu. Ukienda kwa shemeji zangu kule wana dawa moja hivi; ukiumwa Malaria hawakupeleki hospitali. Nikapima, wanakwambia wewe tulia, kuna dawa moja inaitwa Omushana. Kwa hiyo, nikamkumbuka, nikasema siyo ajabu ameshaanza kunywa Omushana ile ambayo huwa inapandisha *immunity* zile ambazo zinasaidia kupambana na maradhi. Ila kitu kikubwa ni kuwasikiliza wataalam wetu, Mheshimiwa Rais ameshakabidhi Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Dada Ummy ambaye anafanya kazi nzuri sana pamoja na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile tuendelee kuwasikiliza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sijagongewa kengele ya mwisho kabisa kuhusu ushirika; pale Manyoni tumeletewa barua watu wamezuiwa kuuza mazao yao; zile Dengi, Ufuta na nini, eti mpaka wakauze kwenye Chama cha Ushirika. Hebu ushirika wajipange kwanza...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mungu akubariki.

SPIKA: Tunakushukuru sana Mheshimiwa Martha Mlata. Nilishakutaja Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na utafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu katika Bunge hili la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mwenyezekiti wa CHADEMA Taifa, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe, kwa kunitfea katika kipindi hiki kifupi kuwa Naibu Waziri Kivuli kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Namshukuru sana kwa kuniamini na namwahidi sitamwangusha na sitawaangusha wenzangu. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Hawa inaelekea safari hii wamepewa wanawake watupu. Inakuwaje hii?

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: *Yah!* Inaonesha kwamba ni kwa namna gani wanawake tunaweza kufanya kazi vizuri na kwa uaminifu mkubwa na tukipewa majukumu tunaweza kuyatekeleza kwa uaminifu. (*Makofii*)

SPIKA: Kwamba Mheshimiwa Mbewe ana imani sana na akina mama, ahsante sana. Endelea tu. (*Makofii/Kicheko*)

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naanza kuzungumzia kwa upande wa suala zima la afya na kipekee kabisa nizungumzie suala la *Corona*, suala linaloendelea katika nchi yetu kwa sasa. *Corona* imefika, ipo Tanzania, nami naomba sana pamoja na wenzangu wengi kulielezea vizuri sana suala hili la *Corona*. Napenda sana niwakumbushe akina mama wenzangu, akina baba kuona ni namna gani tunafuata maelekezo ya wataalam wetu wa afya. Tusidharau jambo hili kwani lipo, tutakuфа тутаача watoto wetu; watoto wetu watakuфа watatuacha wazazi, inaumiza sana. Tunaoa kwa wenzetu, kwa hiyo, tunaomba sana tujitahidi kufuata maelekezo ya wataalam wetu wa afya.

Mheshimiwa Spika, watu wengine wameshauri kwamba kuwe na angalau mambo mbadala ambayo yanaweza yakafanyika. Hata hivyo kuna mambo ambayo yanaendelea kwenye mitandao ya kijamii ambayo ni mbadala yanatisha. Yaani unakuta mtu anakwambia chemsha sijui miarobaini, weka tanganwizi, weka ndimu, ukichemsha mpaka unaona yale mapovu yanatoka, mtu anatia kwenye kikombe anakunywa. Jamani, tutauana.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Ndugulile unafahamu kabisa pele Muhimbili kuna chuo maalum cha tiba asilia tusaidieni ndugu zangu tutakuфа. Kuna mtu juzi alikuwa ana-*blend* kabisa zile Ndimu anachukua anaweka kwenye *Blender* ana-*blend* ameweka pamoja na Tangawizi mule ndani katia kwenye *glass* na akatoa tahadhari kwamba jamani hii dawa ni chungu kweli kweli lakini Mtu akisikia kwamba inasaidia anafanya anachoweza kukifanya. Tunaomba sana mtusaidie hili janga linatisha na kila mtu anaogopa tunahitaji kupona ndugu zangu na tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu tumuweke kwenye maombi kila mtu kwa dini yale ili janga hili liweze kutuepuka lisije likafika kama walivyofikiwa wenzetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna namba ambayo imetolewa katika kipeperushi cha Mheshimiwa Waziri wa Afya. Namba ile unaweza ukapiga leo ikapokelewa kesho, hii ni hatari sana. Hizi namba watu wanapopiga hii namba ambayo imetolewa

kwenye kile kipeperushi ni muhimu sana pengine wana taarifa sahihi kuhusiana na suala la watu ambao wako kwenye maeneo yetu tayari wana maambukizi, tayari wanaonesha dalili lakini hawataki kujitokeza. Kwa hiyo, tunaomba sana kama hii namba inakuwa haiwezekani kupokelewa ziwekwe hata tatu, nne, tano ili angalau kuwe na watu wanaoweza kupokea na kuweza kusaidia nduguzanguni lakini vinginevyo hii namba moja haipokelewi na malalamiko yamekuwa mengi. Kwa hiyo, ningeomba sana Wizara iangalie jambo hili, Serikali iangalie jambo hili, jambo hili ni muhimu, jambo hili ni nyeti, tutakwenda kupona kama tutaambizana ukweli. (Makof)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba ya Waziri Mkuu kuzungumzia masuala mazima ya afya lakini kuna changamoto nyingi sana katika sekta hii ya afya; kwanza bajeti inayotoka huwa ni ndogo pamoja na changamoto zilizopo lakini pili; tumekuwa tukiambiwa zaidi kwamba bajeti inaongezwa kwenye dawa, kwenye dawa, kwenye dawa lakini mgonjwa utampa vipi dawa kama hajapimwa na kugundulika ugonjwa wake? Kwa hiyo, nilidhani hasa kwenye hospitali zetu za rufaa tujitahidi sana Serikali kupeleka vifaa vyaa kupimia kwa sababu unakwenda wkenye hospitali, unafika kwenye hospitali ya rufaa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano; nikitolea mfano hospitali ya Kitete-Tabora, unafika pale kuna mgonjwa ana matatizo ya moyo unambiwa machine ya *ECO* imeharibika ukimuuliza tangu lini imeharibika? Ina mwaka haifanyikazi, mashine ya *ECG* imeharibika ukimuuliza imeharibika tangu muda gani mpaka leo kabla sijaja humu ndani ya Bunge nimempoigia simu Daktari na kumuuliza mashine imepona ama hajapona? Kaniambia imepona sasa kama imepona kweli ama alikuwa ananidanganya lakini ukweli ni kwamba mashine ilikuwa ni mbovu. Mtu anapewa rufaa kutoka Urambo, kutoka Kaliua, kutoka Ulyankulu aende Kitete, akifika Kitete nako hapati ile huduma anapewa tena rufaa ya kwenda hospitali ya Bugando sasa kuna maana gani ya hospitali kuiita ya rufaa kama haina hata vifaa vyaa upimaji? (Makof)

Mheshimiwa Spika, hayo hayo nimeyaona katika hospitali ya Mwananyamala. Nimefika pale nimekwenda kutibiwa nimekuta wazee wengi sana wamekaa pale wakienda kupima moyo. Roho ilinuma sana nimefika pale ilibidi niondoke kabla sijafanya chochote kwa sababu wangeona mimi natangulizwa kuanza kuingia mule ndani wangeumia sana nikajisikia vibaya. Imefika muda wangu kuingia nafika kuna mashine tatu zote zimeandikwa tarehe mpaka na mwaka mashine zile zilipoharibika. Mashine imeharibika tarehe 09.05.2016 ya *ECG machine*, ya *ECO* mpaka leo mashine ile hajatengenezwa. Kipo kimashine kidogo tu ambacho ndiyo kinatumika kwa msururu ule na ile ni hospitali ya Mkoa sasa kwa kweli hali ni mbaya. Tungeomba sana pamoja na bajeti mnazoziongeza kwenye dawa ongezeni basi na bajeti kwenye vifaa vyakupimia kwa sababu hizi hospitali zetu za rufaa watu ndiyo tunazozitegemea. Hali ni mbaya kuliko ambavyo tunaelezwa, kwa hiyo niseme tu pamoja na dawa lakini na vifaa hivi viongezwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la utoaji wa dawa pia limekuwa na changamoto sana. Hospitali ya Kitete ni hospitali ya rufaa lakini ni hospitali inayohudumia Wilaya mbili; inahudumia Wilaya ya Uyui, inahudumia na Wilaya ya Tabora Manispaa ambazo Wilaya hizi hazina hospitali za Wilaya. Bajeti ya hospitali ya Wilaya ya Tabora Mjini imetengwa lakini bado hajatoka hiyo milioni 500 mwezi huu ninavyozungumza. Angalau Uyui wameshapata na wameanza lakini hospitali ile ya Kitete inapokea wagonjwa wengi kutoka Tabora Manispaa pale pale na wengine wanatokea Uyui.

Mheshimiwa Spika, changamoto inapokuja bajeti ya dawa inayopelekwa hospitali ya Kitete ni ile ile ambayo inapelekwa kwenye hospitali zingine za rufaa bila kuangalia kwamba Kitete inapokea wagonjwa wengi ambao wanatoka kwenye Wilaya ya Tabora na kwenye Wilaya ya Uyui. Kwa hiyo, niombe sana bajeti ya dawa iongezwe katika hospitali yetu ile ya rufaa ili iweze kuendana na mahitaji ya watu wanaohitaji.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kuhusiana na suala zima la Msajili wa Vyama; Msajili wa Vyama majukumu yake yanaeleweca lakini yapo mambo ambayo yanatokea katika Nchi hii hatuoni akiyakemea. Kuna baadhi ya viongozi wa vyama vyta siasa wanatoa kauli ambazo hazipendezi kauli ambazo zinataka kututengenisha, kauli ambazo zinataka kuleta hali ya sintofahamu katika Nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kiongozi wa Chama cha siasa anapotoka na kujinasibu kwamba yeze anayo Dola, anaweza akatumia Dola ili aweze kupata Dola hii kauli kwa kweli siyo nzuri. Tumekaa muda mrefu hatujasikia majibu yoyote ama neno lolote likitoka kwa Msajili wa Vyama lakini na sisi tumkumbushe Msajili wa Vyama kwamba sisi tunao Wananchi na tunaamini kwamba wananchi hawa watakwenda kutusaidia na sisi tutakwenda kuingia kwenye Dola kama yeze anaamini katika Dola na sisi tunaamini katika wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuombe sana Msajili wa Vyama vyta Siasa atumie nafasi yake kuhakikisha kwamba anatulinda badala ya kutuvuruga. Kama mtu anatoa matamshi iwe ni kwenye Dola, iwe ni sisi huku wa watu wote kila mmoja anatakiwa afuate Sheria na taratibu za Nchi yetu. Kwa hiyo, ningeomba sana hizi kauli zinazotolewa na viongozi wa vyama vyta siasa hasa katika kipindi hiki cha uchaguzi zisiangaliwe tu kwenye vyama vingine hasa vyama vyta upinzani lakini viangaliwe hata kwenye Chama Tawala. Hawa viongozi wa Chama Tawala na matamshi yao yanakuaje na yanaathiri namna gani hapo baadaye baada ya uchaguzi mkuu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka nzungumze kidogo kwenye suala zima la Tume ya Uchaguzi; hizi kelele zinazoendelea za Tume huru, Tume huru, Tume huru nashukuru juzi ulisema kwamba utakaa na sisi pemberi ili tukuambie kwamba hii Tume huru ni nini, nini ambacho kinatakiwa.

SPIKA: Nataka mseme hapa hapa.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA Mheshimiwa Spika, muda hautoshi tuna mambo mengi lakini ni vizuri tukikaa tukakueleza nini hasa tunachokitaka katika kuhitaji hii Tume huru siyo kwamba tunasema lakini tuna mambo ambayo tunayaona kwamba hayaendi sawa katika Tume ya uchaguzi kwa hiyo tunataka yawekwe sawa ili mambo yaweze kwenda sawa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, leo tunakwenda kwenye uchaguzi, wanawake tunakwenda kugombea...

SPIKA: Ahsante sasna, kengele ya pili

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

SPIKA: Ahsante Hawa. Unasema unakwenda kugombea Majimbo yote yameja wagombea wa CCM utagombea wapi sasa? Ahsante sana. Mheshimiwa Goodluck nilishakutaja utafuatiwa na Mheshimiwa Anastazia Wambura. (*Kicheko*)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia nitoe mchango wangu mdogo.

Mheshimiwa Spika, nataka nianze walipomalizia wenzangu kwenye jambo hili la Tume huru ya uchaguzi; katika uhalisia kijana anayedai, anayeomba kuo katika familia ni kijana ambaYe ana base yaani ameshaonyesha ana mwanga, anajua maisha yake ataishi vipi aidha anafanya kazi au analima ana shamba. Sasa wapinzani kitendo cha kudai Tume huru ya uchaguzi wakati hakuna mlilowafanyia wananchi ni sawa sawa na kijana ambaye kula na kulala bure anayedai kuo.

Mheshimiwa Spika, wapinzani walipewa Wabunge zaidi ya 100, Madiwani zaidi ya 1500, hamna walichokifanya. Sasa hivi umefika wakati wa uchaguzi wanadai waongezewe

tena ili wafanye mabadiliko. Kama mlishindwa hivyo hata tukiwapa Nchi hamna kitu mtakachokifanya.

Mheshimiwa Spika, Chama Cha Mapinduzi tuko tayari kwa uchaguzi. Tumefanya mambo mengi sana. Nimpongeze Mheshimiwa Rais katika kila Nyanja. Niwape mfano, upande wa Vijiji; wananchi wetu wa Vijiji asilimia 90 ni wakulima na wengi wanalima kwa ajili ya chakula. Mwananzu Mwananchi akilima kidebe chake kimoja hawesi kukatisha mageti yalikuwa kibao lakini Rais wetu kwa kuliona hili akaondoa ushuru wote kwa hiyo wakulima sasa hvi ukilima ukiwa chini ya tani moja hulipii ushuru wa namna yoyote. Hizo ndiyo *base* zetu zinazotufanya twende kwenye uchaguzi kifua mbele.

Mheshimiwa Spika, kwenye mazao ya biashara kama Pamba, Tumbaku, Kahawa, Mkonge, Miwa kodi zilikuwa zaidi ya 140 lakini zimepunguzwa sasa hivi ziko chini ya 125. Hizi zote zinatufanya sisi twende kifua mbele kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, mtaani, bodaboda niwatolee mfano; wenzetu walikuwa wanawapa viroba bodaboda sisi tumewaondolea kero. Kwa mfano; trafiki walikuwa wanawasumbua sana. Bodaboda akikatiza anapigwa *fine* 60,000 au 100,000 au 120,000 lakini sasa hivi kipindi kile Waziri ni Kangi alipiga marufuku bodaboda *fine* ni moja tu na bodaboda zote ambazo zilikuwa kwenye vituo vy'a Polisi zimefagiliwa zote wamerudishiwa wenyewe sasa hawana watu wa kuwasaidia na hao ndiyo walikuwa watu wanaowasaidia katika kampeni.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Machinga; Machinga zamani walikuwa wanalipia ushuru kila kona wanayokatiza sasa hivi Machinga anapewa kitambulisho cha shilingi 20,000 marufuku kusumbuliwa anakwenda kufanya biashara popote, wao walikuwa wanawatumia katika maandamano.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa wasomi; elimu ya juu tunakumbuka tulikuwa tuna maandamano kila siku, kila Chuo utasikia leo mgomo, kesho mgomo. Zamani mikopo

ilikuwa inatolewa kwa matabaka sasa hivi mikopo hakuna kutoa kwa matabaka. Kwa hiyo, Wanafunzi wanapata mikopo kwa hiyo wamekosa watu wa kuwasaidia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, madarasa yanajengwa; juzi *World Bank* wametuidhnia mkopo wa Dola milioni 500. Wapo wapinzani ambao walikuwa wanakwenda wengine walikwenda hadi nje ya Nchi. kwenye hili nataka kujua, Tume ya Maadili ya viongozi wajibu wapo ni upi? Kiongozi anapotoka kwa ajili ya kwenda kuichafua Nchi huko nje, Tume ya Maadili isiishie tu kuangalia mikopo, madeni na mali zetu, iangalie na viongozi kama hawa. Niwaambie tu viongozi, wazee wetu ambao mnatulea tuko humu, watu kama hawa sijui mmewaleaje mimi hata sielewi.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa ardhi; tumeshuhudia zamanii hati ya nyumba, ya kiwanja walkuwa wanapata matajiri tu sasa hivi hadi masikini wa kawaida. Mimi kule Ulanga wamefanya *pilot study*yaani wamechukua eneo kama ndiyo *case study*, kila Mtu anayemiliki ardhi anapewa hati bure. Sasa hati ilitoka kutoka miaka 10 hadi wiki mbili. Wizara ya Ardhi pale Mtu anapimiwa kiwanja ndani ya wiki mbili ameshapata haki yake. Zote hizo tunakwenda kifua mbele kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara na nishati kwenye *REA*; Vlijiji vyote sasa hivi vinapata umeme hizo zote ni nyenzo zetu kwenye uchaguzi ndiyo tunakwenda navyo.

Mheshimiwa Spika, unyenyekevu wa viongozi wetu wa juu; Chama Cha Mapinduzi viongozi wa juu wananyenyekoa viongozi wa chini lakini wenzetu viongozi wa juu wanawalangua viongozi wa chini, wanawachangisha michango. Hizo zote ni nyenzo zetu za kwenda kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Rais wetu, kiongozi ,mwenye maono. Kwanini nasema hivyo? Rais wetu alipoingia madarakani alipiga marufuku safari za nje. Hebu *imagine* na *corona* hii maana yake kipindi kile Wabunge badaa ya vikao

vya Bunge wote walikuwa wanakwenda nje. Vikao vinapotaka kuanza ndiyo wanarudi sasa Wabunge wangerudi na *corona* hii tungekuwa wageni wa nani? Kwa hiyo, Rais wetu alikuwa na maono. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa vituo vya afya na hospitali za Wilaya; vituo vya afya zaidi ya 400, hospitali za Wilaya zaidi ya 67, hospitali za rufaa. Hivi na *corona* hii tungekuwa wageni wa nani tusingekuwa na vituo vya afya hivyo na hospitali za Wilaya?

Mheshimiwa Spika, nataka nijikite kidogo kwenye janga la *corona*; kwanza naomba Wabunge tuambiane ukweli, tofauti ya *corona* na *HIV* maana yake wengi wanailazimisha Serikali ianze kupima watu, hiyo siyo suluhu. Tungekuwa na mahali tukishawapima hawa watu tunawapeleka hiyo ingekuwa sawa lakini eti unampima mtu halafu unamuachia aende akarudi nyumbani. Janga la *corona* uamuza uko mikonini mwa kila Mwananchi, kila Mwananchi usafi wako ndiyo utakaokupelekea wewe kutokuwa na *corona* au la!

Mheshimiwa Spika, cha msingi hapa naomba katika Majiji, Wilaya, Halmashauri zetu tutunge Sheria ndogo ndogo za dharura. Kwa mfano; kwenye vyombo vya usafiri kama bajaji na daladala na usafi katika mitaa yetu hiyo itatusaidia. Niipongeze Serikali, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutokurupuka katika janga hili maana yake kuna Nchi kwa mfano; Nchi za wenzetu jirani wamekimbilia kuna Nchi moja hapo walifunga mipaka wiki tatu zilizopita walizua Ndege lakini wagonjwa kila siku wanazidi. Sisi hatujafunga mipaka mpaka leo tuna wagonjwa 20. Kwa hiyo, naomba niendelee kuwaasa wananchi wote, kuwapongeza madereva bajaji, madareva bodaboda na wananchi wengine kwa kuendelea kuzingatia haya.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba niongelee suala pensheni; Mheshimiwa Jenista Wazee wa Ulanga watakulaani. Nimetoka Ulanga Wazee zaidi ya 57 wastaaifu, walimu waliostaifu tangu mwaka juzi hawajapata kiinua

mgongo, hawapati pensheni yao ya mwezi. Hebu *imagine* mtu amefanya kazi miaka 30 alizoea kila mwisho wa mwezi anapata mshahara leo hii ana mwaka wa pili hajapata pensheni yake, hapati pensheni ya mwezi. Nimeenda Ofisi ya Kanda Morogoro hawana majibu wanasema iko Dodoma. Jamani huo uhakiki gani mtakuja kuwaua wazee wa watu. Wametaka kuja Dodoma kwenye Bunge hili nimewaambia hapana wageni hawaruhusiwi wamesema bora wafe na *corona* kuliko kufa na njaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba nikupongeze wewe na huu mfumo wa *E-parliament* kwa kuwa na maono. Hivi leo hii na mavitabu yale tungepona na hii *corona*? Leo nimeona kuna kigazeti kimoja kimeandika "mnyukano mpya wa Lissu na Ndugai". Wewe uko imara ndani umewagonga na kanuni wametoka nje na nje wakikuchokoza najua watakutana na bakora.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Goodluck Mlinga. Sijaona bado hiyo ya mnyukano mpya lakini mbona niko vizuri yaani asiyenijua mpaka sasa hivi. Sisi huwa tumejipanga na tunakwenda kwa *facts* wala hatumuonei mtu. Hii habari ya watu wanadai posho hadharani vitu kama hivyo ni vitu vidogo vidogo sana. Kama mtu kweli ana kaposho kake anadai ni kusema tu. Tuko hapa tuchukue posho ya mtu itusaidie nini? Halafu mtu si uko Ulaya huko tunasikia Ulaya ndiyo kuzuri zi ule vya huko basi. Yaani vitu vingine *we are more than ready for that*, tunasubiria kwa makini na tutajibu hija kwa hoja. Mheshimiwa Anastazia Wambura atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kakunda.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja ya wachangiaji kwa siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa neema na rehema zake ambazo

amekuwa akitujaalia kwa kila iitwapo leo lakini zaidi sana, napenda sana kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Rais wa Zanzibar pamoja na timu yote ya Mawaziri kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakitekeleza vizuri na kwa uzalendo mkubwa na kwa umahiri llani yetu ya Chama Cha Mapinduzi, hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi kwasababu wao wamekuwa wakisimamia kwa ukaribu sana utekelezaji huu wa llani ya Chama Cha Mapinduzi na kwa namna ya pekee nimshukuru sana Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, Dkt.Bashiru Ally kwa namna ambavyo amekuwa akituongoza vizuri katika chama chetu lakini pia kwa jinsi ambavyo amekuja Mkoani Mtwara mwezi uliopita na amesimamia vizuri, amekagua miradi ambayo imekuwa ikitekelezwa. Kwa hiyo, nampongeza na namuomba aendelee na moyo huo.

Mheshimiwa Spika, nichukue pia nafasi hii kukushukuru na kukupongeza sana kwa kazi nzuri ambayo unaifanya na niseme hili suala la *E-parliament* limekuja kwa wakati muafaka kwa sababu nilikuwa najiuliza hapa kwamba ingekuwa ni wakati ule wa kuhangaika na makabrasha sijui kama kuna mtu ambaye angeweza kusoma makabrasha yale kwa sababu kila mmoja angekuwa anogopa kupekuwapekua. Kwa hiyo, nimuombe Mwenyezi Mungu akubariki sana wewe na Naibu Spika, Katibu wa Bunge pamoja na timu yako kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkitujali na kuwa na maono ya kutusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mtwara; Wananchi wa Mkoa wa Mtwara wamenitura nilete shukurani zao za dhati kwa jinsi ambavyo Serikali yetu ya Awamu ya Tano imekuwa ikiwasaidia na ikiweka jitihada katika kuwainua kimaendeleo na kwa kuanzia tu niseme; katika maendeleo ya miradi ya maji tunakwenda vizuri. Manispaa ya Mtwara sasa hivi imefikia hatua ya kupunguza kwa kiasi kikubwa sana mgao wa maji

na sasa iko katika hatua za kutengeneza chujio la maji kule Mtawanya.

Mheshimiwa Spika, pia kuna mradi wa Mkwiti ambao una *lots* tatu; *lots* mbili ziko katika hatua za utekelezaji lakini kuna *lot* moja ambayo imebaki na naiomba Serikali sasa iongeze kasi ili kusudi wananchi wa Tandahimba na Newala waweze kupata maji kwa sababu mradi huu wa maji ya Mkwiti utatumika pale *lot* ya tatu itakapokuwa imekamilika.

Mheshimiwa Spika, nishukuru pia kwa upanuzi wa uwanja wa ndege ambao unaendelea kule Mtwara, lakini pia upanuzi wa bandari ujenzi wa hospitali ya rufaa ya kanda na ujenzi wa hospitali za wilaya pamoja na vituo vya afya ambavyo vinaendelea na vitatusaidia sana kuhakikisha kwamba afy ya wananchi wa Mtwara inaboreka.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna ya pekee, nishukuru sana sana kwa ujenzi wa barabara ya uchumi ambao unaendelea kwa sasa, lakini kwa upande huu niiombe Serikali pia iongeze kasi kwa sababu bado kidogo naona kilometra ambazo zimekuwa *covered* ni chache, lakini naamini kabisa katika bajeti hii tutakuwa tumepiga hatua kubwa.

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema wenzangu kuhusiana na ugonjwa wa *corona*, nami niungane na wenzangu wote kutoa mchango wangu katika eneo hili. Sidhani kama kuna mtu ambaye atakataa kwamba ugonjwa huu hauna dawa ugonjwa, hauna dawa na kilichobaki, ni kumwomba Mwenyezi Mungu. Hili tukimwachia Mwenyezi Mungu naamini kabisa atatusaidia kama alivyotusaidia kutuokoa kwenye kimbunga kilichotokea mwaka jana ambapo hakuna ambaye alitarajia kimbunga kile kisingeweza kutupata, lakini ni kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kimbunga kile kiliyeyuka bila kutarajia.

Kwa hiyo, naamini kabisa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu atatuepusha na janga hili, kwa hiyo, ni wajibu wa kila mmoja wetu kusali na kumwomba Mwenyezi Mungu

atuepushe na hili janga laini pia atusamehe popote pale ambapo tumemkosea kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango wangu kidogo, Waziri Mkuu ametuambia kuwa, kuna kamati tayari imeshaundwa ambayo inakutana. Sijui wajumbe wa Kamati hii pamoja na kwamba ametuambia ni Mawaziri na wataalam kutoka sekta mbalimbali, lakini napendekeza kwamba tungekuwa na wataalam wa lishe waliobobe a ambao wangeingia kwenye Kamati hii, lakini na wataalam wa *micro biology*, naamini kabisa tunao. Kwa hiyo, wataalam hawa kwa mfano kwa upande wa lishe, ukiangalia *clips* nygingi sana watu ambao wamekuwa wakishambuliwa na huu ugonjwa wanajitibu kutokana na vyakula.

Mheshimiwa Spika, lakini vyakula hivi vina kazi kubwa sana ya kuzuia nikiwa na maana kwamba kuna kuwa na zile *contents* ambazo zinakuwa na uwezo mkubwa wa kutoa kinga dhidi ya maradhi ya *virus*, kwa mfano wengi wamekuwa wakitaja kwamba wametumia machungwa, malimao, tangawizi na vyakula hivi kwa kifupi tuseme ni vile vyakula ambavyo vinakuwa na *zinc* na *vitamin C*. Sasa ukiangalia tabia ya *zinc* ina kazi kubwa sana ya kusaidia kinga ya mwili dhidi ya maradhi mbalimbali. Kwa hiyo niombe tu kwamba wale wataalam wa lishe watatusaidia sana sana kutushauri kwa mfano, katika matumizi ya tangawizi, vitunguu swaumu, mbegu za maboga maziwa korosho na watatuelekeza mazao mengi ambayo yanatoa hivi vitu ambavyo vinatusaidia katika kuongeza kinga ya mwili.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo suala la mafuriko. Suala hili ni matokeo ya mabadiliko ya tabia nchi na limekuwa likisumbua sana kwa muda mrefu, kwa hiyo, ni ushauri wangu sasa Wizara ya Ujenzi ikae na kuangalia ule mpango ambao nchi yetu uliweka katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi na Wizara ambayo inahusika na ujenzi ikae iangalie ni mambo gani ambayo imeyaruka ili kusudi iweze kuyajumuisha katika mpango wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Nimekauka koo, ahsante sana.

SPIKA: Watakuletea maji, watakuletea maji muda si mrefu.

MHE.ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, haya ahsante nasikia kukauka koo sijui ni kwa nini. (*Kicheko*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Anastazia Wambura.

MHE.ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Jamani tunaelekea kwenye uchaguzi mkuu, sasa makombora ni mengi, unajikuta unasimama kuomba kura, unabaki mimi naitwa, mi, mi, mi(*Kicheko*)

Hii hasa kule maeneo ya Usukumani na Unyamwezini kule shida kubwa ya haya makombora.

Nataka kuwakumbusha Waheshimiwa katika kujifukizia, mimi sijui kujifukizia kwa wengine inakuwaje, kwa Wagogo huweki jiko la mkaa au kuni halafu ukaweka chungu halafu ukajifukizia, hapana. Kwa sababu ukiweka hilo jiko la mkaa utaimeza ile *carbon dioxide* ambayo ni sumu, kile chungu kinachemka kimefunikwa halafu unakiweka hapa *almost* kama unakipakata, unakuwa karibu kabisa kwenye kiti kifupi cha miguu mitatu, halafu unaunaifunika shuka. Sasa kile chungu kile unakitoa mfuniko kwa hiyo unapata ule mvuke *pure* mvuke siyo jiko la mkaa, usije ukajifunika ukaishia kwenye jiko la mkaa, ikawa shida, mambo haya yanataka maelekezo mazuri. Unaweza ukawa peke yako kwenye chumba unafanya hivyo umekosa hewa halafu inatuletea shida nyininge watu watasema *corona, corona kumbe*.

Mheshimiwa Kakunda sasa ninyi Wanyamwezi ndiyo mnamtindo wa kujifukiza mkaa.

Mheshimiwa Kakunda tafadhalii, atafutiwa na Mheshimiwa Mchungaji Innocent Bilakwate. (*Kicheko*)

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa ushauri huo ambaao umeutoa wa kitaalam kweli kweli kwa ajili ya kuepuka *carbondioxide*, hongera sana kwa utaalam huo na nitakufuata nije nijifunze funze kidogo mambo ya miti shamba.

Mheshimiwa Spika, watu wa Sikunge wamenituma kuititia mikutano ambayo niliifanya kwa kila kijiji mwaka jana, nije nitoe shukrani za dhati kabisa na pongezi nydingi kwa Serikali inaongozwa na Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa miradi mingi ambayo tumeipata Sikunge na imesimamiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu bila kumsahau Makamu wa Rais, Mawaziri wote, Watendaji Wakuu wa Serikali, kwa ujumla wao tunawapa pongezi kubwa sana kwa weledi ambaao wameutumia katika kuiongoza nchi hii kwa viwango nya kihistoria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nichukue nafasi hii kukupongeza wewe binafsi na uongozi mzima wa Bunge kwa kuendesha Bunge kwa weledi wa hali ya juu, lakini kwa kutuletea Bunge Mtandao imekuwa ni historia kubwa sana kwa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, binafsi kama Mbunge wa Sikunge, niliomba miradi mingi kwa niaba ya wananchi wa Sikunge, Serikali ilikubali na utekelezaji umekuwa mkubwa na nikwambie kwa mara ya kwanza tangu dunia iumbwe, wananchi wa Sikunge wameanza kuona lami ambayo inatoka Tabora, inapita Sikunge inakwenda mpaka Mpanda, hilo ni jambo la kihistoria kwao na kwa mara ya kwanza watu wa Sikunge watapata Mahakama ya Wilaya, ambayo ilikuwa ni shida kubwa, wengine walikuwa wanasafiri kilomita 500 kwenye Mahakama ya Wilaya, Tabora Mjini.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa mara ya kwanza tangu dunia iumbwe, wananchi wa Sikunge watapata Hospitali ya Wilaya ya Serikali. Kwa mara ya kwanza pia kumekuwa na ukarabati mkubwa sana kwenye Chuo cha Maendeleo ya Wananchi kimekuwa kipyaa cha kisasa. Kwa mara ya kwanza nyingine tumepata vituo nya afya viwili vikubwa Kituo cha

Kipili na Kituo cha Nyahua; wananchi hao kutoka sehemu mbali kabisa kilomita 380 Kipili na kilomita 200 Nyahua wataanza kupata huduma vipimo na dawa huko huko waliko bada ya kwenda kusafiri kwenda Sikunge, Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, tangu dunia iumbwe, Jimbo langu la Sikunge na Wilaya ya Sikunge, tumepata shule mpya mbili za kidato cha tano na sita ambayo nayo ni historia. Niseme tu kwa mara ya kwanza shule zetu kongwe ambazo walisoma viongozi wetu wa juu kabisa wa nchi hii, akiwemo marehemu Mzee Sitta, zimekarabatiwa Shule ya Msingi Sikunge, Shule ya Msingi Chabutwa, imekarabatiwa sasa ni mpya kabisa. Kwa hiyo, kwa kweli mambo mengi yamefanyika Sikunge ambapo katika kipindi hiki cha miaka mitano imekuwa ni historia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maji kwa mara ya kwanza tumepata bwawa kubwa maana yake tulikuwa na Bwawa la Utiyati ambalo lilijengwa mwaka 1959. Kwa mara ya kwanza tumepata Bwawa lingine la Igumila ambalo ni kwa ajili ya matumizi ya wananchi. Ingawa huku mjini tutakuwa na maji kutoka Ziwa Victoria, ambayo sasa yamefika Tabora Mjini.

Mheshimiwa Spika, lazima nizidi kuipongeza Serikali kwamba yote haya yamefanyika chini ya usimamizi wa Chama cha Mapinduzi. Kamati ya Siasa ya Mkoaa ilipotembelea Sikunge hivi karibuni ilitoa shukrani zake za dhati kwa Serikali kwa utekelezaji mzuri sana wa llani ya Uchaguzi katika Jimbo la Sikunge na kwa kweli kama Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya nizipokee hizo pongezi na naomba nizifikishe Serikalini kupitia kikao hiki cha Bunge ambayo ilipitia hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, bado ziko changamoto chache ambazo ningependa kuzainisha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mafuriko, hii ni changamoto ni ya nchi nzima, lakini kwetu sisi katika jimbo imekuwa ni

changamoto maalum kwa sababu mafuriko yametutenganisha na mawasiliano ya mikoa miwili. Hatuna mawasiliano na Mkoa wa Katavi na hatuna mawasiliano na Mkoa wa Mbeya kwa sababu ya mafuriko. Kwa hiyo, naomba hii changamoto Mheshimiwa Waziri Mkuu aipe kipaumbele cha juu kabisa kwa upande wetu katika Jimbo la Sikunge na Mkoa wa Tabora ili angalau tupate suluhisho la kipaumbele cha haraka sana ili tuweze kurudi katika mawasiliano na wenzetu wa Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Mbeya. Maeneo mengine yote ambayo yameharibiwa na mvua pia ni vizuri yakapatiwa mpango wa dharura wa utengenezaji ili wananchi warudi katika shughuli zao za kiuchumi za kawaida.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyininge bado tunaendelea na ufinyu wa arди ya kilimo na ufugaji katika Jimbo la Sikunge. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili alipotembelea Sikunge mwaka jana alituahidi kwamba Serikali itafanya utaratibu wa kuboresha na kuzipandisha hadhi hifadhi zetu na misitu iliyoko katika Wilaya ya Sikunge ili kupunguza maeneo yale ya misitu ambayo hasa ambayo hayatumiki sana ili kuwaongezea wananchi maeneo ya kulima na maeneo ya ufugaji. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili kuitia kwako, walikumbuke suala hilo hili mbunga zetu, hifadhi zetu na misitu yetu iboreshwe ipandishwe hadhi ili lipatikane eneo kubwa zaidi kwa ajili ya kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni tumbaku, kwetu sisi Sikunge au Mkoa wa Tabora Wilaya kama tatu au nne na baadhi ya wilaya nyininge nchini hapa tumbaku ni uchumi. Sisi ni wategemezi wakubwa sana wa tumbaku ili kupata fedha, wakulima wetu katika kipindi cha miaka mitatu minne iliyopita wamekuwa na changamoto kubwa sana ya soko, sehemu ya kuuzia tumbaku naamini hiyo ni kengele ya kwamba.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana *TLTC* waliondoka hapa Tanzania, kwa hiyo mnunuzi mmoja amepungua, hata kama hajaondoka *TLTC* bado tulikuwa na soko finyu la kuuzia tumbaku. Sasa ameondoka *TLTC* tangu mwaka jana *British-*

American Tobacco wanaomba kuingia kwenye soko la Tanzania na tangu mwaka jana kumekuwa na majadiliano kati ya *BAT*, Wizara ya Kilimo, na Wizara ya Fedha kuhusiana na masuala ya kodi.

Naomba hiki kikosi kazi cha kodi kitilie maanani na wazingatie wakulima wa tumbaku ili kuhakikisha kwamba kama kuna vipengele vya kodi ambavyo vinahitaji marekebisho, basi vije kupitia *Finance Bill* ya mwaka huu mwezi sita ili mwezi wa Saba, *BAT* waingie kwenye soko la tumbaku ili kununua tumbaku.

Mheshimiwa Spika, hiyo itakuwa ni kazi kubwa sana na itakuwa ni mchango mkubwa sana kwa wakulima wetu kwa sababu *BAT* yeye kwanza kwa miaka miwili ya kwanza ataingia kununua tumbaku ambayo imekuwa inazalishwa kwa ziada na hii tumbaku ambayo imekuwa ikizalishwa kwa ziada, ndio tumbaku ambayo wakulima wamekuwa wananyonywa sana.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita kwa taarifa ambazo tunazo sisi kutoka Tabora, ni kwamba, wapo wakulima ambao walikuwa hawajauza, wameuza tumbaku kilo moja Sh.280 ambao ni unyonyaji wa hali ya juu sana kama anaingia *BAT* kununua tumbaku imezidi ziada ya mikataba maana yake ni kwamba atanunua kwa bei ambayo alinunua *Alliance One* ambayo alinunua mnunuzi mwingine itakuwa ni faraja kubwa sana kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali itilie maanani suala hili, vile vingezo ambao walikubaliana, najua Mheshimiwa Bashe ni mtu ambaye amelishughulikia sana suala hili na kwa kushirikikana na *BAT* na Wizara ya Fedha wamefanya vikao vingi sana tangu mwaka jana, lifikie hitimisho hili mapendekezo ambayo wamependekeza hapo awali yaweze kuingizwa kwenye sheria ili tuweze kupata mnunuzi mpya.

Mheshimiwa Spika, ya kwangu yalikuwa ni hayo kwa niaba ya watu wa Sikunge nashukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Joseph George Kakunda. Nilishakutaja Mchungaji Innocent Sebba Bilakwate, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Abdalah Juma.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru kwanza Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya na nguvu ya kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo wa Kyerwa. Nichukue nafasi hii kwanza kukupongeza wewe binafsi kwa miaka hii kwa kweli umeonesha uchapaji kazi mkubwa kwenye Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mimi kama unavyosema kama mchungaji naendelea kukuombea Mwenyezi Mungu akupe afya na nguvu ili urudi tena uendelee kuchapa kazi hii ambayo umeichapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake. Ni ukweli usiopingika Mheshimiwa Waziri Mkuu amechapa kazi kubwa na amekuwa msaada mkubwa kwa Mheshimiwa Rais kwa ziara nyingi ambazo amekuwa akizifanya hata kule kwetu Kagera, ziara ambazo amekuwa akizifanya wale ambao walikuwa wakionekana ni Mungu watu siku hizi wamekuwa wapole. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nichangie kwa upande wa sekta ya kilimo; kwenye hotuba ya Waziri Mkuu sekta ya kilimo ni muhimu sana na ndiyo sekta ambayo ina wazalishaji wakubwa. Niombe sana Serikali imefanya mambo makubwa sana, lakini katika sekta hii bado hatujaweka nguvu kubwa. Tunasema hii nchi ni Tanzania ya viwanda, lakini hivi viwanda lazima vipate malighafi kutoka kwa hao wakulima, tuisipowekeza nguvu kubwa tutaendelea kuleta malighafi kutoka nje na tutaendelea kunufahisha Mataifa mengine wakati hizi malighafi zingeweza kuzalishwa hapa kwetu. Kwa hiyo, niombe sana pamoja na jitihada za Serikali, lakini iongeze nguvu, kwa kweli bado kabisa hatujaona nguvu kubwa kama ambavyo tumewekeza kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kwa mfano suala la mazao haya ya kimkakati. Haya mazao ya kimkakati naamini tukiweka nguvu kubwa yatatusaidia sana kuongeza pato la Taifa na ndiyo mazao ambayo ni muhimu lakini pia yanaweza kutuingizia pesa ya kigeni kwa mfano, niseme kahawa, hili ni zao la muhimu sana. Pamoja na jitihada za Serikali za kulturudisha kwenye ushirika bado bado, mimi niseme kama mkulima ambaye natoka kwenye mkoa ambo tunalima kahawa bado hatujaona jitihada kubwa sana kubwa sana ambazo Serikali imeweka.

Mheshimiwa Spika, niombe sana tuendelee kuweka jitihada ili huyu mkulima ambaye anazalisha aendelee kuongeza uzalishaji. Mimi naamini tusipoweka nguvu kubwa katika mazao ya kimkakati wakulima hawa watakata tamaa. Maeneo mengine hata kule kwetu Kagera watu wameanza kukata tamaa sehemu zingine ile mibuni wanaikata wanaweka mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana Serikali iongeze nguvu lakini ni pamoja na kuwa na soko la uhakika. Hawa wakulima wanapolima mazao yao wapate soko la uhakika lakini pia wapate bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kahawa kumekuwa na sintofahamu. Majirani zetu Uganda inasemekana wana bei kubwa na hili limeleta changamoto kubwa kwenye Mkoa wa Kagera na hasa kwenye Jimbo langu. Alipokuja Mheshimiwa Naibu Waziri alipofika kule akasema wamefanya utafiti Uganda wamekuta wana bei kubwa. Sasa baada ya kusema wana bei kubwa nini kinafuata?

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri kama kweli wana bei kubwa kwa nini tusiwaruhusu hawa wananchi tukaweka utaratibu kahawa hii hawa Waganda wakaja wakanunua wakatupa bei nzuri kuliko kuja unawaambia wananchi halafu unaondoka. Hata hivyo, Naibu Waziri mwингine anasema tatizo la bei ya kahawa ni soko la dunia. Kwa hiyo, hii inawachanganya wananchi hata sisi amba ni wawakilishi

tunakosa majibu ya kuwaambia wananchi wetu. Kwa hiyo, kama Uganda kuna bei kubwa ambayo inaizidi ya Tanzania na changamoto kama sio soko la dunia niombe sana Mheshimiwa Waziri basi hawa Waganda wawekewe utaratibu waje wanunue kahawa yetu ili wakulime wapate bei nzuri na wasiendelee kulalamika na mwisho wa siku wakakata tamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi kama mwakilishi furaha yangu ni kuona wananchi wangu wanapata bei nzuri ya kahawa na wanajengewa ambayo mazuri kuweza kuuza kahawa yao. Hailjalihi ni nani atakayenunua hata kama anatoka Uganda au Ulaya, cha muhimu Serikali iweke utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuliongelea ni usala la miundombinu. *TARURA* wana barabara nyingi ukilinganisha na *TANROADS* na ndio wako vijijini ambako ndiko kuna uzalishaji mkubwa. Hawa *TARURA* tunaendelea kuwapa asilimia 30 wahudumie mtandao mkubwa amba hata *TANROADS* hawafikii nusu, hili kwa kweli halijakaa sawa. Niombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie jambo hili na ikiwezekana msiwaachie hawa Mawaziri kwa sababu kila mmoja anavutia upande wake. Mheshimiwa Waziri Mkuu aingilie kati hili jambo *TARURA* wapewe pesa ya kutosha ili waweze kuhudumia barabara zetu. Vinginevyo wananchi hawa wanapozalisha hawatakuwa na miundombinu rafiki ya kusafirisha mazao yao kufika kwenye masoko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mikoa mingine ambayo kwa kweli tumejaliwa, ukiondoa hii mvua iliyokuja kipindi hiki lakini sisi kwetu Kagera, kwa mfano kwangu Kyerwa miezi karibu kumi yote sisi tuna mvua, sasa huku barabara zinaharibika sana. Niombe sana Serikali maeneo haya ambayo yana mvua kipindi kirefu yaongezewe pesa ili barabara ziweze kutengenezwa. Kwa kweli nipongeze kwani Serikali imejitahidi *TARURA* wanafanya kazi nzuri wakiongezewa pesa naamini watafanya kazi nzuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la *Corona*. Mimi niipongeze kwa kweli Serikali imejitahidi sana na huyu mama yetu Mheshimiwa Ummy Mwalimu pamoja na msaidizi wake wanafanya kazi nzuri na tumeona Waziri Mkuu kazi anayoifanya. Hawa wanaobeza siku zote wanasema mpiga debe huwa si msafiri acha wanaosafiri waendelee kuchapa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali lakini wengine walikuwa wanashauri sijui kuna kujifukiza na kadhalika, lakini mimi nije mbele yako na niombe hili neno kama litapata kibali chako lifanyike kwa sababu una mamlaka ya kuamua jambo lolote ukiwa kwenye Kiti chako. Ukitosha kwenye Maandiko Matakatifu magonjwa yote yaliporuhusiwa na Mungu ilikuwa ni dhambi. Dhambi ndiyo imesababisha magonjwa haya yaje yatupate kwa sababu Mungu hawezি kuruhusu watu wake waguswe na adui kama hawajatenda dhambi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi pamoja na juhudii hizi zinazofanyika niombe sana, sisi hapa Bungeni ni wawakilishi wa wananchi wa Watanzania wote, Kiti chako kama kitaridhia tutoe dakika hata tano tusimame mbele ya Bunge hili tukatubu kwa ajili ya Taifa la Tanzania. Mheshimiwa Rais alishaonesha mfano mzuri na akatoa Maandiko sasa niombe sana na wewe utupe kibali kutoka kwenye Kiti chako tusimame tutubu kwa ajili ya dhambi ya Tanzania. Ninaamini Mungu ataturehemu na ataliponya Taifa letu tutakuwa salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la *NIDA* ambalo kwa kweli halijakaa vizuri na limeleta vurugu. Wewe unawaambia wananchi simu zitafungwa wakati *NIDA* hawajatoa vitambulisho, hivi huyu mwananchi unayemfungia simu zake hujampa kitambulisho, hujampa huduma kosa lake ni lipi?

Mheshimiwa Spika, niombe hili jambo Serikali iliangalie na ikiwezekana wakae wajipange, halijakaa sawa. Kule kwetu limeleta mpaka rushwa, imekuwa ni biashara,

anayekuwa na pesa nyingi ndiye anaweza kupata kitambulisho, haliko vizuri kwa ujumla. Niombe sana Serikali ijpange jambo hili iliangularie na ikiwezekana wafuatilie maeneo mengine waone linaendaje.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana kwa ushauri wa Kichungaji Mheshimiwa Innocent Bilakwate. Hakika bila kutubu tutaangamia. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Asha Abdallah Juma atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naanza kwa kumshukuru Mungu aliyenipa uwezo na nguvu ya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa na kwa sauti kubwa, naomba nichukue nafasi hii ya kwanza kabisa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa jinsi anavyosimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa kusimamia maendeleo ya wananchi na uchumi wa nchi yetu Tanzania. Vilevile niwapongeze wasaidizi wake wakuu, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa jinsi walivyosimama na kuwajibika katika kusimamia maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninayo mambo mawili makubwa ya kuanza nayo. Jambo la kwanza ni hili lilitotokea hivi karibuni lilitoikumba nchi yetu nalo ni mafuriko. Mvua zimekuwa nyingi na zimeleta uharibifu kwenye makazi, mashamba, watu wanahangaika, mifugo inapotea na mazao yanaharibika.

Naamini Serikali inachukua hatua za kutosha katika kuwasaidia hawa waliopatwa na madhara haya. Nawapa pole kwa sababu hili jambo ni kubwa lisipochukuliwa vizuri watu wetu wengi wanaweza wakapata shida baadaye. Kwa hivyo, nina imani Serikali inafanya kazi yake kama inavyostahili kuli-*address* jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ni kubwa na ni tishio kwa dunia nzima ni hili la *Covid19*, hii *Corona* ambayo kwa kweli imeangamiza maisha ya watu wengi hapa duniani na inatia wasiwasi na taharuki sana. Niombe tuendelee kusikiliza na kutekeleza yale ambayo tunashauriwa na Serikali katika kudhibiti maradhi haya yasienee. Naamini kwamba Serikali yetu pamoja na wale ambaao walipewa dhamana ya kushughulia jambo hili akiwemo Waziri, Mheshimiwa Ummy, Naibu Waziri wake na wote wale ambaao wanashughulika kwamba wanafanya kazi nzuri na watajipanga vyema katika kuhakikisha vifaa vyote vinavyohusika vinapatikana pamoja na hizo *ventilators* ambazo tumekuwa tukiona katika taarifa za habari huku duniani hata Marekani hazipatikani kwa hiyo watu wenye tatizo la kupumua inakuwa shida. Hii ikienda sambamba na kuwaandaa madaktari na wahudumu wote watakaowasaidia watu wanapopatwa na matatizo haya ya pumzi. Tunamwomba Mungu atusaidie balaa hili litokomee mbali kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nataka kuchukua nafasi hii ya kipekee pia kumpongeza Rais wa Zanzibar, Dkt. Ally Mohamed Shein ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa utekelezaji wake wa Ilani kusimamia mapinduzi na kuyalinda na kuulinda Muungano ambaao umepelekea nchi yetu kuwa na amani na utulivu na sisi wengine tuko hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, nije kwenye Wizara hii ya Waziri Mkuu. Natoa pongezi kwa Mawaziri Mheshimiwa Jenista, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Antony Mavunde na Mheshimiwa Stella Ikupa. Hawa wote wamefanya kazi nzuri sana kusimamia utekelezaji

wa majukumu katika Wizara hii. Hongereni sana ndugu zangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiendelea na mchango wangu, nije kwako wewe *special*. Wewe unatisha, umesimamia mabadiliko makubwa katika Bunge letu hili (Bunge mtandao). Pongezi nyingi sana kwako, leo Wabunge tunafanya kazi zetu kwa njia ya kisasa zaidi, kwa wepesi zaidi kwani taarifa zote ziko katika *finger tips*, huu ni ukombozi mkubwa. Vilevile hii itaokoa pesa nyingi ambazo zilikuwa zinatumika kuzalisha makaratasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pongezi pia kwa Naibu Spika, Wenyevit, Katibu wa Bunge na watendaji wote wa Bunge kwa jinsi tulivyoweza kushirikiana katika kufanya kazi mpaka Bunge letu hili ambalo ni la mwisho.

Mheshimiwa Spika, vilevile siwezi kusahau watu wetu ambao wametufanya tukakaa hapa Bungeni vizuri, hawa ni wahudumu wa sekta ya afya. Nayo hii ni timu kubwa ikiongozwa na mwenyewe Dkt. Temba na madaktari wenzake Dkt. Nuhu na Dkt. Ruge; Wauguzi, Sister Disifa, Sister Farida; Mfamasia Salma; Madereva wa *Ambulance*; Wahudumu wa Hospitali na *Technician* wa *Lab*. Hawa wote wametufanya sisi tumekuwa imara kuliko tulivyokuja. Mimi hapa mnavyoniona niko imara kuliko Halima Mdee na ninyi mnaniona leo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na utekelezaji...

SPIKA: Mheshimiwa Asha na bahati nzuri hajabisha kabisa, kwa hiyo, endelea kuchangia. (*Kicheko*)

MHE. ASHA ABDALLUH JUMA: Mheshimiwa Spika, naomba sasa niongelee miundombini, hii *Standard Gauge* inanipa raha sana na kwa kweli ni ukombozi mkubwa kwa sekta ya usafiri. Hii ni reli ambayo inatoka Dar es Salaam kupitia Morogoro hadi Mwanza na Kigoma. Reli hii itakuwa msaada mkubwa kwa usafirishaji wa bidhaa, abiria, mazao

na kuunganisha miji na vilevile kusaidia katika uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, mbali na hayo lakini reli hii inaweza kuja kuzalisha ajira nyingi sana zipatazo 13,177. Ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wetu. Naamini itakamilika kwa muda na ni jambo ambalo nchi yetu hii tutajivunia.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri Mkuu anazungumzia suala la bajeti yake lakini kuna wananchi na wao wanafikiria bajeti zao. Kuna kadhia moja kubwa imewakumba baadhi ya wananchi wale ambao walikuwa wateja na wafanyakazi wa *FBME Bank*. Watu hawa suala lao lilikuwa likiletwa hapa Bungeni mara kadhaa lakini limekuwa likipata majibu mepesi, mepesi. Watu hawa fedha yao iko kule hawapati msaada wowote, wengine wanakufa, familia zao bado zinateseka na jambo hili hallishi.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu wafanye utaratibu wa kuandaa Kamati, kama ile iliyokwenda kuzungumzia kuhusu madini yetu ikapata suluhu. Namna gani Kamati hiyo itakuwa wanajua wao. Kama wataweka Maprofesa wao waliobobea katika sheria pamoja na wadau lakini watu hawa ni kweli wana dhiki kubwa kwa sababu pesa zao nyingi zilikuwepo kule. Najua Serikali yetu ni sikivu na iko hapa kuwatetea wanyonge ambao pesa yao ya maisha iko kule na sasa hivi kazi imekuwa ngumu, kila kitu kimekuwa kigumu. Waziri Mkuu naomba alione jambo hili liweze kufikia mwisho wake kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kuchangia katika miradi ya Mahakama. Utekelezaji wa miradi hii umekuwa mzuri sana (*first class*), majengo ya Mahakama yamekuwa mazuri mno, kila mtu anayekwenda kule hawezি kusema katoka kule kaonewa. Majengo ya Mahakama Kuu Kigoma, Chato yamejengwa vizuri sana na Mahakama za Wilaya zote zimekarabatiwa na nyingine zimejengwa upya ziko kwenye hali nzuri sana pamoja na kupata *furniture* nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, ila kuna baadhi ya majengo haya ya Mahakama hayana uzio (*fence*) kitu ambacho ni hatari. Hii ni kwa sababu imeshawahi kutokea *incident* Mahakama ya Wilaya ya Uyole ilipigwa mabomu. Kwa hiyo, nashauri Serikali ijitahidi iweze kujenga uzio kwenye Mahakama hizi.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika pia katika watendaji ambao wamesimamia kazi hizi ni huyu Injinia Katunzi. Injinia huyu kwa miradi ya Mahakama amefanya kazi nzuri sana.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Asha, naona muda hauko upande wako.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Spika, naam.

SPIKA: Muda wako umeisha.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Spika, hapana, ndiyo kwanza kengele ya kwanza.

SPIKA: Leo sijui Katibu ana matatizo gani Mheshimiwa Asha.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Spika, basi naunga mkono hoja lakini uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ni huru. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Asha Abdullah Juma. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma nilishakutaja na baada ya hapo tuhamie *CUF*, tutamsikiliza Mheshimiwa Sulemani Bungara.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kutoa pungezi. Kwa kweli ni furaha sana kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu mambo mengi mazuri sana yamefanyika. Nampa pungezi Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mwenyezi Mungu azidi kumbariki.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpa pungezi pia Mheshimiwa Rais kwa kufanya mambo mengi mazuri. Tunampongeza sana na tunamwombea mbele ya Mwenyezi Mungu, tunaamini kuwa utapita bila kupingwa, hakuna Mpinzani mbele yako. Nikirudi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya mambo mazuri sana kumsaidia Mheshimiwa Rais na wewe Ruangwa watakupa kura za kutosha utapita bila kupingwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Jenista kwa kumsaidia mambo mengi Mheshimiwa Waziri Mkuu. Vilevile niwapongeze Mheshimiwa Kairuki kwa mambo yote anayosaidia; Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Stella Ikupa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe umefanya mambo mazuri sana. Tunajidai kwenye Bunge hili kwa kuwa na Bunge mtandao. Mwenyezi Mungu akubariki na umeacha alama, kila mmoja atakuwa anajua kuwa wewe ndiyo ulianzisha Bunge mtandao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia tunakushukuru sana na tunakupongeza sana pamoja na Naibu wako pamoja na Wenyeviti wote kwa kutuongoza kwa muda wa miaka mitano kwenye Bunge hili. Tunawashukuru na Mwenyezi Mungu awabariki nyote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafanikio ni mengi ambayo yote yameandikwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kila mmoja anayaona kama anajidai haoni sijui yeye yuko wapi. Reli tumeionna, elimu tumeionna, hospitali tunaziona, maji tunaona, kila kitu tunaona. Kwa kweli Serikali yetu ya Awamu ya Tano tunaipongeza, Tanzania tunajivunia na tunafurahi kuishi kwenye nchi yetu, inapendeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nianze kuongelea kuhusu miundombinu. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kweli wamejitahidi pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu, mmefanya mambo mazuri sana. Nianze na barabara. Barabara za lami zimejengwa, tumeunganishwa. Naweba nikatoka hapa nikaenda Ruvuma siku hiyo hiyo; nikaenda Mtwara siku hiyo hiyo nikafika; nikaenda Lindi siku hiyo hiyo nikafika; nikaenda Kagera nikafika siku hiyo hiyo; nikaenda Mara siku hiyo hiyo nikafika. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa mambo hayo ambayo mmeyafanya kwa kuunganisha barabara za lami. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia nashukuru kwa upande wa barabara za vijiji, zilikuwa zimejengwa kweli siyo uongo, lakini mambo ya tabianchi hatuwezi kuyabadilisha. Ni kweli tumepata mafuriko, yametokea na tumeyaona, Ila nawashukuru sana, tena sana kwa sababu ingawa yametokea kwa mfano kwenye Daraja letu la Kiegea ambalo linaunganisha barabara na usafiri wa kwenda mpaka nchi za nje, Mheshimiwa Rais alifika, Mheshimiwa Waziri Mkuu amefika, Mheshimiwa Waziri, *Eng.* Kamwelwe amefika na Waheshimiwa wamefika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kuwa licha ya kuondolewa hayo madaraja, lakini Serikali inachukua tahadhari haraka sana na kurudisha usafiri na sasa hivi magari yanapita kwenye Daraja letu la Kiegeya ambalo liko kwenye Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Kilosa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande huo huo, naomba tena sana, kwa sababu barabara za vijiji kutokana na mabadiliko ya tabianchi na mafuriko yaliyotokea barabara nyingi za vijiji zimeharibika. Kwa sababu barabara nyingi za vijiji ziko chini ya TARURA, nami naungana na watu wanaosema kuwa TARURA waongezewe fedha za bajeti kwa sababu ya kutengeneza hizo barabara. Madaraja mengi ya vijiji yameharibika, siyo Morogoro tu, ni mikoa mingi imepata dharura hiyo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu iwe dharura, iweze kuchukuliwa ili hayo madaraja yaweze

kutengenezwa na tuweze kupata usafiri hasa kwa mazao pamoja na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, kwa kweli tunashukuru sana kwa ujenzi wa Vituo vya Afya, ujenzi wa Zahanati, ujenzi wa mahospitali na hata Mkao wangu wa Morogoro yamejengwa, tunakushukuru sana. Naomba kutoa ushauri kuwa mpaka sasa hivi unakuta Vituo vya Afya vingine na zahanati nyingine kuwa wataalam hawatoshi. Kwa hiyo, naomba huo mgawanyo wa wataalam; manesi, madaktari bingwa, wataalam wa maabara, uweze kuangaliwa ili tuweze kupata mgawanyo vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunajivunia hata hospitali zetu za kanda, sasa hivi kwa kweli zinafanya vizuri. Ukiiona Benjamin Mkapa inafanya kazi vizuri, Muhimbili inafanya kazi vizuri hata za Kitaifa. Kwa hiyo, sasa hivi tumeponguzza hata wagonjwa kwenda nchi za nje na hasa ukiangalia na ugonjwa huu wa *Corona*. Kwa hiyo, tunamshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *Corona* nami naomba kuongelea *Corona*; kwa kweli ni ugonjwa ambao unaumiza sana. Nilikuwa naangalia kwenye mtandao, unaona unawashika hata watoto wadogo, wanatenganishwa na wazazi wao. Kwa hiyo, ninachokiomba kwa Ugonjwa kwa ugonjwa wa *Corona*, tuuangalie kwa makini. Pia nawashauri wazazi waweze kuchukua ushauri ambao tunapewa pamoja na Mawaziri wetu, Rais wetu na Waziri Mkuu ili tuweze kuwalinda hata watoto wetu ambapo wewe mzazi unaweza ukapona lakini mtoto wako akachukuliwa akawekwa kwenye karantini. Kwa hiyo, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea kuhusu elimu. Natoa pongezi kwa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa mambo mengi inayoyafanya kuhusu elimu na hasa kwa mkopo huu ambao umeidhinishwa wa *World Bank* wa Dola za Kimarekani milioni 500 ambazo zitasaidia watoto wetu wa sekondari pamoja na kupunguza mimba za utotoni kwa

sababu hata mahosteli yataweza kujengwa. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali pia kwa kurudisha usafiri wa treni kwa upande wa Dar es Salaam kwenda Moshi na Tanga kwenda Moshi, pamoja na uendelezaji wa ujenzi na ukarabati wa Reli ya Kati pamoja na ujenzi wa Reli ya *SGR*.

Mheshimiwa Spika, ombi langu na ushauri wangu kwako na Mawaziri wote, naomba sana hizi reli zitakapokamilika, tupunguze malori yanayopita kwenye barabara zetu ili mizigo inayobebwa kwenye malori haya iweze kubebwa kwenye treni hizi, kwa sababu haya malori yanaharibu barabara zetu. Hebu angalia Wabunge wote tunasafiri kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam, lakini unakuta mahali pengine barabara zetu siyo rafiki kwa sababu ya haya malori ya mizigo. Pia yanaleta msongamano na yanasaababisha ajali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ulinzi na usalama. Nchi yetu imebarikiwa kuwa salama chini ya Jemedari wetu, Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Tunashukuru sana vyombo vya ulinzi na usalama, vinafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba sana wananchi wote wanisikilize kwamba tuzidi kutunza amani na usalama kwenye nchi yetu kusudi tuweze kuendelea vizuri kwani amani hainunuliwi, inatunzwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mambo ya Mfuko wa Taifa wa Vijana, natoa pongezi kwa sababu wamefikiwa vijana wengi, vikundi 586, vijana ambao wamefikiwa tayari ni 4,222, lakini ninaomba licha ya kutoa pongezi, elimu izidi kutolewa kwa vijana wote, waweze kupata elimu jinsi ya kupata huu mkopo na hasa kwenye Halmashauri nyingine ambazo bado hazijafikiwa kwa sababu ni Halmashauri 155 ambapo mpaka sasa hivi wametoa hivi vikundi na wameweza kuwapata hao vijana. Hii mikopo iweze kuwasaidia hata vijana ambao wako kwenye kada zozote zile kuanzia wahitimu wa Vyuo Vikuu

mpaka wale wa Darasa la Saba, wote waweze kupata na waweze kujiajiri kwa sababu ajira kama tunavyojuu haipo. Ajira ni ya kujiajiri na ajira ni wewe mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naomba kuongelea ni kuhusu nishati. Namshukuru sana Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kalemani pamoja na Mheshimiwa Subira kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Ni nzuri sana. Wamefanya kazi nzuri, tumeona umeme. Watu wengine tulikuwa tumezaliwa na kukulia kwenye vibatari, lakini sasa hivi tunaona umeme. Kwa hiyo, jambo ninaloomba ni moja tu; kama mpango ulivyopangwa kuwa vile vijiji pamoja na Vitongoji vilivyorukwa kwa mpango huu wa *REA III* viweze kufikika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano pale Morogoro kuna Kitongoji cha Chekereni, hakina umeme, lakini naona kuna kiwanda cha mikunde kinawasha umeme pamoja na pale Mtego wa Simba umeme upo, lakini chenyewe kiko katikati hakina umeme. Kwa hiyo, naomba na chenyewe pamoja na vijiji vingine ambavyo vimekosa umeme vipatiwe umeme.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ni kuhusu pensheni. Kwa kweli kuna wale wafanyakazi wengine ambao hawakufanya kazi kwenye mfumo wa Serikali, wanalia huko, hawajapata pensheni. Walikuwa wanaomba kama inawezekana, watu wote waweze kupata pensheni waweze kupata hela kidogo kama *TASAF* inavyofanya angalau kuangalia wale ambao hawana uwezo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kweli Tanzania yetu inapendeza, tusonge mbele chini ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu tunawapa pongezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma na hasa kwa kutumia muda wako vizuri sana.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

SPIKA: Kuhusu Utaratibu.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba niweke wazi, nimesema Tume Huru ya Uchaguzi, yaani hivyo ilivyo inafaa na itafanya uchaguzi karibuni, japo kwamba haina neno huru katika jina lake. Ndivyo nilivyokusudia, maana nimemwona Mheshimiwa Esther kafurahi kweli kweli! Asije akafikiri ninadai Tume Huru. Hivyo ilivyo nimeikubali. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Tulikuelewa sana kwamba ndivyo ulivyomaanisha. Mheshimiwa Selemani Bungara.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameleta mafuriko ameleta Ugonjwa wa *Corona*; Mwenyezi Mungu ambaye amewapenda Watanzania kwa kuuchelewesha Ugonjwa wa *Corona* kuja Tanzania kwanza na ugonjwa huo kuanzia China. Huu ni mpango maalum wa Mwenyezi Mungu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naona mlimshangaa Mheshimiwa Bungara, hajakosea, imeandikwa tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kila jambo. Endelea Mheshimiwa.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, hivi walikuwa na matatizo hapo? *Kheri shari minallah i taalah.* Kwa hiyo, tunamshukuru Mwenyezi Mungu, kama lingekuwa jambo hili limeanzia Kariakoo na hali hii tuliyokuwa nayo sisi hii, aah saa hizi Tanzania ilishateketea! Kwa kuwaimeanzia China ili sisi huku tujipange. Tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika watu ambao wamenufaika katika Awamu ya Tano, ah, basi Jimbo langu mimi *Alhamdulillah*. Katika Vituo vya Afya, nina vituo vya afya vitatu, aah, vizuri vyote! Nanjilinji mambo safi, Pande mambo safi, Masoko mambo safi. Barabara ya kwa Mkochi imekwisha, barabara za lami pale Masoko zimejengwa; aah, mambo *Alhamdulillah!* Mahakama nzuri kabisa, Chuo cha Maedeleo, aah, utasema watoto wako Chuo Kikuu cha nani, kizuri kabisa! Hakika katika sifa ambazo Chama cha Mapinduzi kinasifiwa, basi Kilwa *Alhamdulillah*, hasa Kilwa Kusini! Mambo mazuri kabisa. Ninaamini kabisa kwa juhudi za Serikali ikisimamiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haya mambo ndio yametimia.

Mheshimiwa Spika, maana yake kuna wengine wanasema sijui Serikali Chama cha Mapinduzi; hapana, kazi ya Bunge ni kuvisimamia Serikali na kuishauri Serikali. Kwa hiyo, haya yote yanayofanyika ni kwa sababu Bunge lako liko *strong*. Wala siyo CCM, CCM ilikuwa zamani tu, haya hata hayakufanyika. Hayakufanyika haya! Hii inatudhihirishia sasa, kumbe CCM hii ikitesa kwa makusudi, lakini miaka minne tu mambo mazuri eti. Miaka 50 ya CCM imeshindwa. Ingelikuwa *speed* hii mnayoifanya ya miaka hii minne kama mngeliana miaka 50, sasa hivi tusingeongea habari hizi. Yangakuwa mengine kabisa, lakini mmetuchelewesha. CCM imetuchelewesha! (*Kicheko/Makofi*)

MBUNGE FULANI: Sana tu!

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, kama mngelifanya haya, kwa *speed* hii kwa mpangilio huu, aah, sasa hivi Tanzania kama Ulaya.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Kwa hiyo, mimi nashukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Bungara, kuna taarifa.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Muda wangu, muda wangu jamani.

SPIKA: Aah, tunauchunga. Maana ulianza vizuri, halafu unataka kuharibu tena! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri tafadhalii. (*Kicheko*)

TAARIFA

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Bungara ambaye anaendelea kuongea sasa hivi kwamba Chama cha Mapinduzi wananchi walikikubali kikamchagua Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ndio Rais wa Tanzania, hakuna Rais mwagine. Rais alichaguliwa na wananchi wote mpaka hao wa Kilwa. Ndiyo maana Rais wetu hana upendeleo na katika kauli zake thabiti amesema maendeleo hayana chama, ndiyo maana katika uongozi wake ametekeleza maendeleo maeneo yote, ilimradi ni Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niliona nimpe ndugu yangu, Mheshimiwa Bungara, hayo ili aweze kujua anachokiongea, ni kwamba imetekelezwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Rais wa Watanzania wote.

SPIKA: Anachosema Mheshimiwa Bungara ni kwamba Serikali hii imetekeleza miradi yote hii bila upendeleo pamoja na kwamba wapinzani mlipiga kura mfululizo kwa miaka yote ya hapana kwa bajeti hiyo. Ndicho anachosema tu.

Endelea Mheshimiwa.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, mimi naona hatugombani sana kwa sababu kasema; nami nilisema zamani kwamba hii Serikali siyo ya CCM, ni ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli. Kwa hiyo ananiunga mkono tu. Kwa hiyo, wala sina matatizo na hilo. Mimi nilichosema, Serikali

ya CCM miaka 50 imeshindwa, lakini ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli si ndiyo imefanya! Sasa tunapishana wapi? (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitunzie muda wangu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazuri haya na safari hii mimi nitapiga kura ya *neutral*, inaitwaje ile?

MBUNGE FULANI: *Abstain,*

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: *Abstain;* sisemi hapana wala ndiyo, kwa sababu kuna mazuri halafu kuna mabaya. Kwa hiyo, nitakaa kati kwa kati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na maendeleo haya yaliyokuwepo lakini sisi Waheshimiwa tunaishi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tunaapa hapa kuwa tutailinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tunachukua misaafu na nini, tunalinda, tunaapa! Ukiapa hapa ina maana kuilinda Katiba ni pamoja na kukaa katika Ubunge miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuna watu wameapa hapa, nitailinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; katikati ya miaka mitatu wameshuka, wametoka Bungeni amekwenda CCM.tatizo liliokuwepo, walipokwenda kule wakaahidiwa watapata Ubunge. Kwa hiyo, wakaacha Ubunge. Waliapa kwamba sisi tutakuwa katika Bunge miaka mitano, halafu wakatoka wakaingia CCM, halafu kufika CCM kule, wakaomba Ubunge. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kitendo kile cha kuomba Ubunge; na kwa kuwa waliahidiwa kwamba watapata Ubunge, wakasimamia, ndipo tunaposema Tume sio huru sasa. Tume sio huru hapo. Wakahakikisha lazima Mheshimiwa Maulid Mtulia awe Mbunge tena. Kwa kuwa wapinzani tulikuwa tuna nguvu, wakafanya figisufigisu kwa sababu wamevunja Katiba ya Jamhuri, akapigwa mtu risasi; alivyopigwa mtu risasi ni kwa sababu ya huyu Mtulia aliyevunja Katiba...

SPIKA: Samahani kidogo Mheshimiwa Bungara. Nilikuwa nawatafuta baadhi ya watu humu ndani; hivi Mheshimiwa Lusinde yupo! Ndio mchangiaji atakayefuata baada ya hako wewe. Nilitaka kumpa taarifa tu.

Endelea Mheshimiwa Bungara. (*Kicheko*)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, anapokuja leo Mheshimiwa Mtulia akasema Chama cha CHADEMA kifutwe kwa sababu ya kuua, lakini sababu ilikuwa Mtulia. Aliacha Ubunge ndani humu Mheshimiwa Mtulia wa Kinondoni huyu. Tunaposema tume siyo sawasawa, huyu Mtulia akapita bila kupingwa kwa tume kusema kwamba watu wa CHADEMA na CUF hawakupeleka fomu, akapita bila kupingwa.

Mheshimiwa Spika, tunaposema tume siyo huru wala halali, kwetu Kilwa sisi Madiwani wetu wamerudisha fomu kabisa, Mkurugenzi akasema fomu hazikurudishwa, wamepita bila kupingwa. Tunaposema tume siyo halali, siyo kwa sababu tu tume siyo huru; pale Maalim Seif anaposhinda na anaposema kwamba mimi naongoza ukafutwa uchaguzi. Tunaposema tume siyo halali ni hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana, tume huru ipo lakini watu sio huru. Sijui mnanielewa! Tume huru katika Katiba ipo, imeandikwa tume huru, lakini watu sio huru na wasimamizi sio huru. (*Makofi*)

SPIKA: Samahani kidogo. Tume hiyo hiyo inapomtangaza Selemani Bungara zaidi ya mara moja kwamba ameshinda uchaguzi, ni huru siyo huru?

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, inakuwa hivi, lazima utoe kongoro kwenye mchuzi. Inaitwa kongoro mumchuzi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo tunavyoongea hapa tumesema mengi katika Bunge hili kuiambia Serikali, lakini miaka mitano imepita sasa hivi hali si nzuri. Nilisema hapa

kuna watu wamepigwa risasi katika msikiti, Mheshimiwa Ismail Bweta kapiqwa risasi msikitini; tumesema kwa Waziri Mkuu, kwa Waziri wa Mambo ya Ndani, hamna chochote kinachofanyika, hali mbaya.

Mheshimiwa Spika, juzi wamekamatwa watu, wamechukuliwa watu na watu wasiojulikana, watu sita njia nne hapo; mtu wa kwanza Juma Selemani Farahan, Omary Kassim Mkwachu, Rashid Abdallah Mwinyigoha, Nurdin Ally Mnysiwiwa, Selemani Sefu, Yussuf Ramadhan, tarehe 15 Januari, wamechukuliwa hatujui wapi walipopelekwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaposema kwamba, Serikali ya CCM hamuwezi kushinda Masheikh wetu mpaka sasa hivi wako gerezani miaka sita, hamuwezi kushinda! Tunaposema Serikali ya CCM haiwezi kushinda sio kwa sababu ya kujenga barabara, barabara hata Afrika Kusini zipo, Marekani huko zipo na watu wanatolewa vilevile, barabara nini? Sisi Kilwa Kivinje barabara tulikuwanayo tukaikataa CCM, barabara sisi hatuchagui barabara tunataka utawala bora, utawala wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo watu wanatekwa wanapotea, wanapigwa risasi, Serikali ya CCM imekaa kimya tu. Katiba inasema kabisa kila mtu ana haki ya kuishi, nataka Serikali ya CCM Masheikh watoke Mahakamani; hatuna matatizo kukamatwa kwa watu, tuna matatizo mkiwakamata! Muwapeleke Mahakamani. Watu wetu wamekamatwa hawa sita Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 15 wamekamatwa watu sita hatujui waliko na wamechukuliwa na watu, nini jamani? Halafu ninyi mchukue nchi ninyi? Mchukue nchi kwa kitu gani? Kwa barabara? Kwani Afrika Kusini barabara zilikuwa hakuna? Umeme ulikuwa hakuna? Walienda watu wakaenda wakamtoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana Waziri Mkuu tunakuomba sana. Tena Waziri Mkuu hata Kilwa hujaja kila siku unatuongopa tu nakuja leo, nakuja leo; njoo Kilwa tuje kukuambia mambo...

SPIKA: Mheshimiwa Bungara nchi hii kubwa anazunguka kila mahali atakuja tu.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, na Kilwa si katika nchi? Au Kilwa sio nchi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana vijana hawa sita hawa wamechukuliwa eti Serikali ya CCM miaka mitano mnashindwa watu kuwajua watu wasiojulikana, mnashindwa kuwajua ninyi? Kweli mnashindwa kuwajua ninyi? Intelijensia ninyi, mukutano wa Bwege mnauzuwia, intelijensia, watu wanachukuliwa vijana wetu...

MBUNGE FULANI: Wamechukuliwa na nani?

MHE. SELEMANI S. BUNGARA:....Hamuwawezi, hamuwezi kuwakamata?

MBUNGE FULANI: Wamechukuliwa na nani?

MHE. SELEMANI S. BUNGARA:...kuna nini Mheshimiwa, sikiliza, kuna kitu gani? Kuna siri gani?

Mheshimiwa Spika, tuliambiwa na Mkurugenzi wa Upelelezi hapa wa Usalama wa Taifa hakuna jambo linalofanyika Tanzania Usalama wa Taifa hawalijui, hapa kuna nini hapa? (*Makofii*)

SPIKA: Labda kulisaidia Bunge japo muda wako umeisha, wamechukuliwa na nani hawa watu?

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, na watu wasiojulikana.

SPIKA: Hawa vijana sita?

MHE. SELAMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, watu wasiojulikana, lakini CCM mnawajua, mnawajua. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Bungara muda wako umeisha. Ahsante sana Mheshimiwa Selemani Bungara. (*Makofi*)

Sasa ni Mheshimiwa Lusinde atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mungu sana kunipa wasaa huu wa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake, Waheshimiwa Mawaziri Mheshimiwa Jenista pamoja na Mheshimiwa Angela Kairuki; Manaibu, Mheshimiwa Ikupa pamoja na Mheshimiwa Mavunde, lakini Makatibu Wakuu Ndugu Nzunda, Ndugu Massawe pamoja na Dada Doroth. Tunawapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Chama Cha Mapinduzi ni kweli kinalea watu vizuri. Ukitazama wakati ule anatoka Mheshimiwa Mizengo Pinda na anaingia Mheshimiwa Majaliwa alikuwa mtu mpole, mtulivu, mwanamichezo tena alikutwa uwanjani; watu wengi hatukufikiri kwamba, Mheshimiwa Majaliwa angeweza kukimudu kiatu cha Mzee Pinda, lakini leo ninapochangia hotuba ya mwisho ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nataka nichukue fursa hii kukupongeza sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa, kiatu umekivaa kimetosha, lakini umekuwa Mheshimiwa Majaliwa yuleyule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtakubaliana nami kwamba, Mheshimiwa Majaliwa cheo hakijamvaa, amebaki kuwa Mheshimiwa Majaliwa, mtu mpole, mtu anayeheshimu kila mtu, mtu anayefanya kazi zake kwa utaratibu mzuri. Mheshimiwa Majaliwa tunakupongeza sana na kweli Chama Cha Mapinduzi ni msitu, kinatoa viongozi wakutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mengine unayowasikia watu wanajaribu kuamsha tu *moral* ya wapiganaji ili waingie

kwenye uchaguzi walao wakiwa na *moral*, lakini nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Rais timu aliyoipanga, hili Baraza la Mawaziri linalofanya kazi wakati mwingine mpaka usiku wa manane limeiweka CCM katika hali nzuri ya kuingia kwenye uchaguzi tukiwa na ushindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, chama chetu kingepwaya kama ninyi msingepambana, lakini Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri mmepambana katika sekta zote; sekta ya afya, sekta ya ardhi, sekta ya madini, sekta ya uwekezaji, yaani mmetuweka katika mazingira mazuri ambayo wapinzani wetu sasa hoja hawana wanakimbilia kwenye vitu vidogovidogo kama kutafuta refa awe huru, refa awe nini, ukishaona timu inakimbilia kwa refa, jua jiyo timu tayari iko taabani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba, uchaguzi tu joto la uchaguzi ndio linalosababisha unaona tume sasa inaitwa sio huru. Sijui utawapata wapi, juzi tumeona kiongozi mkubwa kabisa tena anayeongoza upinzani Bungeni akiteuwa watu anasema nimekuteuwa kuwa Katibu Mkuu na watu wanapiga makofi. Anasema nimekuteuwa Mheshimiwa Heche kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu na mziki unafuata, “*Mbowe tubebe*”, wala hakukuwa na tume, alikuwa mwanaume mmoja anafanya uteuzi na watu wote wanapata nafasi. Aah! Sasa leo hii wanazungumza kitu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maana tumeona. Maana hivi vitu sio siri unaona wazi...

SPIKA: Mheshimiwa Lusinde na hapa Bungeni wanashukuru kuteuliwa.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, naona kabisa na uteuzi umekuwa mzuri kwa sababu Wabunge wanaume hawaaminiki sasa Mheshimiwa Mbewe karudi kwa wanawake ambao naamini kwamba, hawa wanaaminika kuliko hawa wanaume walioachwa kwa hiyo, amefanya vizuri kwa kweli. Nakubaliananaye kwamba,

hawaaminiki kwa sababu, hata kwenye chai ukikutananao kuna wengine wana mpango wa kuhamza mwishoni kwa hiyo, Mheshimiwa Mbewe yuko sawa kabisa kuwaacha hawa wanaume na kufuata akinamama, yuko sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema kwamba, jambo zuri wangelifanya baadhi ya Wabunge wa upinzani kama alivyofanya Profesa. Profesa ameonesha, unajua kama unaona maji mazito aga, jamani tumieni Bunge hili kuaga kuweni wastaarabu; hivi saa hizi unaomba lami kweli jamani, Bunge hili unaomba lami? Hiyo *game* imeisha hiyo, *game* imeshaisha hapa tunajadili uchaguzi, keshokutwa Rais anakuja anasema Bunge limevunjwa, wewe unaomba lami kilometra 70, taabani hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwashauri tutumle haki ya kidemokrasia wakati mwingine kuaga. Ukiiona maji yamezidi unasema jamani eeh!, kama alivyo sema mama kwamba, jamani naomba niwashukuruni safari ijayo sitakuwepo na wewe tumia zile dakika tatu ambazo umemuachia nina hakika huyo Mbunge atatumia kuaga badala ya kuendelea hata kuzungumza mambo mengine.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Taarifa Mama Anna, Profesa Tibaijuka.

TAARIFA

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Spika, asante sana, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Lusinde kwamba, mimi sikuaga kwa kuwa maji ni marefu, kule Muleba Kusini niko imara kabisa, nimeaga kwa sababu ninang'atuka, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, mama maji kule mazuri si tuko CCM mama, nazungumza ambao hawako kwenye chama hicho ndio ambao maji

yanazama mama yangu, sizungumzii wewe Profesa. Wewe ungepita bila kupingwa. (*Makofi/kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nimeona hapa Wabunge wanazungumza kwamba, ooh, magereza wanapiga wanawake. Jamani magereza hawawezi kupiga wanawake, Jeshi letu la Magereza haliwezi kupiga wanawake hata siku moja, Jeshi la Magereza linashughulika na wahalifu sio jinsia, halishughuliki na jinsia ya mtu. Kwa hiyo, akiwa mhalifu mwanamke wanachukua, akiwa mhalifu mwanaume wanachukua, yaani wao hawashughuliki na jinsia wanashughulika na matatizo kwa hiyo, nataka niwapongeze sana Serikali hii kwa kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeona namna ambavyo mwaka huu mvua imekuwa kubwa na Ofisi ya Waziri Mkuu ndio inashughulikia maafa. Barabara nyingi za Wabunge, hasa zile za vijiji, barabara zimegeuka mito kwa hiyo, tunaomba muiweszeshe *TARURA* kwa haraka ili itengeneze barabara za kwenda kukusanya kura maana hizi kura tutazifuata vijiji kwa hiyo, barabara zitengenezwe ili watu waweze kufika, wafike Manda, wafike kule *Mvumi Mission* lile daraja litengenezwe, wafike kule chini Loje kule tukusanye kura za Mzee Magufuli, habari ya uchaguzi na hoja mnaziona hapa hazipo.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kusimamia ukusanyaji wa mapato na nidhamu ya matumizi ya fedha, maana kukusanya kitu kingine, lakini nidhamu jambo jingine. Tumeona namna ambavyo kwa kutumia pesa zetu za ndani kila kijiji kinapata umeme kwa sababu, ya nidhamu ya mapato na nidhamu ya matumizi. Tumeona namna ambavyo migogoro ya ardhi inashughulikiwa na Mawaziri mpaka usiku wa manane kwa sababu ya nidhamu ya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa watu waliofanya, nataka niseme, CCM haiwezi kujisifu kwamba, inapendwa ila vitendo vinavyofanywa na viongozi wa Serikali vinaonesha chama hiki kinapendwa. Chama Cha Mapinduzi kadiri

mtakavyotenda mema ninyi Mawaziri mnaturahisishia kazi, tunakaa kwenye mserereko wa kuingia moja kwa moja, yaani kama ni meli iko kwenye chetezo inaingia tu baharini. Sasa hapa tunashindana na nani jamani hii hali mnavyoiona hivi? Hamna kitu na ninataka niwaambie wakati mwингine watu wasiseme tunafuta demokrasia, hatufuti, timu ya mpira wa miguu inajifuta yenyewe kwa kufungwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na timu hapa inaitwa Zimanimoto, iko wapi? Tulikuwa na timu inaitwa *CDA*, imefungwa na ndivyo ambavyo hawa mwezi wa 10 tunakwenda kuwafungilia kwa mbali na kuwashusha daraja, wala sio kwamba, kwa kufuta demokrasia ni nguvu tu; kazi imefanyika Watanzania wameamini, wamekiamini Chama Cha Mapinduzi wanakwenda kukichagua Chama Cha Mpinduzi, sio suala, lazima tuwambie hapa wazungu. Hatufuti...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Lusinde nafikiri tutakubaliana kwamba, mkimuona ile suti yake ilivyokaa kwa kweli, ni kiwango. (*Makofi/kicheko*)

Ilikuwa ni kengele ya kwanza tu Mheshimiwa bado unaendelea na dakika zako, malizia. (*Makofi*)

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, tunakushukuru wewe kwa kuongoza Bunge vizuri, Bunge limeongozwa kisayansi. Ule upinzani wakukurupukia hoja ndogondogo hizi oooh! Ufisadi, haupo sasa kwa sababu, nidhamu iko Serikalini kwa hiyo, maana yake nini?

Mheshimiwa Spika, maana yake Watanzania sasa wanakwenda kufanya uchaguzi mwepesi ndio maana mnaona sasa inalalamikiwa tume. Hoja iliyopo sasa sio CCM mafisadi, hoja iliyoko sasa sio CCM kuna wizi wa fedha, hoja iliyoko sasa sio CCM wameshindwa kumaliza migogoro, aah aa, hoja iliyoko ya refa, wanataka refa, sasa huyu refa anatoka wapi? Atatoka nchi gani refa atakayesimamia uchaguzi? Mbona kwenye chama chao hawatuoneshi

namna ambavyo wanafanya uchaguzi? Tunaona tu mwanaume mmoja kwenye *clip* anasema nimekuteuwa kuwa Katibu Mkuu, nimekuteuwa kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu, nimekuteuwa, halafu na kanyimbo kanamsindikiza; mbona hawabishi kule wanakujaje kubisha huku?

Mheshimiwa Spika, Tena huku hakuna uteuzi, huku ni shughuli tu. Unaenda kuomba kura, unapewa kura shughuli zinaisha. Kwa hiyo, nataka nikuombe Bunge lako hili tujipange kuhakikisha kwamba, mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, habari ya *corona* imezungumzwa hapa, ninachotaka mtusaidie tu, maana mnaposema kila mnayemuhisi ana *corona* mnampelika kwenye kambi na wagonjwa wako kwenye kambi. Sasa hapa watusaidie maana kuhiwi sio kuugua, unaweza ukahisiwa una *corona* halafu ukapelekwa kwenye kambi yenyé wagonjwa wa *corona*, sasa pale unakuwa tena umepelekwa kupata *corona* au umepelekwa kusaidiwa?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ingekuwa vizuri Serikali ikuatuonesha kambi tofauti kwamba, kambi fulani iwe kwa ajili ya wanaohisiwa tu, haina mgonjwa. Kambi fulani hii ni kwa ajili ya wagonjwa tu, haina mtu anayehisiwa na kambi fulani wanapelekwa hotelini wale waliotoka nje, lakini mkisema tu kila mnayemuhisi, Mloganzila, wagonjwa Mloganzila, eeh ee!

Mheshimiwa Spika, sasa tunapata shida hapa. Ni lazima kuwe na tofauti ya mtu anayehisiwa na mtu anayeugua, ili tusije tukachukua watu tunaowahisi tukawapeleka kwenda kuugua badala ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la mwisho nakushukuru sana, umefanya kazi kubwa, umeliongoza Bunge kisayansi. Na hata wale ambao walikuwa na mashaka na wewe wakati unaingia mashaka wameondoa, wamegundua kwamba, Mzee Ndugai ni mzee wa viwango. Anaweza kulibadilisha Bunge hata akina Lusinde sasa tunabofya tu, maana mwanzoni tulikuwa tunaonekana mimi

na Bwege labda tutapata shida katika kubofya, lakini watu wako wametusaidia mpaka mimi na Bwege sasa tunabofya na tunaingia humu ndani na mambo yanakwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Livingstone Lusinde, nakushukuru sana kwa mchango wako. nilikwishakutaja Mheshimiwa Fatma Toufiq na utafuatiwa na Mheshimiwa Sophia mwakagenda.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa nami kuchangia hoja ilio mbele yetu katika hili Bunge lako Tukufu. Kwanza naomba nichukue fursa hili kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwilingi wa rehema, mwiningi wa ukarimu kwa kunipa uhai wa kuweza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Wabunge wenzangu wote kwa ajili ya kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote pamoja na watendaji wote kwa kuandaa hotuba hili. Kazi ambayo imefanywa na uongozi chini ya uongozi wa Rais wetu mpwendwa Dkt. John Pombe Magufuli inaonekana. Tunachotakiwa sisi ni kuendelea kumtia moyo, kumpongeza, pamoja na wale wote ambao wameunda timu kuhakikisha kwamba, Tanzania yetu inafikia ile azma ambayo wamejiwekea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nizungumzie kuhusiana na suala kwanza la ugonjwa huu wa *corona*. Wenzangu wengi wamelizungumzia, niungane na wenzangu kutoa pole kwa Watanzania wenzangu ambao Ndugu zao wamepatwa na ugonjwa huu, lakini pia ambao wameondokewa. Nipongeze sana Serikali kwa juhudhi kubwa sana ambayo inaifanya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, wananchi wanapata elimu ya kutosha kuhusiana na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, lakini bado suala la misongamano lipo na hii inaweza ikaleta athari kwa baadhi ya maeneo. Sambamba na hilo elimu katika maeneo ya pembezoni inahitajika sana, Ndugu zetu wa vijiji ni bado hawana elimu ya kutosha kwa hiyo, nilikuwa naomba nitoe rai kwa Serikali pamoja na Wizara tuone ni jinsi gani elimu katika maeneo ya pembezoni inafika, ili kusudi Wananchi hawa waweze kujikinga na huu ugonjwa hatari ambaao umeleta maafa makubwa sana katika dunia yetu.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa huu wa *corona* umesababisha baadhi ya wafanyabiashara hali ya biashara zao kudorora. Nichukulie kwa mfano, najua kwamba nia nzuri sana ya Serikali kufunga vyuo, kufunga shule, hii ilikuwa ni katika kuhakikisha kwamba, huu ugonjwa hauenei, lakini sambamba na hilo sasa kuna baadhi ya wafanyabiashara ambaao wamekuwa wakifanya kazi kwa kuzihudumia taasisi hizi. Wafanyabiashara hawa sasa biashara zao kwa kweli, zimedorora na kuna baadhi yao wamechukua mikopo. Je, Serikali inaona hawa watu itawasadia kiasi gani kwa sababu, katika kipindi hiki cha mpito ambacho sasa hili janga linaendelea kuwepo na hawa baadhi ya wafanyabiashara wengine waliochukua mikopo benki. Sasa nilikuwa naiomba Serikali ijaribu kuona itawasaidiaje hawa watu, ili kusudi sasa baada ya hiki kipindi cha mpito waweze kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 26 wa hotuba hii umezungumzia kuhusu shughuli zilizochangia ukuaji wa pato la Taifa ambaao umefikia 6.9%. Niipongeze sana Serikali yangu kwa jinsi inavyofanya kazi nzuri ya ukusanyaji wa mapato, lakini sambamba na hilo kuna kundi ambalo natamani kundi hili kwa mfano Serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa makundi ya vijana, makundi ya wanawake, watu wenye ulemavu, lakini pia na wajasiriamali mbalimbali. Nilitamni nione kwamba, hawa nao tunaona wanachangiaje katika pato letu la Taifa, ili mwisho wa siku na wenyewe nao ufanyike utaratibu, kama ni tathmini, au utafiti waweze kuweza kuchangia katika hili pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie kwenye *issue* ya utalii. Naipongeza sana Serikali kwamba, katika hotuba hii kumekuwa na matangazo mengi sana ya vivutio vya utalii katika maeneo mbalimbali, lakini Serikali imebainisha kuwa kuna mkakati wa kuwekeza zaidi katika utalii na hasa katika utalii wa fukwe, utalii wa meli, utalii wa mukutano, utamaduni, mali kale, ikolojia na jilolojia. Nilikuwa naomba niishauri Serikali kwamba, mkakati huu uendane pia na kupatikana na wataalam ambao wataweza kusimamia aina hii ya utalii. Ninaamini kabisa kama tukiwa tuna wataalam wa kutosha basi utalii huu utaleta tija kubwa sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie pia suala la UKIMWI. Nimesikia wenzangu wengi wamelizungumza na tunafahamu kwamba Serikali imejitahidi sana naipongeza sana kwa kufanya kampeni kubwa sana. Zimefanyika kampeni kubwa sana katika kuhakikisha kwamba UKIMWI unapungua au unakwisha kabisa. Hata hivyo, kuna hii *AIDS Trust Fund*, nashauri Mfuko huu tuone tunafanya utaratibu gani wa kuweza kupata rasilimali za kutosha. Kutokana na taarifa zilizopo ni kwamba hawa wafadhili ambao wamekuwa wakitoa ufadhili kwa ajili ya dawa na kadhalika wameanza kupungua.

Mheshimiwa Spika, naona kama litapatikana tozo la kuweza kusaidia Mfuko huu ukatunishwa, ina maana kwamba sisi wenyewe kama nchi tutaweza kujitegemea na hivyo suala zima la *prevention* na mambo mengine ambayo yanahusiana na hayo Mfuko huu utaweza kusaidia. Hivyo, kupitia makampuni mbalimbali kama ya simu au pengine taasisi mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanya miradi mbalimbali tunaweza tukawawekewa utaratibu maalum wa kuwa na tozo maalum kwa ajili ya Mfuko huu, naamini kabisa nayo hiyo inaweza ikasaidia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kushauri ni kuhusiana na suala zima la mkakati wa *behavioral change* kwa ajili ya vijana wetu kuanzia miaka 15 – 24 kwa

sababu inaonekana kwamba hili ni kundi kubwa ambalo limekuwa likiathirika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ni kuhusiana na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Kwanza nipongeze sana Mkutano wa Wakuu wa nchi wa SADC kwa kuamua kwamba Kiswahili kiwe ni mojawapo ya lugha rasmi katika mikutano hiyo. Sambamba na hilo, imeonesha kwamba bado wataalam wa Kiswahili tunao wachache sana. Kutokana na taarifa iliyopo katika ukurasa 104 wa hotuba hii, imebainika kwamba wataalam waliopo wa Kiswahili ambao wamesajiliwa ni 1,159. Hii ni idadi ndogo sana, kwa hiyo naiomba Serikali basi vijana wengi zaidi wahamasishwe ili kusudi wawe wataalam wa Kiswahili na hatimaye waweze kutangaza Kiswahili chetu katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, najua muda sio rafiki sana naomba nizungumzie kuhusiana na suala la mikopo kwa elimu ya juu. Ukurasa wa 66 unazungumzia kuhusu mikopo, niipongeze Serikali kwa ule wigo kuwa mkubwa wa upatikanaji wa mikopo. Kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya hawa wanufaika wa mikopo kwamba hii mikopo wakati wa urejeshaji kumekuwa na sintofahamu. Kwa mfano utakuta kwamba pengine mtumishi au kijana katika *salary slip* yake inaonesha kwamba ile *outstanding loan* ni milioni 20 lakini akienda kule Bodi ya Mikopo anakuta *outstanding loan* ni milioni 24. Kwa hiyo natamani labda ungefanyika utaratibu wa kuhakikisha haya madeni ili kusudi hawa vijana wetu wasije wakaona kwamba kuchukua mkopo imekuwa ni *burden* kubwa sana kwao. Kwa hiyo akianza kufanya kazi ile pesa nyingi inachukuliwa, kwa hiyo naomba Serikali ijaribu kuona jinsi gani itaweza kuangalia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hassan Toufiq. Nilikutaja Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Nafikiri pia ninao wajibu wa kuzungumzia suala la ugonjwa wa *corona* lakini nitakuwa tofauti kidogo na wenzangu. Ugonjwa huu ni ugonjwa wa Kidunia na ni tatizo linalotuhusu Tanzania na wanaotuzunguka na dunia kwa ujumla. Nataka kumwomba Rais, afikirie tena aweze kufunga mipaka ya nchi kwa sababu; kuna watu wanafika pale *Airport* wakitokea nje wanarudi nyumbani. Anajua akifika *Airport*, anaita *uber* yake anakwenda kwake labda Tabata au Manzese lakini akifika pale anachukuliwa kwenda kwenye *isolation*, sawa tunakubali siku 14, lakini wanapelekwa kwenye hoteli za gharama na ndiyo maana watu wanatoroka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sijajua ni utaratibu gani unatumika, labda watusaidle na hasa watu wa TAKUKURU, hizi hoteli zimekuwa *vetted* vipi na kwa nini ziwe hoteli za gharama na Ofisi ya Waziri Mkuu ni ofisi ambayo ina fungu la majanga na maafa kama haya. Mimi nikiwa na *corona* na nimetoka safari, sijapanga mimi niwe na *corona*, kwa hiyo ina maana imekuja mimi nikiwa sina pesa. Kwa nini Serikali isifanye maeneo tofauti ya kuwaweka hawa ndugu zetu, wakakaa hizo siku 14 bila gharama hiyo kubwa, dola 150, dola 100, dola 50 hizo ni hela nydingi sana kwa hawa watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nafikiri tuna haja kwanza ya kufunga mipaka kwa sababu sisi sio kijiji na wala sisi hatuna *TBS* ya kuzuia magonjwa yasituingie. Naomba tulifikirie kwa upya na tukae chini kwa upya tujipange na hasa Wizara hii tunayoizungizia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba niongeze suala la Wizara hii ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu alilizungumza. Ofisi hii imetamka vipaumbele vine, moja ya kipaumbele wanazungumzia uchumi wa viwanda, uchumi wa viwanda bila kilimo huwezi kufanya maendeleo yoyote. Asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima. Usipouanganisha viwanda na kilimo huwezi kupata faida yoyote. Tunafahamu kiwanda, mkulima wa korosho amelima korosho, tumeimba

wimbo huu muda mrefu sana kwamba hawa watu wanahitaji viwanda vya kubangua korosho hapa nchini, lakini mpaka leo viwanda hivyo bado havijawa tayari. Tuna wakulima wa chai kule Rungwe, kwenye ripoti ya Waziri Mkuu anazungumzia yule mkulima wa parachichi, yule ni mfanyabiashara binafsi. Serikali inahitaji kuwa na kiwanda, inahitaji kuweka miundombinu ya wakulima wa parachichi waweze kuza kwa bei ambayo yule mfanyabiashara binafsi anapata faida mara nne na sisi tunafikiri tunapata faida kumbe tunamnufaisha mtu mmoja.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa tunapozungumzia viwanda ni lazima tukae chini tuoanishe kati ya viwanda na kilimo, kwamba kilimo kinapolimwa na chai inapolimwa tuwe na viwanda vidogo vidogo vya chai. Zao la chai linanyweka nchi nzima. Kama sio Tanzania lakini dunia nzima wanunuua chai na wala hatujawahi kusikia soko la chai limeshuka bei. Leo hii Wakanya wanunuifaika kwa zao la chai, lakini sisi hatuna viwanda, tunapeleka kitu ambacho hakina thamani zaidi. Tungekithaminisha katika nchi yetu tungesaidia wakulima wetu kupata kipato. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia uchumi ambao unaoanisha uchumi wa mtu binafsi na uchumi wa Kitaifa, mimi naweza nikaona kwamba sipati hela kwa sababu thamani ya mali ninazozizalisha hazifanyiki hapa nchini. Kwa hiyo tuna haja kubwa na ya makusudi tuweze kutengeneza uwezo wa watu wetu kuzalisha na kupata wateja na sisi tuna watu wengi, tukijipanga vizuri, soko la ndani bado linatuhitaji. Kwa hiyo, nilitaka nichangie katika maeneo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia nataka niingie kwenye habari ya siasa, nimesikia watu wengi wanazungumza humu ndani. Chama cha upinzani chochote kilichomo humu ndani kipo kihalali na kikatiba. Kubezana sidhani kama ni njia sahihi, tunapozungumzia haki, haki inabeba vitu vingi sana. Leo hii ni nani humu ndani, mimi najua na kama mama kuna akinamama wenzetu ambao ni wabaya waliolea watoto wa kambo, anamshika mtoto wake ili ampige mtoto wa kambo. Ni kweli yule mtoto anafurahi, ndivyo ambavyo wenzetu humu

ndani wanafurahi, lakini wasijue wanajenga *immune* ya kiburi kwa sababu kila siku ukipigwa, kesho tena umepigwa, unajenga kiburi na unajjengea ujasiri, mmetujengea ujasiri *unnecessary*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni nani asiyejua kwamba leo hii watu wanafanya mikutano, kundi fulani linafanya lingine halifanyi. Ukiuliza, intelijensia, intelijensia hiyo iko upande mmoja? Intelijensia hiyo iko kwa nani peke yake?

SPIKA: Umesema nani asiyejua? Spika hajui, tutajie kwamba fulani anafanya mkutano na fulani hafanyi.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, unafahamu kwamba kiongozi wako wa chama cha siasa Mwenezi Polepole anazunguka nchi nzima. Mnyika kazunguka Mwanza mmemkamata! Kama ullkuwa huna taarifa nakupa taarifa! Ni watu wangapi wanafanya mikutano? Mheshimiwa Sugu Mkoa wa Mbeya hafanyi mikutano, *RPC* anakwambia intelijensia inakataa, Tulia juzi tu hata siku nne hazijaisha na *corona*, yuko na wananchi! Ina maana huoni? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, undugu tuliozaliwa nao, urafiki tuliokuwa nao...

SPIKA: Mheshimiwa Mwakagenda, kawaida ya Maspika wote duniani wao huambiwa!

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, nakwambia.

SPIKA: Ahsante!

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: *Mheshimiwa Spika, undugu tuliojengewa humu ndani kuna watu wana maboyfriend humu, kuna watu tuna kunywa chai pamoja humu lakini kwa tabia hii... [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

SPIKA: Mheshimiwa Sophia, una hakika? Maana meza yangu haijui hayo...

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: ... mimi ninaye!
(*Kicheko*)

SPIKA: Meza inakutaka basi utoke wazi maana umeamua kutoka wazi! (*Kicheko*)

MHE. SOPHIA H. MWAKAENDA: Mheshimiwa Spika, nimetuma barua kwa Mwakagenda, akishaniridhia nitatoa hadharani.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji umaja, kujenga umaja ni kazi kuubomoa ni kitu kidogo. Sisi sote tunawakilisha wananchi...

SPIKA: Nafikiri Sophia hapo ulipokwenda ama uendelee ama ufute kwa sababu umelituhumu Bunge na nina hakika magazeti yote yatajaa kwamba watu wana mahawara humu ndani na watu wana wake zao na waume zao na heshima zao. Kwa hiyo ni bora ukajitokeza tu wazi ukaeleza nani na nani ni mahawara humu...

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, mimi nimefuta, naomba niendelee.

SPIKA: Basi kama umefuta tunaelewana.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyositisiza umaja ni muhimu, mwisho wa siku sisi ni ndugu tumetumwa na wananchi kuwawakilisha, tufanye kazi kwa pamoja bila kubaguliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee suala la Tume ya Taifa. Ameizungumza msemaji mmoja kwamba tunakimbilia kusema refa atutetee. Tume ni refa ndio wala sio utani! Lazima asimame katikati na sisi tumesema toka mwanzo tungebadilisha kanuni zetu na taratibu zetu,

Mwenyekiti wa Tume akachaguliwa na Bunge hili au na kitu kingine chochote tusingekuwa na malalamiko haya.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Tume ni uchaguzi, mwanzo wa mwaka mpaka miaka mitano inapoisha, ndiyo kazi yake. Kazi yao kuhakikisha watu wanajiandikisha kwenye madaftari, watu wanapiga kura na kusimamia uchaguzi na kuhakikisha mtu anayestahili kutangazwa anatangazwa, lakini utakuta siku za kuijandikisha Tume inaweka siku chache. Watu wengi hawaajaandikwa, tukienda kule Zanzibar, watu wengi hawana vipande, wameshindwa kuijandikisha kupiga kura ili waje wachague mtu wanayemtaka.

Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Mheshimiwa Sophia pokea taarifa. Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, naomba tu nimpe Taarifa Mheshimiwa Sophia, utaratibu wa Tume katika kufanya jambo lolote ambalo linahusu uchaguzi ni utaratibu shirikishi. Kabla Tume haijaanza kuandikisha wapiga kura, kabla haijaanza kuboresha daftari vyama vyote vya kisiasa vimekuwa vikishirikishwa na vinakuwa na maamuzi ya pamoja. Kwa hiyo naomba tu nimwambie Mheshimiwa Sophia kwamba hicho anachotaka kukisema si kitu cha kweli kwa sababu kila jambo limekuwa ni shirikishi na baada ya ushirikishwaji Tume ndiyo inaanza kufanya kazi na safari hii imefanya vizuri kweli, hata mikoani haikuanza kazi kabla ya kuwashirikisha wadau wote ikiwemo vyama vya siasa na nafikiri hata Sophia alikuwa anashiriki hiyo mikutano. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu nimpe hiyo Taarifa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

SPIKA: Mheshimiwa Sophia pokea taarifa.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, sijaipokea Taarifa kwa sababu kazi yangu mimi ni kuishauri

Serikali na yeye ni Serikali. Namshauri kwamba Tume kazi yake ni kusimamia uchaguzi mwaka wa kwanza mpaka mwaka wa tano. Tunaomba Tume haina kazi yoyote, Tume haishughuliki na *corona* wala malaria, inashughulika na uchaguzi. Kwa hiyo tunaiomba Tume kuanzia mwaka wa kwanza tunapomaliza uchaguzi iendelee kuwaandikisha watu wapya wanaofikia umri wa miaka 18 ambao walikuwa na miaka 17 wameingia 18 iwaandikishe. Kama kuna watu wamekufa iwatoe kwenye daftari na ukifika wakati tunaenda kwenye uchaguzi sasa, tupate majina mapema. Kwa hiyo, ninachoomba, naishauri Serikali, sio kwamba lazima uchukue Mheshimiwa Jenista, mimi nashauri kama Mbunge ambaye nina wajibu wa kuishauri Serikali na ndiyo kazi iliyoniingiza humu ndani.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa bado sio huru na kama wako vizuri, wamejenga reli, wamefanya kazi zote, kwa nini wana wasiwasi na hiki kitu kidogo tu cha kuunda Tume Huru, kwa sababu wakiunda watashinda! Kwa sababu wana madaraja kama wanavyosema! Tunataka tusiwe na *doubt* yoyote, ndiyo maana tunashauri iundwe Tume Huru ya Uchaguzi na kama uko vizuri, Mbunge unapendwa...

SPIKA: Mheshimiwa Sophia, tangu jana tunauliza, Tume Huru inafananaje? Kila mtu akisimama Tume Huru, Tume Huru...

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Hasemi kwa sababu wasiwasi...

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Usiwe na haraka, dakika zako tunazitunza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Ahsante!

SPIKA: Wasiwasi wetu ni kwamba leo huyu mtu atasema refa hatumwamini, mkibadilisha refa atasema *linesman*, mkibadilisha, Kamisaa, mkibadilisha *TFF*, sasa Tume

Huru hiyo mnayoiongea, wote inafanana? Kila mtu ana picha ya Tume yake au ni nini ili Serikali iweze kukuelewa na kuwaelewa wote wanaoiongelea *subject* hiyo.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Tume Huru na hasa Mkurugenzi Mkuu na watendaji wengi wanateuliwa na Rais ambaye kikatiba na kikanuni ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na nchi hii ni nchi ya Vyama Vingi. Kwa hiyo natoa wazo leo, ni vyema wakaomba kazi, tukawafanyia *vetting*, wakaletwa Bungeni, tukawachagua tukapata mmoja ambaye tunamuamini sisi kama wananchi wa Tanzania na wala sio kuteuliwa na mtu mmoja. Leo hii Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi ndiyo Rais, kesho atakuja mwingine.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

SPIKA: Je, ni nchi gani ambayo unadhanini ina mfumo ambaao Bunge ndiyo linateua Mwenyekiti wa Tume, Sophia.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, tuko kwenye mjadala mpana wa kusaidia Taifa letu, hata kama maongezi yangu unafikiri hayajaenda sambamba lakini wako watu waliopelekwa shule na wanasoma...

MWENYEKITI: Kwa sababu inaelekea unaongelea *subject* ambayo hujafanyia utafiti wa kutosha!

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, tuna Kenya...

SPIKA: Kenya bado pamoja na Bunge kushiriki, Rais ndiye anayemteua Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi. Mimi sikatai hoja yenu, mnielewe! Mimi nia yangu ni kwamba yaani mje na vitu ambavyo mmejiandaa, mmejipanga vizuri, mnapofanya *presentation* mimi siwazuii, unapofanya *presentation* yako yaani unashuka umejipanga, ndiyo maana tunaanza saa nane ili kuwapa nafasi Waheshimiwa Wabunge kuchambua, kuangalia *references* na kadhalika na sisi wengine tunajuajua kidogo kinachoendelea kwa hiyo huwezi

kutudanganya. Hatusemi kwamba Tume iliyoko ni malaika, lakini ni vizuri kujipanga kidogo na kutoa mifano ambayo, yaani kulisaidia Taifa kweli kwa mtu ambaye umefanya *homework* yako, unashuka vizuri. Endelea tu Mheshimiwa Sophia.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, kama chama tumeandika barua kwa Msimamizi Mkuu wa Nchi japokuwa tunaona siku zinasogea nafikiri na maelezo unayozungumza wewe ambayo yameenda kisomi na yaliyoandikwa kihalali ili waweze kusaidia Serikali. Tumeshaandika barua.

Mheshimiwa Spika, viongozi wetu wameshiriki na kuongea na Rais wa nchi kutaka kuitwa na kuzungumza na kuwa na maridhiano ili waweze kueleza ni nini wanachokitaka. Naomba niendelee...

SPIKA: *As long as* hiyo barua hamjaandika kwa Spika wala nakala Spika hamjampa na Waheshimiwa Wabunge hawa hawajui kinachoendelea sidhani kama ni haki kutueleza, maana sisi tunashangaa yaani, hatuelewi ndiyo maana... Nauliza hiyo kwa nia njema unielewe vizuri.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, Serikali kuna Bunge, kuna Mahakama, tumetuma kwa Serikali, mimi naongea hapa ndani kama Mbunge ndani ya Bunge.

SPIKA: Hebu kaa chini! Huyu ni Mbunge gani asiyejielewa? Kama umeandika vitu kwenye mihimili mingine kwa nini unaongea hapa sasa? Subiri, kama unaongea hapa, tueleze na sisi! Unaongea kuhusu kitu gani ufanuzi wake ni nini? Barua yenu ina nini na wewe unaongelea nini? Kuna ubaya gani katika ushauri huo? Kuna ubaya gani katika ushauri huo? Sisi barua yako hiyo hatuna, hatujui! Wewe ndiyo unaijua na huko ulikopeleka. Tunapokutaka sisi tueleze ni kitu gani unaeleza, tunakosea nini hapo?

Anayefuata kuchangia ni Mheshimiwa Aeshi Hilaly, mjipange! Unapokuja jipange!

MHE. KHALFAN H. AESHI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu. La pili, naomba niwapongeze sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa wote kwa kazi kubwa wanayoifanya na hatimaye kuhakikisha Tanzania yetu inasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana pamoja na timu yako nzima kwa kazi kubwa ulioifanya na hatimaye sasa tunakwenda mwaka wa tano ukituongoza kwa umahiri, kwa ujemedari mkubwa na hatimaye Bunge letu liimefanya kazi kwa ufanisi mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nina ajenda moja tu ambayo naomba unisikilize vizuri na Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba ali pe nafasi jambo hili. Nitaongelea suala la wavuvi.

Mheshimiwa Spika, tumelalamika sana kuhusiana na wakulima na hatimaye Serikali ikatusikiliza. Hata hiyo, kwa sababu Mkoa wa Rukwa umezungukwa na maziwa; Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika na Wanazumbawanga wengi ni wavuvi na wakulima leo nitaongelea kuhusu wavuvi. Kwa hiyo, kwenye sekta hii ya uvuvi nataka Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie kwa sababu ameongelea kwenye ukurasa namba 49.

Mheshimiwa Spika, suala la uvuvi, naunga mkono kabisa hoja ya Serikali ya kupinga uvuvi haramu, sigombani nao katika hili. Wavuvi wa *Lake Tanganyika* wanakwenda kununua nyavu hizi madukani.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze kidogo kwamba kuna sheria imepitishwa kwamba nyavu ambazo zinatakiwa zivue ndani ya *Lake Tanganyika* ni milimita 8. Sasa hii milimita 8 inapitishwa na nani? Hii milimita 8 inapitishwa na watu wa *TBS*. Kwa hiyo, wale wenye maduka wanaagiza mzigo kutoka nje, unakuja *TBS* wanaukagua na *TBS* wanapitisha unakwenda madukani na madukani wananchi wale wanakwenda kununua kwa ajili ya kwenda kufanya shughuli mbalimbali za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, inanisikitisha sana, kule *Lake Tanganyika* wale wavuvi wamekwenda madukani, wameuliza nyavu za milimita 8, wamenunua, wamekwenda kwa ajili ya uvuvi lakini kwa bahati mbaya sana Waziri wa Uvuvi pamoja na timu yake ikatuma na kipimo kingine kipyä milimita 8 nyingine ambayo sijui wameitoa wapi. Wamekwenda tena kupima kule, wamekamata nyavu wakasema zile nyavu zipo chini ya kipimo chao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilimpigia simu Mheshimiwa Waziri Mkuu nikamueleza jambo hili, nilimpigia Waziri wa Uvuvi na Mifugo na Waziri wa Viwanda na Biashara, hapa kuna mchanganyiko, inasikitisha sana. Unakuta kuna raia au mtumishi amestaafu, amekwenda nyumbani kafika kule chini *Lake Tanganyika* amekuta kazi hakuna, wakamshauri kazi kubwa tuliyonayo huku ni uvuvi. Yule mtu anachukua kiinua mgongo chake anakwenda dukani kutaka nyavu halali, milimita 8 anaitaka, anapewa. Anafika kule anaunga nyavu zake anaanza uvuvi milioni 15 ameingiza katika uvuvi. Anakuja mtu mwingine wa uvuvi na kipimo chake kingine tofauti na cha *TBS* anapima anasema hii siyo milimita 8, anamkamata, anamtoza faini shilingi milioni tano lakini yule mzee anasema mimi nimenunua dukani; kwa nini hawa wanaouza nyavu wasikamatwe nikamatwe mimi ambaye sijui chochote? Mheshimiwa Waziri Mkuu watu hawa wanaumia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri sana Serikali ilifuatilia ikaunda Tume huru ikaenda kule; wamo watu wa *TBS*, Wizara ya Uvuvi na Usalama wa Taifa kupima zile nyavu zimeonekana ni halali. Sasa Waziri anatoa tamko kwamba anatoa miezi mitatu nyavu zile ambazo zipo chini ya kiwango cha kwaao wao kuwa mwezi Juni wawe wameziondoa. Kwa hiyo, amewapa muda wa miezi mitatu waweze kuvua kwa muda ili waweze kufidia nyavu zile ambazo wamezinunua madukani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kosa la Serikali, Serikali imekuja na vipimo viwili; *TBS* wana kipimo chao lakini Wizara ya Mifugo na Uvuvi na wenyewe wana kipimo

chao, mwananchi atajuaje kipimo halali ni kipi? Mwananchi huyu anayekwenda dukani kununua nyavu atajua vipi kuwa hii ndiyo *TBS* haitakiwi na hii ndiyo Wizara ya Uvuvi inatakiwa kwa sababu nyavu zipo madukani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana au kwa bahati nzuri sana, baada ya Serikali na Tume kugundua kwamba Serikali ndiyo yenyе makosa, wakaruhusu kwamba nyavu hizo zitumike ndani ya miezi mitatu, lakini wameruhusu nyavu wakati sio wa uvuvi. Masika hii wavuvi wote wanasmamisha uvuvi kwa sababu wakivua dagaa wakizianika zinalowana. Wametoa miezi mitatu mwisho mwezi Juni lakini kosa sio lao. Kwa msingi huo ilitakiwa Serikali ilipe fidia kwa sababu makosa ni ya Serikali; makosa ni ya Wizara ya Uvuvi na Wizara ya Viwanda na Biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nillimpigia Waziri wa Viwanda na Biashara anajua na Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikampigia Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi, wamekwenda wamechunguza imeonekana *TBS* wana makosa au Wizara ya Uvuvi ina makosa, kwa sababu wamekuja na vipimo viwili. Ushauri wangu tungewapa watu muda wa mwaka mzima. Shilingi milioni 15 kuirudisha ndani ya miezi mitatu kwa kosa la Serikali haitowezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mvuvi huyu naye anaongeza mapato ndani ya Mfuko wetu wa Taifa, mvuvi huyu ni sawa na mkulima na mvugaji lakini anaonewa siku hadi siku. Mheshimiwa Waziri Mkuu nikuombe sana muda aliota Mheshimiwa Waziri wa miezi mitatu ni mdogo kwa kosa la kwetu sisi wenyewe. Kama Serikali ingeweza kutusaidia basi huu muda ambao tumewapa wa miezi mitatu ambapo wavuvi wamesimamisha uvuvi kwa sababu kuna mvua, hawawezi kuvua wakati huu, uvuvi raski unaanza mwezi Juni, basi waruhusiwe kuanzia mwezi Juni, wapewe muda wa mwaka mmoja waweze kurudisha gharama zao ama Serikali ifidie gharama hizo iwarudishie fedha zao walizonunua nyavu madukani ambapo maduka hayo yanauza nyavu halali na leseni wanazo. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu

atusaidie wavuvi hawa wanahangaika sana na sisi ni wawakilishi wao tuna haki ya kuwatetea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache, naunga mkono hoja. Nikupongeze sana kwa kazi kubwa, nimpongeze na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayofanya kuitumikia nchi yetu. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Aeshi Hillary.

Mheshimiwa Lijualikali nilikuwa nimekuahidi dakika tatu, kwa hiyo, zimebakia dakika tatu za mwisho zile kama ungependa kuzitumia.

Baada ya hapo Mheshimiwa Owenya ana maelezo binafsi nitampa nafasi tuweze kuyasikiliiza.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa tena dakika zangu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa kwenye *issue* ya barabara ingawa ndugu yangu Kibajaji pale anasema huu siyo muda wa barabara na kwamba muda umeisha. Mimi nataka nimwambie tu kwamba mimi ni Mbunge kwa miaka mitano na nimeapa kukaa hapa mpaka nitakapofika mwisho.

Kwa hiyo, mimi nitasema mambo ya Kilombero mpaka siku ya mwisho. Mimi kazi yangu ni kusema mambo ya Kilombero. Ninyi Serikali ya CCM na Rais Magufuli kazi yenu ni kutenda yale mimi nayoyasema kuhusu Kilombero. Kwa hiyo, mimi hapa nitafanya kazi yangu mpaka siku ya mwisho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ifike hatua kule kwenye sheria ya sifa za kuingia Bungeni kidogo zibadilike, shule pia inatakiwa itumike angalau hata *form four* hivi. Mambo mengine ni kutokana na shule inawezekana ikawa watu hawaelewii mazingira ya humu ndani. Kwa hiyo, niombe ifike hatua shule pia iingizwe, mtindo wa kusema kwamba tu mtu ajue kusoma

na kuandika kama Taifa sasa hii issue ifike mwisho, shule itajwe *form four, form six*. Kama dereva wa Serikali anaambiba lazima awe *form four*...

SPIKA: Dakika tatu zinaisha...

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Spika, ni bora ziishe lakini nchi ijue ukweli. Kwa sababu kama kuna Mbunge anakambia eti bwana wewe muda umeisha wakati anajua kabisa tumeapa miaka mitano...

TAARIFA

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuzingatiele elimu kwenye kuchagua Wabunge.

SPIKA: Taarifa, Mheshimiwa Lijualikali naomba ukae upokee taarifa. Mheshimiwa Deo Sanga.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji ajue hata waliomaliza *form four* na wenye *degree wapo failures*. Kwa hiyo, *form four* siyo maana yake ndiyo inayokuingiza hapa. Wapo watu hawana *form four* lakini vichwa vyao ni sawa na mtu mwenye *PhD. (Makof)*

SPIKA: Na huo ni ukweli wa maisha. Mheshimiwa Lijualikali pokea taarifa.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Spika, *issue* siyo kufeli au kufaulu; kama tunasema madaktari wawe na *level fulani*, kama madereva wetu tu lazima wawe na *form four*, wewe unakaa hapa upitishe sheria za nchi, uisimamie Serikali halafu uwe tu darasa la pili au shule huna kabisa. Lazima tuitendee haki nchi yetu. Huyu nimwambie kabisa mimi sijakimbia shule, kwa hiyo, lazima tubadilishe twende kwa *style* hiyo, shule itumike. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kilombero iwe ni mwaka huu au mwakani kwa sababu wahisani wameshatoa fedha na fedha mnazo, mimi kama Mbunge wa Kilombero nawataka mfanye kazi yenu ya kutuletea barabara yetu. Haiwezekani mmepewa fedha za bure kabisa, fedha mnazo mmekalia hamtaki kazi ifanyike kwa sababu zozote zile. Halafu Mheshimiwa Waziri alikuwa anasema suala la VATni suala la kitaalam tu wakati mmeshikilia mitambo ya mwekezaji, mmeshikilia mitambo ya mkandarasi asifanye kazi leo hii unasema kwamba hili suala ni la kawaida tu, maana yake nini?

Mheshimiwa Spika, nimtake Waziri iwe kesho, keshokutwa ama mwakani Kilombero tunataka barabara yetu tuliyopewa na mabeberu. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lijualikali. Kwa sababu ya mkanganyiko kidogo wa muda, nitamuomba Mheshimiwa Vedasto Manyinyi awe mchangiaji wa mwisho, baada ya hapo tutaongeza robo saa tu ili tuweze kumsikiliza Mheshimiwa Lucy Owenya. Mheshimiwa Manyinyi tafadhalii.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili walau niweze kuwa mchangiaji wa mwisho katika siku hii njema ya leo.

Mheshimiwa Spika, nami naungana na wenzangu kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo kusema ukweli imejitosheleza. Hili ndilo Bunge letu la mwisho, tunamaliza miaka yetu mitano na tuna nafasi ya kurudi tena kwa wananchi wetu waangalie kwa yale tuliyowaahidi katika kurejea tena katika *angle* nyagine.

Mheshimiwa Spika, labda niseme jambo moja tu la shukrani ambazo napaswa kumpa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Mwaka 2015 alipokuja pale Musoma wakati wa kampeni, naomba umfikishie hizi salamu, tulimuomba

mambo manne ambayo yote ameyamaliza vizuri sana.
(Makof)

Mheshimiwa Spika, la kwanza, tulikuwa na tatizo kubwa la maji pamoja na kwamba tunaishi karibu sana na maji. Kusema kweli amelisimamia vizuri, tulipata fedha zisizopungua shilingi bilioni 45, leo tatizo la maji kwa Musoma Mjini ni historia. Kazi iliyobaki ni kumalizia tu katika maeneo machache kwa maana ya usambazaji. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo tulimuomba wakati ule, tulikuwa na matatizo ya barabara, barabara zetu nyingi hazikuwa katika kiwango cha lami. Leo nafurahi na umpelekee salamu kwamba ameweza kutupatia fedha zisizopungua shilingi bilioni 13. Kwa hiyo, barabara zetu pale mjini nyingi sasa zipo kwa kiwango cha lami na hii ni ahadi aliyoitao yeye. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, ahadi ya tatu aliyoitao, tulikuwa na tatizo kubwa la Hospitali yetu ya Mkoa ambayo ilikuwa ni Hospitali yetu ya Rufaa ilijoengwa zaidi ya miaka 40 na ilikuwa imeshindikana kuisha. Mpaka hii leo ninavyoongea kwa mwaka jana peke yake kwenye hii bajeti ya mwisho aliweza kutupatia fedha zisizopungua shilingi bilioni 15. Leo kwa furaha niliyonayo ni kwamba katika mwaka huu kabla haujafika mwisho ile hospitali itaanza kutibu, ni Hospitali ya Rufaa ilikuwa imekaa kwa muda mrefu sana. Hayo ni baadhi ya mambo aliyokuwa ameyaahidi. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ilikuwa ni suala la uwanja wa ndege. Yeye aliahidi kukajitokeza kuwa na mchanganyiko pale lakini bahati nzuri limeisha, *tender* imetangazwa, Jumatatu tarehe 6 ile *tender* inafunguliwa.

Mheshimiwa Spika, nimwombe tu Mheshimiwa Waziri Mkuu ampelekee salamu kwamba ahadi zote zile alizokua amewaahidi watu wa Musoma, hatumdai hata moja. Tunachosubiri ni kumpa tu kura za kishindo ili aweze kuendelea katika *angle* nyingine. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kwa Musoma pale yapo tu matatizo madogomadogo sana. Moja ni hili tatizo la huu ugonjwa wa *Corona* sasa limefanya uchumi wa Musoma ume-*shrink* maana watu wengi sasa wanashindwa kuhangaika kwa sababu hasa ya hilo tatizo la ugonjwa wa *Corona*.

Mheshimiwa Spika, tatizo la pili ni miundombinu. Baada ya mvua kunyesha zile barabara zetu sasa siyo nzuri sana, nadhani hapo tu ndipo tuna changamoto kidogo ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, la tatu, ni suala la uchumi kwa ujumla hasa suala la ajira kwa vijana. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hili suala la ajira kwa vijana, kusema ukweli si Musoma peke yake, ni kwa nchi nzima. Sasa kwa sababu tupo hapa katika kushauri, nashauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kuna hili suala la bodaboda. Leo hii ukitembea katika vituo vingi vya Polisi, zipo pikipiki nydingi pale zimefungiwa na zilinunuliwa kwa fedha za kigeni. Ukiangalia kituo kimoja unakuta kina pikipiki 200 – 1,000 zinanyeshewa na mvua, zinaoza.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, ni kwa nini isiundwe Tume au Kamati wakawenza kupitia, wakaangalia zile pikipiki ambazo wenyewe nazo wanaweza kupigwa faini kidogo wakarudishiwa, watarudishiwa ili waendelee na maisha lakini hata zile ambazo zimeshindikana kuliko kuozea pale ni bora Serikali ingezitaifisha kwa maana ingezichukua halafu ikaziwa hiyo fedha ikarudi Serikalini kuliko ambavyo inapotea. Kwa hiyo, hilo ni la kwanza ambalo wala halitugharimu chochote katika kulitekeleza kuliko kuacha ile rasilimali kubwa inaendelea kupotelea pale.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo linahusiana na ajira ambalo ni kwa nchi nzima. Ushauri wangu, yapo maeneo matatu ambayo vijana wetu pale wanaweza wakaajiriwa na wakapata ajira kubwa; moja ni eneo la kilimo lakini la pili

ni eneo la mifugo. Ukienda kwenye kilimo, mifugo pamoja na uvuvi vijana wengi sana wanaweza wakapata ajira.

Mheshimiwa Spika, nichukue tu mfano kwa mkoa mmoja tu wa Mara na kama litaonekana linafaa tunaweza tukaifanya kwa nchi nzima. Napozungumzia haya maeneo matatu, leo timesoma pale kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, kila mwaka zaidi ya watoto milioni mbili wanaenda darasa la kwanza, tafsiri yake ni kwamba hao ndiyo wataenda mpaka chuo kikuu lakini wote hao mwisho wa yote ni kwamba wanategemea ajira.

Mheshimiwa Spika, sasa ajira zilizopo kwa sababu hazitoshi, huku kwenye kilimo, mifugo pamoja na uvuvi tunaweza kuwa-*accommodate* wengi kwa utaratibu ufuataao. Mimi nichukulle tu kwa mfano wa Mkoa wa Mara. Pale Mara tunayo maeneo, mfano tunalo eneo la Bugwema ambalo ni zuri sana kwa kilimo cha umwagiliaji, pale tu zipo zaidi ya ekari elfu kumi. Ukienda kule Bunda kuna eneo linaitwa Nyatwari zipo zaidi ya heka elfu tatu. Pia hata unapozungumzia habari ya mifugo, ukigusa kule Rorya kwa maana ya Uteji lipo shamba kubwa zaidi ya heka elfu ishirini kwa ajili ya mifugo. Ukienda kule Butiama kuna eneo linaitwa *Buhemba Holding Ground* kuna zaidi ya ekari elfu kumi mpaka elfu ishirini kwa ajili ya mifugo. Sasa nini kifanyike?

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba tulishaanza utaratibu mzuri wa JKT, tuchukue kila mwaka mfano kwa pale Mara vijana wasiopungua elfu tano tukawapeleka JKT wafundishwe kwanza ukakamavu lakini na ile *discipline* ya maisha wakitoka hapo tunawapeleka kama miaka isiyopungua miwili ambapo kazi kubwa chini ya uangalizi wa JKT watajifunza kilimo, habari ya mifugo, unenepeshaji wa mifugo na hata uvuvi wa kisasa. Matokeo yake ni kwamba wale vijana wakikaa pale miaka miwili chini ya JKT wakipata hayo mafunzo, siku wakiondoka hapo naamini Serikali itakuwa na mtaji wa kuwapa kwa sababu wao wenyewe wameutengeneza na wamejifunza na

kutokea hapo naamini kwamba sasa kijana ataondoka na si chini ya milioni kumi na ataenda kuanza maisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa utaratibu huo, ukipeleka watoto elfu tano ambapo ukawapa hiyo mitaji ambayo wameitengeneza wao wenyewe matokeo yake ni kwamba si chini ya watoto elfu tatu wataendelea na maisha yao vizuri. Wapo wachache ambaao maisha yatawashinda lakini kwa sababu wamelelewa kwenye yale mafunzo ya JKT maana yake wanajua muda, watajifunza ujasiriamali na mambo mengi sana.

Mheshimiwa Spika, hayo maeneo ninayoyazungumzia hayapo Mkoa wa Mara peke yake. Yapo kila mkoa maana bahati nzuri mimi katika mihangai yangu nimeweza kutembea katika mikoa mingi, kila mikoa inayo maeneo mengi ambayo yanaweza kuwasaidia.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Lucy Owenya, nakupa dakika 15 jitahidi uzitumie usizidishe.

MAELEZO BINAFSI YA MBUNGE

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, zitakuwa chini ya hapo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maelezo yangu binafsi yanayohusu wagonjwa wanaoishi na Virusi vya Ukimwi, (VVU) wapewe huduma za matibabu ya magonjwa nyemelezi bila malipo. Maelezo

haya yanatolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 28(8) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016.

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua kuwa tatizo la maambukizi ya UKIMWI duniani ni janga ambalo limeangamiza nguvu kazi kubwa ya Taifa na kuzima ndoto za maelfu ya watoto, vijana na hata wazee.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1983 nchi ya Tanzania waligundulika watu watatu wenye maambukizi ya VVU, ulipofika mwaka 1985 watu 140,000 waligundulika kuwa na maambukizi. Hii ni sawa na 1.3% ya waliokuwa na maambukizi kati ya umri wa miaka 15 mpaka 49.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1990 maambukizi yalipanda kufikia watu 900,000, sawa na 7.2% kwa wenye umri katil ya miaka 15 mpaka 49. Mwaka 2018 takriban watu wapatao milioni 1.6 waliishi na VVU nchini kiwango cha maambukizi kikiwa ni 4.6% kwa wenye umri wa miaka 15 mpaka 49 huku maambukizi mapya yakifikia takriban 72,000 na vifo vitokanavyo na UKIMWI vilifikia 24,000 wakati huo takriban 72% ya watu walioishi na VVU walikuwa wanatumia dawa za kufubaza virusi (*ARVs*), takriban 65% ya watoto wenye VVU walikuwa wanatumia *ARVs*.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa tafiti zinaonesha kila siku takriban watu 225 huambukizwa VVU na kati ya hao 90 ni vijana. Vijana wa kike ndiyo wahanga wakubwa kwa kuwa mabinti 72 kati ya umri wa miaka 15 mpaka 24 huambukizwa VVU kila siku. Maambukizi mapya kwa mwezi ni takriban 6,750 hii ikiwa ina maana kwamba kila saa watu tisa hupata maambukizi mapya. Takwimu hizi shirikishi zinatutaka kama Taifa kuwa na mikakati mahsusni na wa dharura wa kuangalia janga hili kwa mapana zaidi hasa tukizingatia nguvu kazi kubwa inayopotea.

Mheshimiwa Spika, huko mitaani kumekuwa na changamoto kubwa ya kupata elimu ya VVU. Elimu ya upatikanaji wa *ARVs* na elimu ya juu ya maambukizi ya VVU haipewi tena kipaumbele kama ilivyokuwa kwa miaka ya

nyuma. Mabango yenyе kubeba elimu ya UKIMWI hayaonekani tena kwenye sehemu za wazi kama ilivyokuwa kwa miaka ya nyuma. Matangazo ya vyombo mbalimbali vya habari yanayohusu ugonjwa huu hayapewi tena kipaumbele kama miaka ya nyuma. Hii ni pamoja na elimu mashulenі na vyuoni na hata taasisi mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vituo rafiki kwa vijana vinavyotoa elimu ya uzazi na malezi kwa vijana ni nadra kuvipata. Kamati za UKIMWI katika ngazi mbalimbali hazifanyi kazi kwa ufanisi. Makundi yenyе tabia hatarishi zinazochochea maambukizi ya VVU hayafikiwi kwa elimu na huduma. Hali hii inazidi kuchochea maambukizi mapya ya VVU na hatimaye vifo vitokanavyo na UKIMWI kuongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudи za Serikali za kupambana na hili janga ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI bado ugonjwa wa UKIMWI umeendelea kuwa tatizo kubwa nchini. Serikali inashauriwa kutenga fedha zaidi katika kupambana na ugonjwa huu hasa ukizingatia kuwa tatizo hili limezidi kuchochewa na uchovu wa wahisani (*Donor Phatic*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Serikali inagharimia dawa za kupunguza makali ya kufubaza VVU, magonjwa nyemelezi yamekuwa msumari wa moto kwa wenyе maambukizi. Matibabu ya magonjwa haya yanahitaji uchunguzi wa kina na wenyе għarama kubwa, mara nyingine matibabu huchukua muda mrefu au kujirudia rudia.

Mheshimiwa Spika, kundi kubwa la watu wenyе maambukizi hususan vijjjini mara nyingi hawazalishi ipasavyo kwa sababu ya hali zao kiafya, hivyo wengi wanaishi katika hali ya umaskini. Hali hii kupelekeea ulaji hafifu na kushindwa kumudu għarama kubwa za matibabu katika hospitali zetu na vituo vya afya na hatimaye kupelekeea vifo vya mara kwa mara vitokanavyo na magonjwa nyemelezi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na huduma zinazotolewa na Bima ya Taifa ya Afya vifurushi vya matibabu kwa njia ya

bima vimekuwa na gharama kubwa sana hasa kwa kundi hili ambalo kila mara wanasumbuliwa na maradhi. Kwa hali ya uchumi ilivyo na ihavyozidi kuwa ngumu ni dhahiri wengi wa wagonjwa wanashindwa kumudu gharama za matibabu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzito wa tatizo hili na gharama za matibabu kwa wenye maambukizi ya VVU ambao kila mara hukumbwa na magonjwa nyemelezi nashauri kuwa ni wakati muafaka Serikali kuridhia kutoa huduma za matibabu ya magonjwa nyemelezi bila malipo kwa kundi la wagonjwa wenye maambukizi ya VVU kwa wale wenye vitambulisho vya kuhudhuria kliniki za wanaoishi na VVU pale wanapohitaji matibabu kwenye zahanati, vituo vya afya au kwenye hospitali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, nchi kama Brazil na Argentina wamefanikiwa sana kupunguza maambukizi na vifo vinavyotokana na UKIMWI kutokana na uamuvi wa Serikali kutoa huduma za matibabu bila malipo kwa wenye maambukizi ya VVU. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kutoa matibabu bure siyo tu kutapunguza maambukizi bali kutachochaea hamasa zaidi ya watu wengi kwenda kupima hali ya maambukizi ya VVU na hatimaye kuanza matibabu stahiki kufuatana na majibu ya maabara. Pia vifo vitokanavyo na UKIMWI vitapungua kwani wenye VVU watakuwa wameanza dawa kwa wakati muafaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nazidi kusisitiza kuwa ni muhimu sana kwa Serikali kuanza kutoa huduma za matibabu bila malipo kwa wanaoishi na VVU na wanaosumbuliwa na magonjwa nyemelezi kama ambavyo nimeyatolea ufanuzi hapo awali ili kufikia malengo ya Serikali ya kupunguza maambukizi ifikapo 2030.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maelezo haya na kwa kuwa Serikali ipo hapa, nina imani kuwa watalifanyia kazi jambo hili na kuhakikisha kwamba

wote wenye magonjwa nyemelezi wanapewa dawa bure.
(Makofii)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofii)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lucy Owenya na hasa kwa kutumia muda vizuri zaidi, lakini pia hoja yako kwa kweli ni nzito, natumaini Serikali wataiangalia kwa uzito wake na iko siku kwa sababu bajeti zinaendelea kuja na pia Mheshimiwa Jenista hajahitimisha bado, huenda siku ya kuhitimisha akagusia kidogo jambo hili, pendekezo ambalo ni jema tu linajaribu kuangalia wale wote ambao wameweza kupatwa na janga hili la ugonjwa huu hatari.

Sasa nashukuru kwamba uchangiaji wetu umeenda vizuri mpaka sasa kwa kweli wengi wameweza kuchanglia na kesho ni Jumamosi, keshokutwa Jumapili, tutaendelea Jumatatu tarehe 6 ambapo kutakuwa na kuhitimisha nadhani jioni ile ya tarehe 6.

Waheshimiwa Wabunge mkiangalia mtaona kwamba kwenye ratiba yetu ya Bunge *weekends* haziko kwenye shughuli za Bunge, kwa hiyo tuna Jumamosi na Jumapili katika mwezi huu wa Nne kadhaa, siku ya Jumanne wiki ijayo tuna *Karume Day* halafu tutafanya kazi kama siku mbili Jumatano na Alhamisi, Ijumaa ya wiki inayofuata tunaanza Ijumaa Kuu Pasaka na kadhalika.

Sasa nimesema haya kwa maana ya kuwashauri kujituliza ikiwezekana wengi wenu mkabakia hapa Dodoma au basi kama mtasafiri ndiyo hivyo lakini kutosahau kwamba wakati huu ni wakati wa hatari ya janga la *corona*, kwa hiyo kufikiria kwenda kujichanganya changanya huko na nini msije mkaji-expose mkapata matatizo. Kama kuna mtu muhimu basi ni bora akasafiri hao muhimu wakaja wakakukuta hapa ukajaribu kuishi nao hapa Dodoma. Ni ushauri tu kwamba tunaviji-*weekend weekend* na vijisikukuu kadhaa katika mwezi huu wa Nne, ni vizuri kuwa na umakini kutumia muda

huu kwa kujaribu kuwa na watu wachache au mwenyewe mwenyewe kadri inavyowezekana.

Kama nilivyosema uchangiaji wetu umeenda vizuri, niendelee kutoa wito kwa wenzetu ambaa na hasa wote tu Waheshimiwa Wabunge mnapokuwa na mjadala unaopendekeza kubadili kitu fulani cha kikatiba ushauri wangu ni kwamba ni vizuri ukafanya *presentation* nzuri. Tena ni vizuri ukatumia dakika zako zote 10 kwenye hilo jambo kwa sababu kwa mazingira haya kwa vile hatuna Bunge Maalum la Katiba naamini wito mnaotoa wa badiliko la kitu chochote kwenye Katiba mnatoa kwenye Bunge hili kwa sababu kwenye mazingira fulani Bunge hili lina uwezo wa kubadili kipengele fulani cha katiba. Kwa hiyo nadhani inastahili unaposhusha kitu kinachohusiana na Katiba ukashuka vizuri watu wakakuelewa unaongelea nini au unataka kitu gani.

Waheshimiwa Wabunge niwape mfano, mtu anaweza kusema kwamba tunataka Bunge ndiyo liwe linateua na siyo Rais, sawa. Kwa mfano tu Bunge hili likakaa likakubali, kikaja hapa kipengele Mwanasheria Mkuu akatuletea, tukabadili Katiba ikasoma hivyo kwamba Bunge sasa ndiyo litakapokuwa linateua au linachagua vyovyote vile itakavyokuwa. Halafu tunajua *composition* ya Bunge letu, tukatangaza wagombee Wenyeiti na Mkurugenzi Mkuu akaomba Mwenyekiti huyu huyu aliyeko leo na Mkurugenzi huyu huyu aliyeko leo na Wabunge hawa hawa wakachagua kwamba huyu na huyu ndiyo wanafaa kuwa Wenyeiti wa Tume ya Uchaguzi *from there onwards* utaita huru si huru utaiitaje? Ndiyo maana nasema unapopendekeza kitu jipange, angalia *scenarios* na hivi vitu vya kubadili Katiba hatuvifanyi kwa uchaguzi unaokuja, tunavifanya kwa leo, kesho na keshokutwa hata kwa muda mrefu kidogo hadi wenzetu wengine nao watakapokuwa na fursa kama hizi za kuweza kufanya mabadiliko yoyote yale.

Pendekezo lolote halikataliwi lakini *at least* watu waelewe ni kitu gani unachotitaka. Nina hakika Wabunge wengi hapa ukienda naye hapo nje ukamuuliza hivi Tume huru inayoongelewa ikoje? Hawajui, mimi mwenyewe

ukiniuliza sijui tume huru inayoongelewa ni Tume gani? Nasema tena *it is not a crime* kusemea jambo hilo lakini inapendeza zaidi *when you stand, make us understand* ni kitu gani kinachoongelewa. Bahati nzuri bado Wizara ya Katiba na Sheria bajeti yake nayo inakuja huko mbele na bajeti nyingine ambazo labda nazo zinahusiana na mambo haya. Kwa hiyo tuna muda Jumatatu wa kuongelea, tuna muda wakati wa Katiba na Sheria na ndiyo mahali pake hasa ambayo nadhani ni siku mbili zile na kadhalika.

Hapa hapa pia niseme kuna mabadiliko ya ratiba yetu, naomba niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge kuwa ratiba ya Mkutano wa Kumi na Tisa imefanyika mabadiliko madogo ambapo Wizara ya Katiba na Sheria ambayo ilikuwa iwasilishe bajeti yake tarehe 20 Mei, tarehe 20 mwezi ujao mbali kabisa sasa tunaisogeza mbele inakuja tarehe 17 Aprili, 2020. Katiba na Sheria itakuwa tarehe 17 Aprili, narudia tena Katiba na Sheria itakuwa tarehe 17 Aprili.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu kwa utamaduni wetu wa Kibunge huwa tunaanza na bajeti ya Waziri Mkuu, halafu inakuja Ofisi ya Rais, halafu inakuja Ofisi ya Makamu wa Rais, halafu inakuja mhimili wa mahakama ambayo ni Katiba na Sheria, halafu zinifuata Wizara nyingine. Kwa hiyo watu wangu walijichanganya kidogo lakini tumeirudisha mahali pake kama ilivyotakiwa iwe. Kwa hiyo ni tarehe 17 mwezi huu huu, kwa hiyo *we have time* ya kuweza kujipanga na kushuka na vitu ambavyo vinaeleweka zaidi kuliko kukurupuka tu.

Jambo la pili alisema Mheshimiwa Lijualikali kwa uchungu natumaini na yeye amefanya *homework* yake labda kwamba mradi huu wa Serikali wa barabara umekwama kwa sababu ya kodi ya VAT. Endapo jambo hilo ni kweli basi sisi ushauri wetu tu kama meza ni kwamba tulipofanya mabadiliko yale ya Sheria ya VAT kuhusu misamaha, tulikuwa tunazingatia kwamba huko nyuma eneo hilo lilitumika vibaya. Kwa hiyo tukarekebisha tukaweka hivi ilivyo leo.

Waheshimiwa Wabunge, hata hivyo, kila marekebisho ya sheria huwa yana madhumuni na sababu, madhumuni na sababu ya Bunge hili kufanya marekebisho hayo haiwezi kuwa ilikuwa ni kwamba sasa tuwe na uguuumu mzungu kwa miradi ya Serikali, kwa *NGOs*, kwa binafsi kwa nini hizo hata kama kuna ukiritimba fulani na nini hizo hatuna neno, lakini kwa miradi ya Serikali yenyewe tulidhani kwamba madhumuni na sababu ya kutunga kumpa Waziri wa Fedha madaraka hayo kwa kweli ilikuwa ni kurahisisha, kwa miradi ya Serikali kama mambo yaweze kwenda haraka zaidi.

Sasa tunasikiasikia malalamiko ya hapa na pale kuhusu eneo hilo, sijui tatizo ni nini, nadhani Mwanasheria Mkuu ni vizuri mkaliangalia, kama bado kuna shida basi mtuletee tena bado tupo, kama kuna mabadiliko fulani ya kufanya ili *ku-speed up* kwa miradi ya Serikali, kwa vitu vya Serikali, utasikia *ambulance* za Serikali zimekwama bandarini sijui miezi sita na kadhalika si habari njema kwa sababu tunashangaa, mbona magari ya Serikali haya, *ambulance* ya Serikali, kwa nini inakaa miezi yote huko bandarini kuna nini? Unaambia *VAT*, sasa *VATimefanyaje*? Vitu vya namna hiyo, sitaki kutoa mifano, lakini kuna mifano miwili mitatu hivi, sasa endapo sheria yetu ile, mimi sijaisoma tena, ina shida basi Mwanasheria Mkuu jaribu kuiangalia.

Waheshimiwa Wabunge, tungependa sisi kama Bunge tu-*facilitate* Serikali kufanya kazi yake na siyo kwamba sisi tuwe tumetunga kitu cha kukwamisha Serikali isifanye kazi yake kwa miradi ya Serikali, kwamba iweze kwenda haraka iweze kwenda spidi, kwa vitu vya Serikali inatakiwa faili likifika leo kesho limetoka, kwa sababu ni mradi wa Serikali, kama ni mtu binafsi, kama ni Mashirika ya Dini, *NGOs* na kadhalika, hayo yafuate huo utaratibu mwingine wowote. Huu ndio ushauri wa jumla ambao ningependa kuutoa.

Basi Waheshimiwa Wabunge mimi ningependa kuwatakia *weekend* njema na Mheshimiwa Waziri Mkuu *weekend* njema ili Jumatatu tuje tuhitimishe hapa, Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri *weekend* njema, tunaona majaribio yetu yanaenda vizuri mpaka sasa

hivi, lakini kama nilivyosema tunaendelea kupokea ushauri wenu, pale ambapo mnadhani tunahitaji kuboresha na kurekebisha kwa namna tunavyoenda katika Mkutano wetu, *we still have time*, tutaendelea kurekebisha kadri tunavyoona inafaa kwa kushirikiana nanyi kujadiliana na kubadilishana mawazo.

Waheshimiwa Wabunge, basi kwa vile yote yaliyopangwa kufanyika kwa siku ya leo yamekamilika, sasa naona niahirishhe shughuli za Bunge hadi Jumatatu tarehe 6, saa nane kamili mchana.

(Saa 12.18 Jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu Tarehe 6 Aprili, 2020, Saa 8.00 Mchana)